Nipashe
MWANGA WA JAMII
Alhamisi Juni 6, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0579937
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper



## NSSF yajigamba ina uwezo kulipa wastaafu bila tatizo

UKURASA 3




UKURASA 13

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

**SEKTA SANAA CHACHU KATIKA PATO LA TAIFA**

SEKTA ya sanaa na burudani nchini, imekua kwa kasi kubwa na kuongoza katika kuchangia pato la taifa kwa asilimia 13.6...

UKURASA WA 8

**MAMA MARIA NYERERE AUGUA GHAFLA UGANDA**

MKE wa Baba wa taifa, Maria Nyerere (88), ameugua ghafla akiwa Uganda kuhudhuria ibada maalum ya kumbukumbu ya mashahidi wa Uganda eneo la Namugongo iliyofanyika Juni 3, mwaka huu...

UKURASA WA 26

**SHEIKH ATAKA WAHALIFU 'TELEZA' WAFICHULIWE**

SHEIKH wa Mkoa wa Kigoma, Hasan Kiburwa, amewataka wananchi wa mkoa huo kuhakikisha wanawafichua vijana ambao wanajipaka...

# Bajeti ofisi ya CAG yafyekwa

**YAPUNGUZWA** kwa bil. 7.8/- kulinganisha na mwaka 2018/19, mishahara, matumizi mengineyo vyapigwa panga... *Endelea uk. 2*



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akihutubia Baraza la Eid El Fitr jijini Tanga, jana. **PICHA: OWM**

# Waislamu wapewa somo kudumisha amani, upendo

UKURASA 2

## Bakita yaanza kuwanoa wasomi

UKURASA 24

**MICHEZO** YANGA YATOA NENO LIGI YA MABINGWA UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6




Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, akihutubia Baraza la Eid El Fitr katika ukumbi wa Sheikh Idrissa Abdulwakil Kikwajuni Zanzibar jana. **PICHA: IKULU ZANZIBAR** .

# Bajeti Ofisi ya CAG yafyekwa

**Na Sanula Athanas,**
DODOMA

MAKADIRIO ya matumizi ya fedha katika Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka ujao wa fedha yamepunguzwa kwa Sh. bilioni 7.791 kulinganishwa na ya mwaka huu.

Kwenye ukurasa wa 175 wa kitabu cha hotuba ya makadirio ya bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka ujao wa fedha, inabainishwa kuwa kwa mwaka ujao, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inatarajiwa kutumia jumla ya Sh. bilioni 61.377.

Kati yake, Sh. bilioni 55.077 ni matumizi ya kawaida (mishahara Sh. bilioni 14.084) na matumizi mengineyo Sh. bilioni 40.993) na Sh. bilioni 6.3 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Makadirio hayo yaliwasilishwa bungeni jijini Dodoma Jumatatu na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango na kuidhinishwa na Bunge siku hiyo hiyo.

Kwa mwaka huu wa fedha (2018/19), Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ambayo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ni mkuu wake, iliidhinishiwa na Bunge matumizi ya Sh. bilioni 69.106.

Kati yake, Sh. bilioni 55.394 zilikuwa za matumizi ya kawaida (mishahara Sh. bilioni 16.648 na matumizi mengineyo Sh. bilioni 38.746) na Sh. bilioni 13.712 zilikuwa za miradi ya maendeleo.

Hata hivyo, katika hotuba yake hiyo, Waziri Mpango, hajaeleza sababu za kupunguzwa kwa makadirio ya matumizi katika ofisi hiyo.

Akiwasilisha hotuba yake bungeni Jumatatu, Dk. Mpango aliliambia Bunge kuwa katika mwaka ujao wa fedha, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi itaendelea kuimarisha ukaguzi wa mapato na matumizi ya serikali kwa lengo la kuimarisha uwajibikaji na uwazi kwenye matumizi ya rasilimali za umma.

Katika kufikia malengo hayo, waziri huyo alisema ofisi imepanga kutekeleza vipaumbele vinane ikiwa ni pamoja na kufanya ukaguzi wa mafungu ya mapato na matumizi ya wizara, idara za serikali zinazojitegemea, wakala na taasisi za serikali, sekretarieati za mikoa, mamlaka za serikali za mitaa katika mikoa yote nchini na mashirika ya umma.

Alisema Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi pia itakagua miradi ya maendeleo inayofadhiliwa na wahisani, ifanye ukaguzi wa kiufundi kwenye maeneo yenye uwekezaji mkubwa wa rasilimali za umma kama vile ujenzi wa barabara na viwanja vya ndege, reli ya kisasa na miradi ya nishati (umeme).

# Waislamu wapewa somo kudumisha amani, upendo

**Na Waandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amewataka Waislamu nchini kuendelea kudumisha amani na upendo wakati wote hata baada ya mfungo kumalizika, kwa kuwa kufanya hivyo ni chachu ya maendeleo na kukuza umoja wa kitaifa.

Alitoa rai hiyo jana alipokuwa akihutubia Baraza la Eid El Fitri kitaifa lililofanyika mkoani Tanga, na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali, dini, na wabunge na makundi mbalimbali ya jamii.

Waziri Mkuu Majaliwa aliwataka Waislamu nchini kuendeleza mambo mema waliyokuwa wakiyafanya wakati wakiwa katika mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, ikiwamo kuwakumbuka watu wenye dhiki.

"Tumeonesha moyo wa upendo na usafi wakati tulipokuwa kwenye mfungo, ninawaomba muendeleze yale yote mema mliyokuwa mnayafanya, dumisheni amani, muwe na umoja na mshikamano," alisema Majaliwa.

Waziri Mkuu Majaliwa pia alilitaka Baraza la Waislamu Tanzania (Bakwata) kuendelea kusambaza huduma muhimu za elimu, afya na maji kwenye kila pembe ya nchi, ili kila Mtanzania anufaike.

**WITO TAASISI ZOTE ZA DINI**

Kadhalika, Waziri Mkuu Majaliwa alizitaka dini nchini kushiriki katika mapambano mbalimbali ambayo serikali imeanzisha ikiwamo mapambano dhidi ya Ukimwi na VVU, kwa kuwataka viongozi wa dini kuzungumza na waumini wao mara kwa mara.

"Ni muhimu viongozi wa dini nchini mkazungumzia suala la maambukizi wa ugonjwa wa Ukimwi, kwani umekuwa ukimaliza nguvu kazi ya taifa, ugonjwa huu hauna tiba wala chanjo, tushirikiane kwa pamoja kuokoa nguvu kazi ya taifa inayopotea," alisema Majaliwa.

Waziri Mkuu Majaliwa aliwataka Watanzania kuacha tabia ya kutegemea vipimo vya wenza wao kwa kuogopa kwenda kupima ugonjwa huo.

**MAPAMBANO YA RUSHWA**

Vilevile, Majaliwa aliwataka viongozi wa dini kushirikiana na serikali katika mapambano dhidi ya rushwa na usafi wa mazingira, kwamba maendeleo ya nchi yatakuja endapo jamii ikiacha tabia ya kutoa na kupokea rushwa.

Pia, aliwataka viongozi wa dini nchini kushiriki katika kampeni zinazoanzishwa na serikali ili kuleta maendeleo, akitoa mfano wa kampeni ya kupiga marufuku

INAENDELEA UK. 8

# Ukuaji sekta ya sanaa wapaisha pato la taifa

**Na Salome Kitomari**

SEKTA ya sanaa na burudani nchini, imekua kwa kasi kubwa na kuongoza katika kuchangia pato la taifa kwa asilimia 13.6.

Kwa mujibu wa hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango iliyowasilishwa bungeni na Waziri, Dk. Philip Mpango, sekta hiyo na ya habari na mawasiliano zimeendelea kufanya vizuri na kukua kwa kasi.

Sekta hizo zipo chini ya Wizara ya Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo chini ya Waziri Dk. Harrison Mwakyembe.

uchumi wa nchi umeendelea kuimarika na mwaka 2018, pato la taifa kwa kutumia bei ya kizio ya mwaka 2015 lilikua kwa asilimia 7.0 ikilinganishwa na asilimia 6.8 mwaka 2017.

"Sekta zilizokua kwa kasi kubwa na viwango vyake kwenye mabano ni pamoja na sanaa na burudani (asilimia 13.7), ujenzi (asilimia 12.9), usafirishaji na uhifadhi mizigo (asilimia 11.8) na habari na mawasiliano (asilimia 9.1)," alisema.

Waziri Mpango alisema ukuaji wa uchumi umeenda sambamba na utolewaji wa huduma bora kwa wananchi zikiwamo maji, afya, umeme, elimu na ujenzi wa miundombinu ya reli, bandari, viwanja vya ndege, madaraja na barabara pamoja na kuimarisha usafiri wa anga.

Alisema mfumuko wa bei umeendelea kushuka na kubakia katika kiwango cha tarakimu moja na kwamba mwezi Aprili 2019, mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 3.2 ikilinganishwa na asilimia 3.8 kwa kipindi kama hicho cha mwaka 2018.

Alisema malengo ya uchumi jumla kwa mwaka 2018/19 yalikuwa ni kuhakikisha pato la taifa linakua kwa asilimia 7.2 mwaka 2018, mfumuko wa bei unabaki katika wigo wa tarakimu moja, mapato ya ndani yanafikia asilimia 15.8 ya pato la taifa na mapato ya 4 kodi yanafikia asilimia 13.6 ya pato la taifa na nakisi ya bajeti inafikia asilimia 3.2.



# UN yaifagilia Tanzania mifuko plastiki

**Na Elizabeth Zaya**

UMOJA wa Mataifa (UN), umeunga mkono na kuipongeza serikali ya Tanzania kwa kufanikiwa kwa kiwango kikubwa kuzuia matumizi ya mifuko ya plastiki.

Mratibu Mkazi wa UN, Alvaro Rodriguez, alisema hayo wakati wa kuadhimisha Siku ya Mazingira Duniani ambayo hufanyika Juni 5 kila mwaka, na kwamba wanasikia fahari kubwa kuipongeza Tanzania kwa hatua hiyo kubwa kwa sababu mifuko hiyo imekuwa miongoni mwa vitu ambavyo vimekuwa vikichafua hewa.

Alisema asilimia 90 ya mifuko ya plastiki huishia baharini na kuathiri viumbe vilivyopo humo wakiwamo samaki ambao ni tegemeo kubwa kwa chakula.

Alisema zipo nchi nyingi ambazo zilijiwekea mipango ya kutokomeza mifuko hiyo, lakini hazikuweza kufikia mafanikio kama ambayo yamefikiwa na Tanzania na kuiomba kuendeleza juhudi hizo ikiwamo kuwekeza nguvu zaidi katika utoaji wa elimu juu ya madhara yake.

"Katika kuadhimisha siku ya mazingira duniani, sisi UN tunaipongeza kwa dhati Tanzania, tunaona imefanikiwa kwa kiwango kikubwa japokuwa ndio imeanza utekelezaji wake kupiga marufuku mifuko hii...tunaamini kwamba kadri elimu itakavyozidi kutolewa, Watanzania watazidi kuelewa zaidi na wataishukuru serikali yao kwa hatua hiyo," alisema Rodriguez.

Alieleza kuwa wameamua kuadhimisha siku hiyo Jumamosi kutokana na kuingiliana na sikukuu ya Idd-el-Fitr ili kutoa fursa kwa watu wengi kushiriki.

Mchumi kutoka shirika la Afya Duniani (WHO), Maxmillian Mapunda, alisema uchafuzi wa hewa huchangia magonjwa mbalimbali ikiwamo shambulizi la moyo, saratani na kuathiri viungo vya mwili.

# NSSF: Hatuna tatizo kulipa mafao

**Na Salome Kitomari**

MFUKO wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), umesema hauna tatizo la fedha la kulipa pensheni, mafao mbalimbali na kugharamia shughuli za uendeshaji.

Akizungumza na Nipashe katika mahojiano maalum, Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, William Erio, alisema fedha zilizopo benki ni zaidi ya Sh. bilioni 741.8.

Alisema mfuko umelipa mafao ya aina mbalimbali yenye thamani ya Sh. bilioni 294.8 kati ya Julai mwaka jana hadi Machi mwaka huu.

Alisema wanufaika wa mafao hayo ni 57,572 na kwamba kwa mwezi Aprili mwaka huu, NSSF imelipa zaidi ya Sh. bilioni 13.7 kwa wanachama 19,335.

Kwa mujibu wa Erio, kwa mwezi Mei wamelipa pensheni ya kila mwezi na fao la kutokuwa na ajira zaidi ya Sh. bilioni 5.8.

"Ni dhahiri kwamba fedha tulizonayo benki na ambayo tumelipa kwa wanachama wetu inatoa jibu kuwa NSSF haina tatizo la fedha, kwa kuwa tumelipa fedha nyingi kiasi hicho na bado tuna fedha benki," alisema.

**Fao la upotevu wa ajira siku 14**

Aprili mwaka huu, Mkurugezi huyo alizungumza na Nipashe na kueleza kuwa ulipaji wa mafao ya ukosefu wa ajira unafanyika ndani ya siku 14 iwapo mwanachama amekamilisha nyaraka zote.

Aidha, katika ukaguzi wa nyaraka za waombaji wa fao la upotevu wa ajira kwa kipindi cha Januari hadi Machi, maombi 880 yenye madai ya Sh. bilioni 8.8 yalibainika kuwa feki.

Alisema utaratibu unaelekeza kuwa ndani ya siku 30 mwanachama awe ameanza kulipwa, lakini wameamua kurahisisha ili kuondoa usumbufu kwa wanachama.

Alisema changamoto kubwa ni wanachama kudanganya kuwa wameachishwa kazi na ndani ya muda mfupi kupata kazi, na kutaka kulipwa fao la upotevu wa ajira.

"NSSF tumejiwekea utaratibu wa kulipa fao la ukosefu wa ajira ndani ya siku 14 baada ya mhusika kuwasilisha nyaraka zote muhimu, ikiwamo mwajiri kupeleka michango yote kwa wakati, lakini utaratibu wa kisheria ni siku 30," alisema Erio.

**Fao la kujitoa**

Erio alisema kisheria hakuna fao la kujitoa kwa kuwa mafao yameainishwa kwenye sheria na kanuni zinazoongoza mifuko hiyo.

"Kwa mujibu wa sheria zetu hakuna fao la kujitoa na mabadiliko ya sheria mwaka jana, fao lililopo ni la upotevu wa ajira ambalo linalipwa asilimia 33.3 ya mshahara wa mwanachama," alifafanua.

Alisema fao la upotevu wa ajira limegawanyika kwenye makundi mawili kwa waliokuwa wanafanyakazi ambazo siyo za kitaaluma kutokana na elimu zao na aina ya kazi zao, lakini kwa wenye kazi za kitaaluma wanalipwa fao la upotevu wa ajira kwa muda wa miezi sita.

"Kwa waliokuwa wanafanyakazi ambazo siyo za kitaaluma mfano vibarua, wabeba zege na kazi za muda mfupi, wao wanalipwa fedha zao zote wanavyoondoka. Hizi zinaendelea kulipwa na makundi yote yanalipwa asipokuwa wenye taaluma," alisema.

**Kikokotoo**

Alisema kikokotoo kinachotumika kulipa wanachama kwa mkupuo ni asilimia 25 ambayo iko kwa mujibu wa Sheria ya NSSF.

**Mafao yanayotolewa**

Kwa mujibu wa Sheria ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2018, kuna jumla ya mafao saba ambayo manne ni ya muda mfupi likiwamo la upotevu wa ajira, ugonjwa, uzazi na mkopo wa nyumba.

Mafao ya muda mrefu ni pensheni ya uzeeni, fao la ulemavu na fao la warithi.



Wachuuzi wa mifuko mbadala, wakiendelea na shughuli zao katika Mtaa wa Congo, Kariakoo, jijini Dar es Salaam jana, bila ya kuwa na vitambulisho vya biashara vilivyotolewa na Rais John Magufuli. **PICHA: JOHN BADI**

# Maelekezo ya JPM kwa ma-DAS, Makatibu Tarafa

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli, amewataka Makatibu Tawala wa Wilaya zote na Maofisa Tarafa wa Tarafa zote nchini kufanya kazi kwa kujiamini, kuzingatia sheria na taratibu na kusimamia kwa karibu miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika maeneo yao ya kazi.

Rais Magufuli aliwapa maelekezo hayo juzi alipokutana na viongozi hao Ikulu jijini Dar es Salaam.

Katika mkutano huo ambao ulihudhuriwa na Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, Rais Magufuli aliwataka viongozi hao kujenga utaratibu wa kuwatembelea, kuwasikiliza na kutatua kero na migogoro mbalimbali inayowakabili wananchi pamoja na kuchukua hatua pale ambapo mambo hayaendi sawa.

Miongoni mwa mambo hayo ni utekelezaji mbaya wa miradi kama ya ujenzi wa majengo ya Serikali, barabara, miradi ya maji na mingine.

Aliwataka Makatibu Tawala kutambua nafasi walizonazo Maofisa Tarafa na wote kufanya kazi kwa ushirikiano badala ya Maofisa Tarafa kugeuzwa kuwa wasaidizi wa Makatibu Tawala wa Wilaya ili majukumu ya Serikali yaliyopo katika maeneo hayo yatekelezwe kwa mafanikio na ufanisi mkubwa.

Rais Magufuli aliongeza kuwa hataraji kuona Ofisa Tarafa anajihusisha na vitendo vya ukiukaji wa maadili na utovu wa nidhamu au hafuatilia utekelezaji wa miradi mikubwa iliyopo ama inayopita katika eneo lake kwa kuwa kufanya hivyo kutakuwa kunadhihirisha kuwa haimudu kazi hiyo.

Aidha, aliwataka viongozi hao kutambua mipaka ya kazi yao, kusimamia vizuri ukusanyaji wa mapato, kusimamia kwa ukaribu utoaji wa vitambulisho vya wajasiriamali wadogo, kuhamasisha watu kufanya kazi za uzalishaji mali, kusimamia ulinzi na usalama, kukomesha wizi na ufisadi wa mali za umma na kuyatangaza mafanikio ya Serikali yao ili kuwapa matumaini wananchi.

Kabla ya kuzungumza na viongozi hao, Rais Magufuli alisikiliza maoni na changamoto mbalimbali kutoka kwa viongozi hao ambapo aliahidi kuwa Serikali itatoa Sh. bilioni moja kwa ajili ya kuwanunulia pikipiki Maafisa Tarafa 399 ambao hawajapata mgawo wa pikipiki na pia alimuagiza Waziri na Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) kuondoa sharti la kutopandishwa cheo kwa Ofisa Tarafa ambaye hajapatiwa mafunzo mafupi ya utumishi.

"Maafisa Tarafa wenye pikipiki ni 171 na wasio na pikipiki ni 399, kwa hiyo nimeamua kutoa maelekezo zinunuliwe pikipiki kwa wote ambao hawana pikipiki, lakini nawasihi sana mtumie vyombo hivyo kwa uangalifu, isije ikawa ndio chanzo cha kuwapa ulemavu," alisema Rais Magufuli.

Rais Magufuli aliwapongeza Maafisa

INAENDELEA UK. 5

HABARI KITAIFA

# Leseni mpya 700 michezo ya kubahatisha zatolewa miezi 10

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

HUKU kukiwa na pendekezo la kuzuia michezo ya kubahatisha nchini, serikali imebainisha kuwa katika kipindi cha miezi 10 ya mwaka huu wa fedha, imetoa leseni 2,062 za michezo hiyo huku 779 zikiwa ni mpya.

Katika ukurasa wa 89 wa kitabu cha hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka ujao wa fedha, inaelezwa kuwa kwa mwaka huu, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha ilipanga kusimamia na kutoa leseni 2,500 za michezo ya kubahatisha na kuhakikisha inaendeshwa kwa mujibu wa sheria.

Hotuba hiyo iliwasilishwa bungeni jijini Dodoma Jumatatu na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango.

Katika hotuba yake hiyo, Waziri Mpango anabainisha kuwa bodi hiyo pia ilipanga kuanzisha mfumo wa kielektroniki wa kusimamia michezo hiyo ujulikanao kama Regulator Central Monitoring System (RCEMS).

"Hadi kufikia Aprili mwaka huu, bodi imefanikiwa kutoa jumla ya leseni 2,062 sawa na asilimia 82.48 ya lengo. Idadi hii inajumuisha leseni mpya 779 na leseni zilizohuishwa 1,283," Dk. Mpango anabainisha.

Kwa mujibu wa waziri huyo, katika kipindi hicho cha miezi 10, bodi ilifanikiwa kukusanya jumla ya Sh. bilioni 3.7 ikiwa ni ada ya leseni, sawa na asilimia 64 ya lengo la kukusanya Sh. bilioni 6.8.

"Bodi pia ilifanya ukaguzi kwa waendeshaji wa michezo ya kubahatisha 53 nchini kwa lengo la kuhakikisha michezo hiyo inaendeshwa kwa kuzingatia matakwa ya sheria ya michezo hiyo pamoja na sheria nyingine za nchi.

"Katika ukaguzi huo, bodi haikubaini ukiukwaji mkubwa wa sheria kwa waendeshaji wenye leseni. Hata hivyo, bodi ilibaini baadhi ya wafanyabiashara kuendesha biashara ya michezo ya kubahatisha bila leseni na ilichukua hatua kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za nchi," Dk. Mpango anaeleza katika hotuba yake hiyo.

Pia alibainisha kuwa kwa mwaka ujao wa fedha, bodi hiyo itaendelea kuratibu na kudhibiti matangazo ya michezo ya kubahatisha ili kuepuka ushawishi wa kupitiliza.

BIL. 78/-, AJIRA 20,000

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha nchini, James Mbalwe, alisema jijini Dar es Salaam mwezi uliopita kuwa michezo ya kubahatisha ilichangia Hazina ya Serikali kwa Sh. bilioni 78 katika mwaka wa wa fedha uliopita (2017/18) na kwamba mwaka huu wa fedha, sekta hiyo inakadiriwa kuchangia zaidi ya Sh. bilioni 96.

"Kwa hiyo, sekta hii ikisimamiwa vizuri, inaweza kutoa mchango mkubwa kwenye uchumi wa nchi yetu," Mbalwe alisema.

Mbali na mapato hayo ya mabilioni ya shilingi, kiongozi huyo wa bodi alisema kampuni mbalimbali za michezo hiyo zimewekeza mabilioni ya shilingi kama mtaji.

Alisema Watanzania takribani 20,000 pia wamepata ajira za moja kwa moja kutoka kwenye kampuni zinazoendesha michezo hiyo nchini.

**PENDEKEZO KUIFUTA**

Hivi karibuni, baadhi ya wadau wakiwamo viongozi wa dini, walishauri serikali ipige marufuku michezo ya kubahatisha nchini kwa madai kuwa inachochea uvivu miongoni mwa vijana.

Tayari serikali ya Uganda imeshatangaza kuzuia michezo hiyo nchini mwake, ikibainisha kuwa wale wenye leseni za kuiendesha hawataongezwa muda baada ya muda wa leseni zao kufika kikomo.



Lundo la takataka likiwa limetelekezwa katika kituo cha daladala cha magomeni Mwambechai, jijini Dar es Salaam jana na kusababisha usumbufu kwa abiria na wakazi wa eneo hilo. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Nyalandu: Chadema itashinda majimbo yote Singida 2020

**Na Enock Charles**

Kada wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Lazaro Nyalandu, amedai kuwa mwaka 2020, chama hicho kitarejesha majimbo yote ya Mkoa wa Singida ikiwamo jimbo alilokuwa akiliongoza la Singida Kaskazini.

Akizungumza katika Kijiji cha Ikungi mkoani Singida wiki iliyopita, kada huyo alisema kutokana na kazi ya kujenga chama katika mkakati maalum unaofahamika katika chama hicho kama 'Chadema ni msingi, chama hicho kitaibuka na ushindi katika majimbo yote ya mkoa wa Singida.

"Kama vile huu mkoa wa Singida ulivyokuwa na watu wawili maarufu yupo Tundu Lissu na yupo Nyalandu, sasa timu hii inacheza moja ,tutaichukua Singida Mashariki tena, tutaichukua Singida Kaskazini kwa mara ya kwanza ,tutashinda Singida Magharibi, majimbo yote mawili ya Iramba na Itigi", Nyalandu alisema.

Kada huyo wa Chadema ambaye pia aliwahi kuwa mbunge wa Singida Kaskazini na Waziri wa Maliasili na Utalii katika Serikali ya awamu ya nne, hivi karibuni alikamatwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) na wenzake wawili akituhumiwa kwa rushwa na mikutano iliyokatazwa na Serikali.

## PM awataka wazazi kuzingatia mafundisho ya dini kwa watoto

**Na Romana Mallya**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amewataka wazazi na walezi kuwaongoza watoto wao kwa kuwapa mafundisho ya dini yatakayowawezesha kumjua Mungu na kuwa raia wema.

Majaliwa aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati aliposhiriki swala ya Eid El Fitr, iliyofanyika katika Msikiti wa Anwar uliopo

INAENDELEA UK. 5


Jipatie Maji ya Kunywa ya Kilimanjaro kwa Bei Elekezi za Rejareja kama Ifuatavyo:-

- Nusu Lita (500ml) – TSHS. 500/=
- Lita Moja na Nusu (1.5L) – TSHS. 1,000/=
- Bei Hizi Elekezi ni Kwa Nchi Nzima
- Maji ya Kunywa ya Kilimanjaro ni Maji ya Kuaminika Kila Siku




215227501

## HABARI KITAIFA

# 57 washindwa kurejesha fomu udiwani

**Na Romana Mallya**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imesema kati ya wanachama 98 waliochukua fomu za uteuzi wa kugombea uchaguzi mdogo wa udiwani kata 32 Tanzania Bara, ambao hawajazirejesha hadi mwisho wa uteuzi ni 57.

Kwa mujibu wa taarifa ya Mkurugenzi wa NEC, Dk. Athumani Kihamia, iliyotolewa juzi, jumla ya wanachama 98 walichukua fomu hizo na hadi mwisho wa uteuzi ambao ulikuwa Mei 31, wanachama 41 ndiyo waliozirejesha na walioteuliwa ni 27.

Dk. Kihamia alisema wanachama 27 ndiyo walikidhi vigezo na kuteuliwa kuwa wagombea na kupita bila kupingwa kutokana na kuteuliwa kwa mgombea mmoja kwa kila kata.

"Katika kata hizo 32, jumla ya wagombea 98 kutoka katika vyama 14 vya siasa walishiriki kuchukua fomu za uteuzi. Vyama hivyo ni AAFP, UMD, ADA - TADEA, CCK, CCM, Chadema, CUF, Demokrasia Makini, NCCR - Mageuzi, NRA, SAU, TLP, UDP na UPDP," alisema.

Pia alisema wanachama wengine watano hawakuteuliwa kuwa wagombea kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kurejesha fomu hizo nje ya muda, kukosa uthibitisho wa malipo ya dhamana na wagombea kuwa na idadi pungufu ya wadhamini.

"Jumla ya wagombea watano wa nafasi ya udiwani waliwekewa pingamizi kwa Msimamizi wa Uchaguzi na hivyo kusababisha wagombea wawili kuenguliwa kutoka katika orodha ya wagombea," alisema.

Dk. Kihamia alisema kuwa NEC ilipokea rufaa moja kutoka kwa mgombea udiwani wa kata ya Ipole iliyopo Halmashauri ya Wilaya Sikonge kupitia CUF na malalamiko kutoka kwa wagombea wa Chadema na CUF katika kata ya Murangi iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Musoma.

"Malalamiko yao ni dhidi ya maamuzi ya Wasimamizi wa Uchaguzi kuwaondoa kwenye

INAENDELEA UK. 8

# Serikali yaanika sababu za kuunganisha mashirika ya umma

## ●Benki tatu zaunganishwa

**Na Sanula Athanas, DODOMA**

SERIKALI imelieleza Bunge sababu nne za kuunganisha mashirika ya umma na kubainisha kuwa tayari mashirika 15 yameunganishwa ili kubaki na mashirika sita.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, alieleza sababu hizo bungeni jijini Dodoma Jumatatu alipowasilisha hotuba kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka ujao wa fedha.

Alisema lengo kuu la kuunganisha mashirika na taasisi za umma ni kuongeza ufanisi katika utendaji, kuondoa mwingiliano wa majukumu, kupunguza gharama za uendeshaji na kungeza tija.

Dk. Mpango alisema wizara kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina, imeendelea kufanya uchambuzi wa miundo na mgawanyo wa majukumu ya taasisi na mashirika ya umma na hadi kufikia Aprili mwaka huu, jumla ya taasisi na mashirika 60 yalikuwa yamechambuliwa.

Alibainisha kuwa kati yake, taasisi na mashirika 54 miundo yake imeidhinishwa na Rais na imewasilishwa kwa taasisi na mashirika husika kwa ajili ya utekelezaji na miundo ya taasisi na mashirika sita iko katika hatua ya kupata idhini.

"Utekelezaji wa zoezi hili umeenda sambamba na uunganishaji wa mashirika ya umma 15 na kubaki mashirika sita," Dk Mpango alibainisha.

Waziri huyo alisema mashirika yaiyounganishwa ni pamoja na mifuko ya hifadhi ya jamii; GEPF, LAPF, PPF na PSPF ambayo iliunganishwa kuunda Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF).

Mashirika mengine ya umma yaliyoguswa na uchambuzi huo ni Mamlaka za Maji (Dawasa na Dawasco) zilizounganishwa kuunda Dawasa, UTT-MFI na SELF-Microfinance kuunda SELF Microfinance na UTT-PID na UTT-AMIS kuunda UTT-AMIS.

Kwa upande wa taasisi za fedha, Dk. Mpango alisema Benki ya Wanawake Tanzania, Benki ya Twiga na Benki ya Posta zimeunganishwa kuunda Benki ya TPB.



Watoto wa Kituo cha kulelea watoto yatima Chakuwama, kilichopo Sinza, jijini Dar es Salaam, wakipokea msaada wa vitu mbalimbali zikiwemo nguo kwa ajili ya sikukuu ya Eid el Fitr, kutoka kwa Mmiliki wa First Super Market, Devotha David, ambaye naye ni yatima, katika hafla iliyofanyika kituoni hapo jana. **PICHA: ROMANA MALLYA**

# Maelekezo ya JPM kwa ma-DAS, Makatibu Tarafa

INATOKA UK. 3

Tarafa wote wanaofanya kazi vizuri na kwa ushirikiano na watumishi wenzao wa umma waliopo katika maeneo yao, na kufuatia utendaji kazi mzuri wa Mtendaji wa Kata ya Engarenaibor Wilaya ya Longido mkoani Arusha, Thomas Ngobei, ameagiza apandishwe cheo na kuwa Ofisa Tarafa.

Wakitoa maoni na changamoto zao, Maofisa Tarafa hao walimpongeza Rais Magufuli kwa juhudi kubwa zilizofanywa na Serikali yake katika kuwahudumia wananchi na walimhakikishia kuwa wapo tayari kuchapa kazi kwa juhudi na maarifa na kusimamia kwa ukaribu miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika maeneo yao.

Waziri wa Utumishi na Utawala Bora, Mhe. George Mkuchika, Waziri wa Tamisemi, Selemani Jafo na Katibu Mkuu wa Utumishi, Dk. Laurian Ndumbaro, walimpongeza Rais Magufuli kwa kuandika historia ya kuwa Rais wa kwanza kukutana na Maofisa Tarafa wa nchi nzima na waliwataka Maofisa Tarafa hao kufanya kazi kwa kuzingatia miiko yao ya utumishi, kuleta tija na kutekeleza maelekezo yanayotolewa na viongozi wakuu.

Samia na Majaliwa waliwataka Maofisa Tarafa hao kujenga uhusiano mzuri na watumishi wengine wa umma, kutoa taarifa ya yanayotokea katika maeneo yao na kufanya kazi kwa kutanguliza uzalendo na mshikamano wa Taifa.




# PM awataka wazazi kuzingatia mafundisho ya dini kwa watoto

INATOKA UK.4

Msasani, jijini Dar es Salaam.

Katika swala hiyo, Waziri Mkuu aliwataka Waislamu wote watumie Sikukuu ya Eid el Fitr kutenda matendo mema na kuwakumbuka wajane na yatima.

"Wakati huu ni mzuri wa kuimarisha mshikamano miongoni mwenu na madhehebu mengine. Hakikisheni mnayaendeleza mambo mema yote, tumeona utulivu uliojitokeza katika mwezi mtukufu, na jambo hili limesisitizwa na viongozi wa dini, Tuendelee kuwa wamoja tuimarishe mshikamano na tuvumiliane," alisema.

Naye, Imamu wa msikiti huo, Sheikh Mhina, alisema Waislamu wanatakiwa kutumia siku hiyo kwa kuhamasisha amani pamoja na kuwasaidia watu wasiokuwa na uwezo.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## HESLB hongera kwa kujiboresha

**BODI** ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), imetoa mwongozo wa utoaji mikopo kwa mwaka wa masomo 2019/2020 unaotaja sifa, vigezo na utaratibu wa kuwasilisha maombi ya mikopo ya elimu ya juu

Hatua hii kwa hakika ni ya kupongeza. Kwa kuwa mwongozo pia umeandaliwa katika lugha za Kiingereza na Kiswahili na kuuweka katika tovuti ya HESLB ambayo ni www.heslb.go.tz inalenga kuwawezesha waombaji au wazazi ambapo wengine hawajui lugha ya Kiingereza sasa wataupata kwa urahisi na kujisomea hivyo kupunguza au kuondoa kabisa usumbufu wa kulazimika kufika kwenye ofisi hizo.

Pamoja na mwongozo huo HESLB wameandaa kitabu chenye maswali na majibu yanayoelekeza namna ya kuomba mkopo kwa lugha ya kiswahili ambacho pia kinapatikana kwenye tovuti yao, hivyo tunaamini kwamba idadi ya waliokosa mikopo kutokana na kukosea kujaza fomu kwa kukosa mwongozo itapungua sasa.

Wameweka wazi nyaraka muhimu zinazotakiwa ikiwa ni pamoja na vyeti vya kuzaliwa ambavyo vimethibitishwa na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) au Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar (ZCSRA). Aidha, kwa waombaji mikopo ambao wazazi wao wamefariki dunia, watatakiwa kuwa na nakala za vyeti vya vifo ambavyo vimethibitishwa na RITA au ZCSRA.

Mambo hayo yatapunguza usumbufu kwa waombaji wa mikopo hiyo kwa kuwa watapata nafasi ya kujiandaa kabla ya kuanza kujaza fomu za kuiomba.

Tunawapongeza viongozi wa HESLB chini ya Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB Abdul-Razaq Badru

kwa usikivu kwani wamebainisha wazi kuwa baadhi ya maboresho wameyafanya baada ya kupokea maoni ya wadau.

Maboresho hayo ni pamoja na kuongeza umri wa waombaji mikopo kutoka miaka 33 hadi 35 na pia mwaka huu wameahidi kuwa watapokea maombi kwa wanafunzi waliomaliza kidato cha sita au stashahada ndani ya miaka mitano iliyopita badala ya miaka mitatu ilivyokuwa awali.

Hii ni habari njema kwa wadau wa elimu na wazazi kwamba mwaka wa masomo 2019/2020, Serikali kupitia HESLB imepanga kutoa mikopo na ruzuku ya elimu ya juu yenye thamani ya Sh. bilioni 450 kwa jumla ya wanafunzi 128,285.

Kati ya hao, wanafunzi 45,000 watakuwa wa mwaka wa kwanza. Mwaka huu 2018/2019, unaoelekea mwisho jumla ya Sh. bilinioni 427.5 bilioni zilitolewa kwa jumla ya wanafunzi 123,000.

Hatua hii ilitakuwa na manufaa makubwa kwa jamii yetu kwani kuongezwa kwa idadi ya wanufaika wa mikopo na kiwango cha fedha za mkopo ni wazi kwamba itaongeza idadi ya wasomi nchini.

Pia kulikuwa na malalamiko makubwa kuhusu kukosa mikopo kwa baadhi ya wanafunzi walioonekana kusoma kwenye shule binafsi za gharama, hivyo kuonekana kuwa wazazi au walezi wao wanauwezo wa kuwalipia hata ada ya elimu ya juu nalo limepatiwa ufumbuzi kwa namna yake.

HESLB imewataka wanafunzi waliofadhiliwa na taasisi mbalimbali katika masomo yao ya sekondari au stashahada, kuwa na barua kutoka katika taasisi hizo zinazoonyesha jinsi walivyokuwa wanafadhiliwa kwa kuwa miongoni mwao wapo yatima au waliotoka kwenye familia zenye kipato duni hivyo walinufaika kusoma kwenye shule hizo kwa fadhila.

Jambo hili linatia moyo kwa kuwa miaka kadhaa iliyopita kuna yatima na watoto wa masikini walikwama kuendelea elimu ya juu kutokana na kwamba mashirika au taasisi zilizowafadhili hazikuweka utaratibu wa kugharamia masomo yao zaidi ya yale ya sekondari au mafunzo kwenye vyuo kwa kiwango cha stashahada.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Idara ya Matangazo:** 0745 700710
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

### Kuzembea elimu hii, ina maana kukikumbatia kipindupindu

**WIKI** hii kuna taarifa ya watu kukumbwa na ugonjwa kipindupindu jijini Dar es Salaam. Wameongezeka kutoka 34 mwishoni mwa Mei hadi 55, watatu wameshapoteza maisha.

Ummy Mwalimu, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, alikaririwa akiwataka watu kutotiririsha majitaka mitaani.

Wataalamu wa afya wanasema ni miongoni mwa magonjwa yanayosababishwa na aina ya bakteria aitwaye 'Vibrio cholerae' na anaweka wazi kwamba, ugonjwa ni wa kuambukizwa.

Njia kubwa ya uambukizaji ugonjwa huo, inatajwa na wataalamu ni viini vinavyoenezwa kupitia kwa kinyesi, kutoka kwa wagonjwa wenye kipindupindu kwenda kwa mtu mwingine.

Dalili za ugonjwa huo ni kuharisha sana hadi mwili unashindwa kujihimili, mgonjwa akiwa amedhoofika.

Namna nyingine ya afya, ni mgonjwa anajihsi kuwa na uchovu wa hali ya juu, anashindwa kutulia na ngozi ya nje na ndani zinajikunja, macho yanaingia ndani na anayeumwa anahisi kichefuchefu, kisha baadhi huangukia katika kiharusi.

Kimsingi, namna ya kuepuka kipindupindu ni kunawa mikono kwa sabuni, viganja, upande wa nyuma wa mkono, katikati ya vidole na kucha kwa sekunde baada ya kumaliza haja kubwa na kabla ya kula.

Vilevile, inaelekezwa kabla ya kutayarisha au kula chakula, kusafisha vyombo kama sahani, vikombe na vingine vingi mtu anashauriwa kunawa, kwa sababu ya kuepuka mlipuko wa maradhi.

Haijaishia hapo, jamii inatakiwa kuacha kutiririsha majitaka mitaani, kutumia vyoo safi na kuchemsha maji ya kunywa, lengo ni kuepuka ugonjwa huo.

Cha kushangaza ni kwamba, baadhi ya maeneo jijini Dar es Salaam, imekuwa ni jambo la kawaida watu kutiririsha majitaka mitaani, iwe kipindi cha mvua na hata wa kiangazi.

Elimu nyingine inayotolewa kwa jamii, tabia ya kufunika vyakula ,ili nzi wasiweke bakteria. Hapo tena, inasikitisha baadhi ya watu wasiozingatia na mwisho wa siku inaibuka maradhi ya kipindupindu.

Tufahamu kuwa mtu anapozembea elimu hiyo ni kuendelea kuhatarisha maisha au kuweka maisha rehani. Hivyo, ni muhimu jamii ikabadilika kuzingatia kile ambacho wataalam wa afya wanaelekeza.

Mtindo wa kuvizia mvua na kuelekezea uchafu wa vyooni kwenye mkondo wa maji ya mvua, ni jambo linalowaweka wakazi wa jiji, katika hatari kubwa ya magonjwa ya mlipuko.

Ninajua katika jamii wapo baadhi wasiotaka kunywa maji yaliyochemsha, wakidai hayakati kiu. Niwaambie kuwa, ni mazoea yanayowapoteza. Wanapaswa kuzingatia elimu inayotolewa na wataalam afya.

Kiafya, nikumbushe usafi ni adui mkubwa wa kipindupindu, hivyo jamii ikizingatiwa ni wazi ugonjwa huo utakoma, lakini kuendelea kukumbatia uchafu ni sawa na kuukaribisha.

Kwa sasa ni rasmi kipindupindu kipo jijini Dar es Salaam na tayari serikali imeshatoa onyo inayowataka wakazi wake kuzingatia kanuni za afya, ili kuepuka ugonjwa huo ambao chanzo chake ni uchafu.

Kipindupindu kitatoweka, iwapo kila mmoja atazingatia maelekezo yanayotolewa na wataalamu wa afya. Tatizo kubwa ni jamii kutokuwa makini.

Oktoba mwaka 2017, ulifanyika mkutano wa kumaliza ugonjwa wa kipindupindu ifikapo 2030, uliojumuisha maofisa kutoka nchi mbalimbali duniani na kufanyika nchini Ufaransa.

Shirika la Afya Duniani (WHO), linaeleza matumaini yake ya kupunguza kwa kiasi kikubwa maambukizi ya kipundupindu duniani na kupunguza idadi ya vifo vitokanavyo na ugonjwa huo kwa asilimia 90 ifikapo 2030, kwa vile ni aibu kuwa na ugonjwa katika karne hii.

Wakati juhudi hizo zikifanyika, jamii nayo iwe tayari kumkabili adui maradhi kwa kukubali elimu inayotolewa na wataalam wa afya, vinginevyo adui atakuwa anaondoka na kurudi kama ilivyodumu nchini.

Kuwapo kipindupindu katika karne ya 21, kunaelezwa ni 'aibu kubwa duniani.

## HABARI PICHA

# Swala ya Eid el Fitr katika picha



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akisalimiana na watoto baada ya kushiriki Ibada ya Eid El Fitr kwenye Msikiti wa Anwar, Msasani jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: OWM**



Sehemu ya waumini wa dini ya Kiislamu Mkoa wa Dodoma, wakishiriki swala ya Eid El Fitr, iliyofanyika katika Uwanja wa Jamhuri jijini humo jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Sehemu ya kinamama wakishiriki swala ya Eid El Fitr katika viwanja vya Jamhuri jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Baadhi ya waumini wa dini ya Kiislam wilayani Muheza, Mkoa wa Tanga, wakichagua vazi kanzu baada ya kutoka katika swala ya Eid El Fitr katika Msikiti Mkuu wa Ijumaa, wilayani humo jana. **PICHA: STEVEN WILLIAM**



Mkazi wa Mtaa wa Alhabasi wilayani Muheza mkoani Tanga, maarufu Mama Habiba (kulia), akiandaa mahanjumati katika soko kuu Muheza Juu katika kusherehekea sikukuu ya Eid El Fitr jana. **PICHA: STEVEN WILLIAM**



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, akipokea heshima za Baraza la Eid El Fitr kwa gwaride Maalum la Jeshi la Polisi Kikosi cha FFU, katika viwanja vya Ukumbi wa Sheikh Idrissa Abdulwakil Kikwajuni Zanzibar jana. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Mama Maria Nyerere augua ghafla

**Na Salome Kitomari**

MKE wa Baba wa taifa, Maria Nyerere (88), ameugua ghafla akiwa Uganda kuhudhuria ibada maalum ya kumbukumbu ya mashahidi wa Uganda eneo la Namugongo iliyofanyika Juni 3, mwaka huu.

Mama Maria, alitarajiwa kuwa mgeni rasmi kwenye sherehe hizo, na Rais Museveni alishindwa kuhudhuria kwa kuwa alikwenda kumtembelea hospitalini jijini Kampala.

Aidha, taarifa zinaeleza Rais Museveni alimtuma mwakilishi kwenye tukio la siku ya mashahidi wa Uganda ili kuwaepusha waumini kusubiri kwa muda mrefu.

Kwa mujibu wa BBC Swahili, Mama Nyerere alisindikizwa hadi uwanja wa Ndege wa Entebbe, kupanda ndege ya kurudi nchini kwa ajili ya matibabu zaidi.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa aliondoka uwanjani humo kwa ndege maalum iliyotolewa na Rais Museveni, kuelekea jijini Dar es Salaam kwa matibabu zaidi.

Kwa mujibu wa BBC, Mama Nyerere alipata matatizo ya kiafya usiku kabla ya tukio la kumkumbuka mumewe Hayati Mwalimu Julius Nyerere.

Mwandishi wa BBC nchini humo, alisema hali ya afya ya mjane wa Mwalimu Julius Nyerere, imeendelea kuimarika

Tangu mwaka 2009, waumini wa kanisa Katoliki wamekuwa wakifanya ibada katika hekalu la Namugongo kwa ajili ya kumkumbuka Mwalimu Nyerere.

Mama Maria Nyerere alikuwa Uganda kwa ajili ya ibada maalum ya kukumbuka mchango wa Hayati Mwalimu Nyerere kwa Afrika na Ukristo.

Juni Mosi, rais Museveni na Mama Maria Nyerere walishiriki pamoja ibada hiyo maalumu iliyofanyika katika hekali la mashahidi wa Uganda la Namugongo.

Nyerere alitoa mchango wa zana kuwasaidia Museveni kwa ajili ya kuung'oa madarakani utawala wa Idi Amin.

Kwa mujibu wa BBC, Mama Nyerere amekuwa akisafiri kwenda hadi Namugongo Uganda kwa miaka 13 mfululizo kwa ajili ya sherehe za kuwakumbuka mashahidi wa Uganda.



Dereva wa bajaj akionyesha utii wa sheria za usalama barabarani kwa kusukuma chombo chake, wakati akivuka kwenye alama ya pundamilia katika Barabara ya Morogoro, eneo la Magomeni Kagera, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**.

# Polisi yatoa namba ya dharura

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi nchini limetoa namba ya dharura kwa wananchi ya kupiga wakati wa Sikukuu endapo kutakuwa na viashiria vyovyote vya uvunjifu wa amani ama uhalifu.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi jijini Dar es Salaam, Msemaji wa Jeshi la Polisi SACP David Msime, alitaja namba hizo za bure ambazo wananchi wanaweza kupiga polisi kuwa ni 0787 668 306, 111 au 112.

Misime alisema Jeshi la Polisi limejipanga kuhakikisha Sikukuu ya Eid El Fitr inasherehekewa bila uvunjifu wowote wa amani.

"Tunatoa onyo kwa wale wanaodhani wanaweza kutumia sherehe hizi kufanya uhalifu watambue kuwa watashughulikiwa kwa nguvu zote kwa mujibu wa sheria za nchi," alisema.

Alisema Jeshi la Polisi katika mikoa yote limejipanga kuimarisha ulinzi katika maeneo yote ya ibada na mengine ambayo yatakayokuwa na mikusanyiko.

"Tunaelekeza kila mmoja usalama uanzie kwake na kwa wale wanaomiliki maeneo ya starehe wazingatie maelekezo ya kiusalama waliopewa na Makamanda wa Polisi wa Mikoa na vikosi na watakayoendelea kuwapa," alisema.

Kuhusu uhalifu alisema bado yapo matukio mchache ambayo Jeshi la Polisi linaomba ushirikiano zaidi kutoka kwa wananchi katika kupeana elimu ya kuyaepuka kuyatenda.

Matukio kama vile mauaji yanayotokana na vitendo vya wananchi kujikulia sheria mikononi, wivu wa mapenzi na ulevi, matukio ya ubakaji na ajali zinazosababishwa na uzembe wa madereva," aliyataja.

Alisema wanaamini kama kila mtu kwa nafasi yake akishiriki katika kutoa elimu kuonya na kuwafichua wanaotenda uhalifu huo, kuanzia ngazi ya familia matukio ya aina hiyo yatapungua kwa kiasi kikubwa.

Akizungumzia mifuko ya plastiki ambayo mwisho wake ni mwanzoni mwa mwezi huu, Misime alisema agizo hilo liendelee kuzingatiwa na wenye mifuko ya aina hiyo waisalimishe kama ilivyoelekezwa.

"Kama kuna mwenye taarifa za mtu mwenye kumiliki mifuko hiyo atoe taarifa polisi au mamlaka zingine ili hatua stahiki kwa mujibu wa sheria na kanuni ziweze kuchukuliwa," alisema.

# Gati sasa kuokoa wasafiri

**Na Mary Geofrey,** MUSOMA

WANANCHI wa mikoa ya Mara, Mwanza, Kagera na nchi za jirani ikiwamo Uganda, wanatarajia kuondokana na adha ya usafiri katika Bandari Mwigobelo, mkoani Mara, baada ya Mamlaka ya Bandari (TPA), kukamilisha ujenzi wa gati la kisasa katika Bandari ya Mwigobelo, lililogharimu Sh. milioni 605.

Wananchi wa mikoa hiyo, walikuwa wakipoteza maisha kwenye Ziwa Victoria, kukanyaga maji, wanawake walilazimika kuvua nguo, kupoteza vitu vya thamani kama simu, kabla ya kupanda au kushuka kwenye meli.

Mhandisi wa Bandari ya Ziwa Victoria, Abraham Msina, akizungumza na waandishi wa habari jana katika bandari za Musoma na Mwigobelo, mkoani Mara, alisema kuwa mradi uliojengwa kwa miezi sita kwa lengo la kuwapunguzia adha watumiaji ambao walilazimika kupanda na kushukia ndani ya maji.

Alisema mradi huo umeshakamilika, wanasubiri ukarabati wa mwisho wa mambo machache na kukamilika kwa taratibu za TPA kabla ya kuanza kutumika rasmi.

"Mradi huu wa ujenzi wa gati ya kushukia abiria na mizigo ya wavuvi, ulianza Novemba mwaka jana na umekamilika Mei mwaka huu na umegharimu Sh. milioni 605," alisema Msina.

Aidha, alisema mwaka ujao wa fedha wa 2019/20 wanatarajia kujenga gati lingine lenye urefu wa mita 200, jengo la abiria, ukuta, soko la samaki na ofisi.

Naye Anna Joseph, mkazi wa Musoma, alisema awali kabla ya ujenzi wa gati hiyo, walikuwa wakilazimika kupandisha nguo wanapokanyaga maji wakati wa kupanda au kushuka kwenye meli hali ambayo ilikuwa ikiwadhalilisha na wakati mwingine kupoteza mali zao kama simu.

## 57 washindwa kurejesha fomu udiwani

INATOKA UK.3

orodha ya wagombea udiwani," alisema.

Alisema katika kikao kilichofanyika juzi kimetoa maamuzi kuwa Tume imekubali rufaa moja ya mgombea Udiwani wa CUF katika kata ya Ipole hivyo kumrejesha kuendelea kuwa kugombea nafasi hiyo.

"Nec imekubaliana na maamuzi ya Msimamizi wa Uchaguzi katika kata ya Murangi ya kuwaondoa wagombea wa CUF na Chadema katika orodha ya wagombea na hivyo wagombea kuendelea kuenguliwa kugombea udiwani," alisema.

Pia alisema katika uteuzi huo wa udiwani kata 32, jumla ya wagombea katika kata 29 wamepita bila kupingwa na mgombea wa CUF kutoka kata ya Kyaitoke Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba na mgombea wa ACT -Wazalendo kutoka kata ya Boma iliyopo katika Halmashauri ya Mji Mafinga wamejitoa kwenye kinyang'anyiro hicho, hivyo kata ya Ipole Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge ndiyo itakayofanya uchaguzi Juni 17.

Dk. Kihamia alisema kampeni za uchaguzi zimeshaanza kwa mujibu wa ratiba ya uchaguzi na zitaendelea hadi Juni 16, ikiwa ni siku moja kabla ya siku ya uchaguzi. kisi ya bajeti inafikia asilimia 3.2.

## Waislamu wapewa somo kudumisha amani, upendo

INATOKA UK.3

matumizi ya mifuko ya plastiki.

Kwa upande wake, Mufti wa Tanzania, Sheikh Abubakar Zubeir, aliwataka Waislamu nchini kuendeleza umoja na mshikamano.

Aliwataka Waislamu nchini kujilekea njia za kiuchumi kwa kujishughulisha ili waweze kujiletea maendeleo.

Pia, aliwataka Waislamu nchini kutii mamlaka zote za kidini na kiutawala, pamoja na kuwatii viongozi waliopo madarakani. **Imeandikwa na Gwamaka Alipipi (Dar) na Dege Masoli (Tanga).**

HABARI MIKOANI

# Waziri Biteko, wawekezaji wajadili sheria ya madini

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Madini, Doto Biteko, amekutana na wawekezaji wa Kampuni ya Ngwena Tanzania Ltd "Ngwena" na kufanya nao mazungumzo kuhusu masuala mbalimbali.

Jambo kubwa lilikuwa ni kutoa ufafanuzi kuhusu marekebisho ya sheria ya madini inavyotoa fursa na mazingira mazuri ya uwekezaji katika sekta ya madini nchini.

Hatua hiyo inafuatia ombi la kampuni hiyo kuomba kukutana na waziri Biteko ili kupata ufafanuzi wa moja kwa moja kutoka kwake kuhusu mabadiliko hayo ya sheria.

Ombi la kutaka kuonana na waziri ni kutokana na kampuni ya Ngwena kupata taarifa za upotoshaji na zisizo sahihi kuhusu mabadiliko ya sheria ya madini yaliyofanywa na Bunge kuhusu taratibu mbalimbali za uwekezaji na shuguli nyingine zinazohusu sekta ya madini.

Upotoshaji unaofanywa kwa makusudi na baadhi ya watu ndani na nje ya nchi kwa lengo la kutaka kuifanya Tanzania kama sio mahali sahihi pa kuwekeza.

Biteko aliuambia ujumbe wa kampuni ya Ngwena kuwa mabadiliko ya sheria yamefanyika kwa kuzingatia maslahi ya pande zote mbili mwekezaji na taifa kwa upande mwingine.

Alifafanua kuwa, tangu mabadiliko hayo yapitishwe, hakuna malalamiko ya kupingwa kwa marekebisho hayo kwa kuwa yalizingatia maslahi mapana ya kila upande na kuhakikisha mazingira ya uwekezaji yanakuwa rafiki na ndio sababu mpaka sasa tangu marekebisho hayo yafanyike, hakuna kampuni au mwekezaji alieacha wala kuonyesha nia ya kufunga shughuli zake kwa sababu ya marekebisho ya sheria.

Aliongeza kuwa, Tanzania inawahitaji sana wawekezaji na mara zote kila panapokuwa na jambo haliendi sawa mara moja hukaa na kujadili na mwekezaji na kutatua changamoto.

Aliitaka kampuni ya Ngwena kwenda kuwa mabalozi ili kuwaeleza wengine kuhusu ukweli ulivyo kuhusu marekebisho ya sheria yaliyofanywa na kuachana na upotoshwaji unaofanywa na baadhi ya watu ambao hawana dhamana ya kuyazungumzia masuala hayo.

Aliwakaribisha watu na wawekezaji wanaotaka kupata ufafanuzi wa jambo lolote kutembelea ofisini kwake jijini Dodoma.

Kwa upande wa kampuni ya Ngwena ukiongozwa na Meneja Mkuu H.E Kavishe, alimshukuru Waziri kwa ufafanuzi mzuri alioutoa na kwamba walichokuwa wanakisikia na alichokisema waziri ni vitu tofauti, na kuongeza kuwa kuonana kwao kumewafungua masikio na kupata ukweli kutoka kwa mtu sahihi na mwenye dhamana ya sekta ya madini.

Aliongeza kuwa ni kweli upotoshaji waliokuwa wanaupata ungeweza hata kuwarudisha nyuma, hivyo watakwenda kufikisha ujumbe kwa wenzao.



Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamisi Kigwangalla, akizungumza wakati akizindua rasmi Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), jijini Dodoma juzi. Bodi hiyo iliongezewa muda wa miaka 3 na Rais, Dk. John Pombe Magufuli Aprili 23 mwaka huu. **PICHA: WMU.**

# Wanaojifungulia majumbani kutozwa faini

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

SERIKALI mkoani Shinyanga inatarajia kutunga sheria ndogo ambazo zitawabana wajawazito kwenda kujifungulia kwenye huduma za kiafya, ikiwamo kuwatoza faini Sh. 20,000 kwa wale ambao watabainika kuzalia watoto majumbani.

Lengo ni kupunguza tatizo la vifo vya mama na mtoto vitokanavyo na uzazi mkoani humo.

Sheria hiyo inatarajiwa kutungwa na kutumika kuanzia ngazi ya kijiji ambapo kutakuwa na daftari la kuorodhesha wajawazito wote kwenye kijiji husika, kisha kufuatiliwa kama wana hudhuria kliniki na kujifungulia kwenye huduma za kiafya, na kuwachukulia hatua ambao watajifungulia majumbani.

Hayo yalibainishwa juzi na Mganga Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Rashidi Mfaume, kwenye kikao cha wadau wa afya, wakati akisoma mapendekezo ya sheria ndogo ambazo zitawabana wajawazito kwenda kujifungulia kwenye huduma za kiafya na kupunguza tatizo la vifo vya uzazi.

Alisema mkoa kwa kushirikiana na wanasheria wametoa mapendekezo ya sheria hizo ndogo zitakavyotumika, kwa kuorodheshwa wajawazito wote kuanzia ngazi ya kijiji na kufuatiliwa mahudhurio yao ya kliniki, pamoja na kuwatoza faini ya Sh. 20,000 ambao watabainika kujifungulia majumbani.

"Lengo la utungwaji wa sheria hizi ndogo ni kupunguza tatizo la vifo vya mama na mtoto vitokanavyo na uzazi, ambavyo idadi kubwa husababishwa na wajawazito kutohudhuria kliniki na kupenda kujifungulia majumbani, pale wanapozidiwa ndipo hukimbilia hospitali na kusababisha ongezeko la vifo vya uzazi," alisema Mfaume.

Mratibu wa huduma ya uzazi na mtoto mkoani Shinyanga Joyce Kandolo, alitaja takwimu za vifo vya mama na mtoto vitokanavyo na uzazi mkoani humo, ambapo mwaka 2017 walifariki wajawazito 73, mwaka 2018 (56) na mwaka huu kuanzia Januari hadi Aprili wameshafariki 18.

Vifo vya watoto wachanga mwaka 2017 walifariki 913, mwaka jana walikuwa 815, na mwaka huu Januari hadi Aprili ni 218.

Mkuu wa mkoa wa Shinyanga, Zainabu Telack, aliagiza sheria ndogo zijadiliwe haraka na kupelekwa kwake ili apate kuzibariki na zianze kutumika.

# Katazo watoto kwenye starehe

**Na Dege Masoli,** MKINGA

DAWATI la Jinsia na Watoto Wilaya ya Mkinga mkoani Tanga, limepiga marufuku watoto kushiriki katika kumbi za starehe zinazofanyika vyakati za usiku kwenye maeneo mbalimbali.

Hayo yalielezwa na mwakilishi wa dawati hilo wilayani hapa, Justina Reuben, kwenye kikao cha wadau wa mapambano dhidi ya ndoa za utotoni kilichoandaliwa na Shirika la World Vision .

Reuben alisema Dawati hilo lililopo chini ya Jeshi la Polisi limeandaa tangazo la katazo la watoto kutokuzurura nyakati za usiku kushiriki katika sherehe kwenye kumbi za starehe zinazofanyika nyakati hizo.

"Lengo ni kuhakikisha watoto wanakuwa salama na kuwaepusha na mambo wanayoweza kufanyiwa na watu ambao si wastaarabu, na agilo hilo na kila mzazi ama mlezi anatakiwa kulizingatia kwa kutomruhusu mtoto wake," alisema Reuben.

Akizungumza katika kikao hicho, mratibu wa World Vision Wilaya ya Mkinga, Evodia Chija, aliitaka jamii kutoendeleza ndoa za utoto na kwamba litahakikisha elimu ya athari za matendo hayo inamfikia kila mwananchi ili kukomesha tamaduni na tabia hiyo.

Chija alisema ili kudhibiti tatizo hilo ni wajibu wa kila mmoja kwa nafasi yake kupaza sauti kwa lengo la kukemea mimba na ndoa za utotoni na kwamba jukumu la msingi ni wazazi na walezi kutekeleza wajibu wao ili kuwanusuru watoto wa kike na hatimaye kuwaepushakuingia kwenye vishawishi.

Meneja wa shirika hilo Kanda ya Mashariki, Pudensiana Rwezaula, alisema mwaka 2018 walizindua kampeni ya mapambano dhidi ya ndoa za utotoni, hivyo ni jukumu la kila mmoja kushirikiana nao ili kuona namna gani ya kupambana na changamoto hiyo ikiwa ni pamoja na kuwekeana mipango kazi ya kutokomeza jambo hilo.

Rwezaula alisema wazazi wanapaswa kuwaelewesha mabinti zao juu ya madhara ya kujiingiza katika mahusiano wakiwa na umri mdogo ikiwamo kutoa elimu kwa watoto wao kuhusu masuala ya ukuaji. Akifungua kikao hicho kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya hiyo, Erick Farahani, aliishukuru World vision kwa shughuli mbalimbali za kimaendeleo ambazo wamekuwa wakizifanya mkoani Tanga kama sehemu ya kuunga mkono jitihada za serikali.

Afisa Ustawi wa Jamii, Sosten Mtena, pamoja na Afisa Afya wilayani Mkinga, Daniel Kijazi, walisema mtoto anapopata mimba wakati wa utotoni huathirika kisaikolojia kutokana na kumwaga damu nyingi wakati wa kujifungua.

# RC aagiza familia iliyoondolewa kwenye nyumba kurejeshwa

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

MKUU wa mkoa wa Ruvuma, Christina Mndeme, amemwagiza Mkuu wa Wilaya ya Mbinga, kuchukua hatua za haraka kuirejesha familia ya Boko Omari Mbwana inayolala nje kwa zaidi ya siku tisa baada ya kuondolewa kinguvu na mfanyabiashara wa mjini Mbinga.

Mndeme alifikia uamuzi huo baada ya familia hiyo kwenda ofisini kwake kuomba msaada ili isaidiwe kuondokana na adha hiyo kutokana na kushindwa kupata msaada kutoka kwa Mkuu wa Wilaya ya Mbinga, Cosmas Nsenye.

Alisema kuwa familia hiyo ambayo imeleta malalamiko ofisini kwake kuwa tangu Mei 23, mwaka huu wamekuwa wakilala nje ya nyumba yao baada ya kufukuzwa na mfanyabiashara, Godfrey Malila.

Alisema kutokana na familia hiyo kukosa ushirikiano kutoka kwa viongozi wa serikali ya wilaya, warejeshwe kwenye nyumba hiyo hadi kesi ya msingi itakapomalizika mahakamani.

Mapema familia hiyo ambayo iliongozwa na Domitila Ndunguru ilifika kwenye ofisi za Chama cha Waandishi wa Habari Mkoa wa Ruvuma na kukutana na waandishi na kulalamika kuwa Mei 23, mwaka huu majira ya subuhi lilifika kundi la watu ambao walidai kuwa walifika kuihamishia nje familia pamoja na mizigo yao.

Alifafanua zaidi kuwa walianza kubeba vyombo na kuvitoa nje kwa kuviweka kwenye upenu wa nyumba ya jirani kisha waliwaondoa kwa nguvu na baadaye walifunga milango kwa makufuli na kuzungushia kamba kuonyesha marufuku mtu kuingia ndani.

"Kinachonishangaza sisi tumefungua kesi ya kupinga kuuzwa kwa nyumba hiyo kwa kuwa hati inayodaiwa kwamba familia ilikaa na kumteua msimamizi wa mirathi wakati baba yetu mzazi yupo hai na alimwachia documents (nyaraka) za nyumba na mimi nikiwa na miaka mitano mdogo wake Boko Omari Mbwana taarifa hiyo inatoka wapi?" alihoji Domitila Ndunguru, mtoto wa mwenye nyumba.

Kaimu Katibu Tawala wa Wilaya ya Mbinga, Enhard Ndunguru, alisema ofisi yake imepokea simu ya maagizo kutoka kwa mkuu wa mkoa wa Ruvuma kuwa jitihada zifanyike kuirudisha familia kwenye nyumba yao hadi kesi ya msingi itakapomalizika mahakamani.

Alifafanua kuwa mkuu wa wilaya ya Mbinga alikuwa safarini nje ya mkoa kwa shughuli za kikazi, lakini naye ametoa maagizo kuwa hilo tatizo lishughulikiwe haraka iwezekanavyo kupitia kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya.

Kwa upande wake mfanyabiashara Malila, alisema nyumba hiyo aliinunua kisheria na ndiyo maana alichukuwa uamuzi wa kuwaondoa.

Alipoulizwa kuhusu agizo la mkuu wa mkoa kuirejesha familia kwenye nyumba hadi kesi ya msingi itakapomalizika, alijibu kuwa mkuu wa mkoa hana mamlaka na siyo mahakama, hivyo maamuzi aliyoyachukuwa kuiondoa familia hiyo ibaki kama ilivyo kwa kuwa hakuna mtu wa kubatilisha amri ya mahakama.

Mkuu wa wilaya ya Mbinga alipoulizwa na Nipashe kwa njia ya simu kuhusiana na kushindwa kulipatia ufumbuzi kwa muda mrefu, alisema ameshaanza kuchua hatua ya kuona umuhimu wa kuirejesha familia hiyo kwenye nyumba yao kama alivyoagiza mkuu wa mkoa.



Wafanyausafi wakiwa wamepumzika baada ya kazi ngumu ya kufagia barabara katika eneo la Jangwani, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Kasi ya kutisha mimba utotoni

**Na Lilian Lugakingira,** MISSENYI

TATIZO la watoto kupewa ujauzito wilayani Missenyi mkoani Kagera linaendelea kuwa kubwa, baada ya wajawazito 366 kubainika kuwa na umri wa chini ya miaka 18, kati ya wajawazito 2,221 waliojitokeza kwenda kliniki hudhurio la kwanza katika kipindi cha Januari hadi Machi mwaka huu.

Akizungumza wakati wa kikao cha tathmini ya kampeni ya kupinga mimba za utotoni inayoendeshwa na shirika la World Vision Tanzania Kanda ya Kagera, Afisa Ustawi wa Jamii wa Wilaya hiyo, Anold Nkongoki, alisema kati ya watoto hao 366, watoto 21 hawakuwa na waume.

"Tafsiri yake ni kwamba hawa ni watoto ambao wamepewa mimba na watu wasiojulikana," alisema.

Nkongoki alisema kwa upande wa ukimwi vijana 1,053 wanaishi na virusi vya Ukimwi, na kati ya hao vijana 556 ambao ni sawa na asilimia 52 ni wasichana.

"Hawa walipata maambukizi kwa njia nyingi zikiwamo ngono zembe kutokana na baadhi ya watu katika jamii kuwa na dhana potofu kuwa wanafunzi hawana Ukimwi wanawakimbilia na matokeo yake wanawaambukiza Ukimwi, lakini wengine wanapata maambukizi ya kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto," alisema.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Missenyi, Denis Mwila, akifungua kikao hicho alisema tatizo la mimba za utotoni linachangia ongezeko la watoto wa mitaani.

"Mimba za utotoni sio jukumu la serikali pekee, ni jambo mtambuka kuanzia ndani mzazi mwenyewe kumfundisha mtoto maadili mema ya Kitanzania, tunapaswa kushirikiana kwa pamoja kukabiliana na tatizo hili," alisema.

Felister Enock, mwanafunzi wa darasa la saba katika Shule ya Msingi Kasambya, alisema umaskini ni moja ya visababishi vya mimba za utotoni na kuwataka wazazi kutokwepa majukumu yao ya kuwahudumia watoto wao.

"Kuna baadhi ya watoto wakiona hawapewi matunzo na wazazi wao wanaamua kwenda kutafuta fedha na huko ndiko anapata mimba, lakini wazazi wengine wanaweza kuwaambia watoto wao kwamba waende kutafuta fedha wakati wanaona kwamba ni watoto," alisema.

Naye Rashid Ramadhan, kutoka Dawati la jinsia Jeshi la Polisi Kyaka, alisema hadi Juni 2018 kesi zilizoripotiwa Kituo cha Polisi Kyaka ni 30.

Akizungumzia kazi zilizotekelezwa na World Vision mradi wa Missenyi, mratibu wa shirika hilo wilayani Missenyi, Renatus Rugakingira, alisema kutokana na kampeni wanayoifanya uelewa umeongezeka, na mimba ambazo zilikuwa haziripotiwi polisi sasa zinaripotiwa.

# Washirikiana na serikali kujenga madarasa

**Na Elisante John,** SINGIDA

WANANCHI wa Ilongero Halmashauri ya Wilaya ya Singida, wameshirikiana na serikali kujenga vyumba viwili vya madarasa, ili kumaliza adha kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu kusoma kwenye vyumba chakavu vilivyojengwa kabla ya uhuru.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Ilongero, Edward Ikhonde, alisema hayo mbele ya Mbunge wa Singida Kaskazini, Justine Monko, aliyekwenda kukagua ujenzi wa vyumba hivyo, vilivyogharimu zaidi ya Sh. milioni 46, yakiwamo matundu sita ya vyoo.

Ikhonde alisema serikali ilitoa fedha hizo kwa ajili ya ujenzi wa chumba kimoja na ofisi, lakini jamii ikaunga mkono kwa kusomba mawe, mchanga na nguvukazi, hali iliyochangia chumba kimoja zaidi kuongezeka, na hivyo kukidhi mahitaji ya wanafunzi wa kada hiyo.

Kutokana na hali hiyo, mbunge Monko aliwashukuru wananchi wa kata, tarafa na jimbo zima la Singida kaskazini kwa juhudi kubwa walizoonyesha katika kushirikiana na serikali yao, ili kutatua matatizo mbalimbali ya kijamii.

Alisema kuwa, hali hiyo itachochea maendeleo na hivyo kufikia lengo la serikali ya awamu ya tano katika kuwaletea watu wake maendeleo, kutokana na mageuzi ya kiuchumi yanayochochewa na ujenzi wa miundombinu mbalimbali, vikiwamo viwanda.

Monko aliwataka wananchi hao kuendeleza ushirikiano zaidi ili kumaliza kabisa kero ya uhaba wa vyumba vya madarasa, madawati, matundu ya vyoo, zahanati na masuala mengineyo ya kijamii, katika jimbo hilo.

Diwani wa Kata ya Ilongero, Issah Mwiru, alisema mwamko mkubwa wa jamii juu ya masuala ya maendeleo, unachochewa na uwapo wa uwazi na ukweli kwenye taarifa, hali inayorahisisha jitihada kwa miradi mingi ya kijamii kutekelezwa kwa wakati.

# Watakiwa kuwaasili watoto yatima

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

WATANZANIA wametakiwa kuwa na tabia ya kuwaasili watoto wanaoishi katika vituo ili kuwasaidia kutokukaa vituoni kwa muda mrefu.

Mkurugenzi wa Kituo cha Kulelea Watoto Yatima na wale waliotelekezwa na wazazi wao cha Samaritan Father, Josephat Mmanyi, alisema hayo juzi alipozungumza na waandishi wa habari baada ya kupokea zawadi za sikukuu ya Iddi.

Alisema ni vyema Watanzania wakajenga tabia ya kusaidia kwa kuwaasili watoto wanaoishi vituoni ili nao wajisikie vyema na wajione wana ndugu na wazazi kama walivyo wengine.

"Unajua watoto hawa ni binadamu na wao wanahitaji malezi ya wazazi kama vile wengine wanavyoitaji, hivyo tunawaomba Watanzania kwa ujumla wajitokeze kuja kuwaasili watoto hawa ili nao wasikae vituoni muda mrefu. Wanavyokaa muda mrefu wanazidi kuwa wapweke zaidi," alisema Mmanyi.

Aidha, alisema hadi sasa watoto watano wameshaasiliwa, watatu kati yao nje ya nchi, huku wawili wakiwa wameasiliwa nchini. Watu wote walioasili watoto hao wamefuata sheria zote za kiserikali.

Akizungumza wakati wa kukabidhi zawadi hizo, Meneja Masoko wa Kampuni ya Promasidor inayozalisha maziwa ya Cowbell, Vitus Mpanda, alisema hiyo si mara ya kwanza kwa kampuni yao kutoa msaada wa aina hiyo kwa kuwa wamekuwa wakitoa na kufanya shughuli za kijamii katika mikoa tofauti.

Mpanda alisema nia ya kutoa vitu hivyo ni kurudisha fadhila kwa wananchi na jamii, kwa kuwa wananchi wamekuwa wakinunua maziwa yao na bidhaa zao, hivyo wameona warudishe fadhila kwa kuwapatia msaada huo.

"Tunataka watoto hawa washerehekee Iddi vizuri kama watoto wengine. Pia tunaamini kuwa kwenye kutoa ndipo Mungu anatubariki vyema" alisema Mpanda.

Alitoa wito kwa wananchi kuendelea kujitokeza kutoa misaada kwa watoto yatima, pamoja na watu wasiojiweza ili Mungu awabariki.

Alitoa wito kwa wazazi hususan wanawake kuacha kuzaa bila mpangilio kwa kuwa kwa kufanya hivyo kunasababisha kutupa watoto au kuwatelekeza, hivyo ni vema kuepuka dhambi hiyo kwa kutumia kinga.

Baadhi ya vitu vilivyotolewa na kampuni hiyo ni mchele, sukari, unga na mafuta.




Mkuu wa Wilaya ya Karatu, Theresia Mahongo, akipongeza Shirika lisilo la kiserikali la World Vision kwa kujenga choo cha kisasa katika shule ya msingi na sekondari Endabash kwa ajili ya kusaidia watoto wa kike wawe na mazingira salama wanapokuwa katika hedhi. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**.

## Apigia debe teknolojia ya uhamilishaji mifugo

**Na Cynthia Mwilolezi**, ARUSHA

WAFUGAJI nchini wamehamasishwa kubadili mtazamo katika kufuga kisasa kwa kutumia teknolojia ya kupandisha kwa njia ya chupa badala ya kutumia madume ambayo yanawezesha kuzalisha kwa wingi zaidi na kwa wakati.

Mratibu Mkuu wa mradi upande wa Tanzania ambaye pia ni Kaimu Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania Kituo cha Tanga, Dk. Zabron Nziku, alisema hayo jana wakati akizungumza kwenye mkutano uliowashirikisha wafugaji wa Wilaya ya Longido.

Mkutano huo pia ulishirikisha wadau mbalimbali kujadili namna ya kuboresha, kuendeleza na kuhifadhi ng'ombe aina ya Sahiwal, ili wafugaji wafuge kisasa na kuongeza tija.

Alisema Tanzania na Kenya kwa pamoja zinatekeleza mradi huo kwa kuboresha ng'ombe wa asili kwa kutumia madume ya ng'ombe bora aina ya Sahiwal, unaofadhiliwa na Umoja wa Afrika (AU). Kupitia mradi huo, wafugaji wameanza kunufaika na ufugaji bora na wa kisasa.

Dk. Nziku alisema kupitia mradi huo, madume matatu bora ya mbegu aina ya Sahiwal yamenunuliwa na kupelekwa kwenye Kituo cha Uhamilishaji (NAIC) kilichoko Usa River, Arumeru mkoani Arusha, kwa lengo la kuvunwa mbegu ili kusambazwa kwa wafugaji kutoka Longido na maeneo mengine nchini.

Alisema mradi huo umelenga kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili wafugaji ikiwamo kuhamasisha matumizi ya kutumia teknolojia ya uhamilishaji, ambayo wengi wao wameona manufaa makubwa.

Kwa mujibu wa Dk. Nziku, mradi huo wa mwaka mmoja unatekelezwa wilayani Longido, katika Kata mbili za Mundarara na Engarenaibor na unalenga kuwafikia zaidi ya wafugaji 1000 kwa kipindi cha mwaka mmoja.

"Kwa hiyo nawaomba wafugaji mtumie Kituo cha Taifa cha Uhamilishaji (NAIC) ili kupata mbegu bora za uhamilishaji na namna bora ya kuboresha ufugaji wao," alisema.

# Wazazi wahimizwa chanjo kwa watoto

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

WAZAZI na walezi katika Halmashauri ya Mji wa Babati mkoani Manyara, wametakiwa kuwa makini na kuhakikisha watoto wao wanapata chanjo zinazotolewa ili kuwakinga na magonjwa na vifo visivyo vya lazima.

Ushauri huo ulitolewa jana mjini hapa na Mratibu wa Chanjo wa Mji ambaye pia ni Ofisa Afya, Grace Ngoo, alipokuwa akizungumza na Nipashe juu ya chanjo zinazohusu watoto kuanzia miaka sifuri hadi mitano.

Alisema tangu mtoto anapozaliwa, siku hiyo anatakiwa kuanza kupata chanjo ya BCG mpaka kipindi cha siku 14.

Ngoo alisema kwa wale wanaokwepa chanjo hiyo wanawaandalia hatari ya kupata ugonjwa wa kifua kikuu na akichanjwa anatakiwa apate kovu ndani ya miezi mitatu, asipopata inabidi arudiwe maana asipopata wataalamu watabaki na mashaka.

"Mtoto ambaye hajachanjwa ni hatari na kinga yake iko chini ila akichanjwa inamwepusha na vifo, hivyo wazazi au walezi wasipuuze chanjo yoyote," alisema na kufafanua kuwa lengo la kitaifa ni kutoa chanjo zote kwa asilimia 90 lakini kwa wilaya ni asilimia 95 japo Babati mjini imekwenda juu zaidi.

Alitaja chanjo zingine ni polio ambayo mtoto hawezi kupata wakati mwingine wowote isipokuwa baada ya kuzaliwa ambayo ni chanjo ya kumweka salama zaidi mtoto.

"Chanjo hii inagawanyika mara tatu ikiwa ni By polio 1, By polio2 na By polio3, hivyo mtoto anapata dozi nne za polio "alisema na kuongeza kuwa polio zingine anapata mtoto anapotimiza wiki sita.

Alizitaja faida za chanjo hizo kuwa ni kumkinga mtoto dhidi ya ugonjwa wa kupooza na inamhakikishia kinga ya mwili na anakuwa si hatari kwa wengine.

Ngoo alizitaja chanjo zingine muhimu kuwa ni IPV ambayo ni kwa ajili ya kutokomeza ugonjwa wa polio nchini. Mgonjwa wa mwisho wa polio alipatikana mwaka 1996.

Dalili za ugonjwa polio anasema ni ghafla mtoto anashindwa kushika kitu mfano mikono au miguu inalegea, kushindwa kutembea na wengine wanatikisika hata vichwa.

Takwimu zilizotolewa na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, bungeni wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka 2017/18 za Januari hadi Desemba, mwaka huo, kipindi hicho zinaonyesha kuwa asilimia 101.2 ya watoto waliolengwa nchini walipatiwa chanjo zote muhimu ili kuwakinga na magonjwa.





# Mbunge ahoji ujenzi barabara ya lami

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

MBUNGE wa Moshi Vijijini (Chadema), Anthony Komu, ameitaka serikali mkoani Kilimanjaro kutoa ufafanuzi wa lini ahadi ya Rais Dk. John Magufuli ya mwaka 2015 ya kuijenga barabara ya Getifonga/Mabogini/Kahe/Chekereni kwa kiwango cha lami, itaanza kutekelezwa rasmi.

Katika ukurasa wake kwenye moja ya mitandao ya kijamii, Komu ameuliza ahadi hiyo itaanza kutekelezwa lini ili kuwapa wananchi wa Moshi Vijijini ahueni katika sekta ya usafirishaji.

Wakati Komu akitaka kutekelezwa kwa ahadi hiyo, siku chache zilizopita Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Moshi lilielezwa na Mhandisi anayesimamia Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (Tarura), Loisheyi Mollel kuwa tayari ahadi hiyo imetengewa kiasi cha Sh. bilioni 22.

Kwa mujibu wa ofisi hiyo ya Tarura, sehemu ya utekelezwaji wa ahadi ya Rais Magufuli, itaanza kuonekana katika bajeti mpya ya mwaka wa fedha unaoanza Julai Mosi, mwaka huu.

Alisema kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Tarura itatumia zaidi ya Sh. bilioni 1.1 katika ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilomita 674.52 ikiwamo ahadi ya Rais Dk. John Magufuli ya ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilomita 20.

Mollel alieleza kuhusu utekelezaji wa mpango huo, baada ya taarifa ya utekelezaji wa robo tatu ya mwaka inayoanzia Januari 2019 hadi Machi kusomwa katika kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi.

Kabla ya kutolewa taarifa hiyo inayoleta faraja zaidi kwa wananchi wa maeneo hayo, Diwani wa Kata ya Mabogini, Emmanuel Mnzava, ilieleza kuwa katika sekta ya ujenzi ndani ya kata yake, ahadi ya Rais (Magufuli) ya kuijenga barabara hiyo bado haijatekelezwa.

Katika taarifa yake, Mnzava alitoa wito kwa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, zaidi akiiomba ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji na Tarura kusaidia kufuatilia ahadi hiyo.

Kata hiyo ya Mabogini ina jumla ya vijiji vinane, vitongoji 45 na ina kaya 8,360 zenye jumla ya wakazi 28,992.

# Mwecau yaingiza wilaya 5 ufundishaji shuleni

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

TUME ya Kikristo ya Huduma za Jamii ya Chuo Kikuu cha Kikatoliki Mwenge (Mwecau), imeziingiza wilaya tano za mikoa ya Kanda ya Kaskazini katika mpango maalum wa uhuishaji wa mbinu shirikishi za ufundishaji shuleni.

Mratibu wa mpango huo kutoka tume hiyo, David Marandu, alisema wilaya zilizochaguliwa kuingia katika mpango huo ni Siha, Mwanga, Meru, Karatu na Monduli.

"Ni kweli kwamba zoezi hilo linahusisha wilaya hizo na hii imetokana na mjongeo chanya wa ufaulu katika mitihani ya kitaifa kwa miaka ya hivi karibuni.

"Mpango huu ni endelevu na tunakusudia kuwafikia wadau wote wa elimu kuanzia ngazi ya wilaya, kata na ngazi ya shule hasa wadau wakubwa wakiwa ni walimu."

Aidha, Marandu ameeleza kuwa wanakusudia katika mikoa ya Kanda ya Kaskazini kuziingiza halmashauri zote katika mpango wa mbinu shirikishi za ufundishaji shuleni.

Kwa mujibu wa Marandu, mpango wa mafunzo ya mbinu shirikishi kwa mikoa ya Kanda ya Kaskazini, unaendelea kutekelezwa kwa mwaka wa nne sasa.

Katika Mkoa wa Kilimanjaro, wilaya pekee iliyoanza kunufaika na mpango huo ni Siha ambayo tayari walimu 60 wa shule za sekondari za wilaya hiyo wameshanolewa ili waweze kutumika kama injini ya kubadili taswira ya ufaulu katika mitihani ya kitaifa.

Katika kuhakikisha kiwango cha elimu kinapanda, serikali na wadau wa elimu wamekuwa wakiendesha mafunzo mbalimbali ili kuondoa tatizo linalosababisha kiwango cha elimu kushuka.

Zaidi Marandu alieleza: "Nia yetu ni kuwawezesha walimu kuwa na uwezo mkubwa wa ufundishaji ili kuongeza uelewa kwa wanafunzi, dhana ni kwamba bila kuwanoa walimu katika baadhi ya masomo yanayoonekana kutofanywa vyema na wanafunzi inaweza kuwa ngumu kufikia malengo yanayotarajiwa."



Mkurugenzi wa Jiji la Mwanza, Kiomoni Kibamba, akipokea vifaa vya kufanyia usafi kutoka kwa Meneja wa tawi la Akiba Commercial Bank, Harriet Bujiku, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani. Makabdhiano hayo yalifanyika Soko Kuu jijini Mwanza, kushoto ni Mwenyekiti wa soko hilo Hamad Nchola (mwenye kanzu). **PICHA : ELIZABETH FAUSTINE**.

# Bil. 2/- kukarabati dampo la Moshi

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

HALMASHAURI ya Manispaa ya Moshi, imesaini mkataba maalum na Kampuni ya Ukandarasi ya Rocktrotinic Ltd ambayo imepewa zabuni ya ukarabati na uboreshaji wa dampo la kutupia taka ngumu ambalo litagharimu kiasi Sh. billioni mbili.

Mkataba huo umesainiwa kati ya Meya wa Manispaa hiyo, Raymond Mboya na kampuni hiyo.

Meya wa Manispaa hiyo, Raymond Mboya, alisema kuwa uboreshaji wa dampo hilo utasaidia kuboresha usafi wa mazingira katika mji wa Moshi, kwa kuwa kwa muda mrefu lilikuwa katika hali isiyoridhisha.

"Tunategemea uboreshaji wa dampo hili utasaidia Manispaa kuendelea kuongoza katika usafi wa mazingira, kwani sasa itakuwa inatupa taka zake kwenye sehemu inayokidhi viwango vya usafi na utunzaji wa mazingira," alisema Meya Mboya.

Manispaa hiyo ipo kwenye mchakato wa ujenzi wa dampo la kisasa pamoja na kujenga kiwanda kitakachotengeneza mbolea kwa kutumia takataka ambacho kitatoa fursa ya ajira kwa wananchi na kugeuza takataka hizo kuwa mali.

Alisema lengo la Manispaa ya Moshi ni kuendelea kuwa kinara katika usafi na utunzaji wa mazingira hapa nchini.

Mwishoni mwa mwaka jana, Manispaa hiyo ilinunua malori mapya matatu ya kisasa kwa gharama ya zaidi ya Sh. milioni 613.5.

Magari hayo aina ya Compactor yakiwamo mawili ya kushindilia taka na moja la kubeba matangi makubwa ya kuhifadhia taka, yanatajwa kama suluhisho la tatizo la uzoaji taka, kwa kuzoa taka tani 96 kwa siku.

Katika hafla hiyo ya utiaji saini, Mkuu wa Idara ya usafi na mazingira wa Manispaa hiyo, Danford Kamenya alisema kuwa uboreshaji wa dampo hilo utafanyika katika eneo la Mtakuja na uboreshaji huo utakuwa ni kujenga eneo la kuzikia taka ngumu, kujenga uzio na kujenga ofisi ya Meneja wa Dampo.

Hata hivyo, Kamenya alisema kuwa mradi huo wa uboreshaji wa dampo utafanyika kwa muda wa miezi sita na utasaidia utupaji wa taka ngumu kwa njia ya kisasa kwa taka hizo zitakuwa zikiwekwa kwenye shimo hilo na kisha kufukiwa kwa udongo na kushindiliwa mara kwa mara.

# ama

**ALHAMISI JUNI 6 2019**

AFYA NA MAZINGIRA



**Aonja ahueni baada ya makali miaka 40**

Ukurasa 17



MAKUBWA VITA YA FISTULA NCHINI

Ukurasa 18




Ukurasa 16

**TGNP: Hii ndio operesheni rasmi inayowabakisha mabinti shuleni**



# Waganga wa jadi waingizwa darasani kukabili TB, Ukimwi

Ukurasa 14


Mlo uliojaa sukari. **PICHA: MTANDAO.**

## Sukari inachukua nafasi ya sigara?

**Mwandishi Wetu**

TANGU kuanza kampeni kuu mwaka 2007, sigara imepigwa vita kwa kiwango kikubwa zaidi, kuwakatisha watu kuendekeza hiyo tabia inayobebesha magonjwa na kuathiri tabia.

Wakati kuna sura hiyo ya mafanikio, kuna upande wa pili unaoendelea na kuendekeza tabia ya kupenda kutumia vitamu vya sukari, sasa nayo imekuwa janga jingine la kiafya, kuchukua nafasi ya sigara.

Sigara ambayo ni kinara wa maradhi kama kansa na kifua kikuu, ndugu yake sukari anakuwa bingwa wa maradhi ya kisukari na mengineyo.

Taasisi ya Utafiti wa Sera za Kodi za Umma(IPPR), kupitia ripoti yake mpya, inasema kuna hatua zilizochukuliwa katika baadhi ya vitamu vya sukari, kama vile juisi, kutozwa kodi kubwa.

Mkurugenzi wa IPPR, Tom Kibasi, anasema mwelekeo mpya sasa unaangukia katika bidhaa kama pipi na zingine zinazofanana nazo, yote ni kutanua wigo wa vita dhidi ya matumizi ya sukari.

Hata hivyo, ni hoja inayopata upinzani kutoka viwanda vya kuzalisha vyakula nchini Uingereza, vikilalamika kwamba vinaingiliwa katika uhuru wao wa kuzalisha vyakula na vinywaji, ikizingatiwa vimo katika upinzani mkali.

Hata hivyo, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, inasema haijafikia uamuzi na inachokisubiri sasa ni kauli ya Mganga Mkuu wa Serikali, Profesa Dame Sally Davies.

Ni mara kadhaa, Mganga Mkuu, huyo ametakiwa kuongeza nguvu kiasi ili kuchukua hatua zaidi kuelekea mafanikio.

AFYA

# Waganga wa jadi waingizwa darasani kukabili TB, Ukimwi

- Wachimbaji madini hali yao inatisha
- Yaliyoko Kahama yanatajwa 'usipime'


Ofisa Mradi wa Kifua Kikuu wa Halmashauri ya Mji Kahama, kutoka katika shirika lisilo la kiserikali la SHDEPHA+ Annasia Mringo, akitoa elimu juu ya ugonjwa. **PICHA: SHABAN NJIA.**

**Na Shaban Njia, Kahama.**

KIFUA kikuu kinatajwa kuwamo katika orodha ya magonjwa makuu matatu yanayowatokea watu masikini na matajiri duniani.

Ni maradhi yanayoingia katika orodha tajwa mchangiaji mkubwa upoteaji wa nguvu kazi ya Taifa, huku magonjwa mengine, ikiwamo malaria na ugonjwa wa Ukimwi.

> **"Mariam Mabanga, ni Mratibu wa Kifua Kikuu na Ukoma kutoka katika Hospitali ya Halmashauri ya Mji Kahama...**

Kurejea tawimu kutoka Kituo cha Hesabu ya Watu cha Marekani (US Census Bureau), maradhi hayo yanatajwa kusababisha vifo vya asilimia 10 ya watu wote duniani, wanaokisiwa jumla la yao ni bilioni 6.91.

Nchini Tanzania, taarifa ya shirika la USAID ya mwaka 2007 inatamka kulikuwapo watu 120,191 waliokisiwa kuumwa kifua kikuu kila mwaka. Kati yao 56,233 waligundulika kuwa na makohozi tata.

Pia, vifo vinavyotokana na ugonjwa huo nchini vilihesabiwa kufika 32,000 kila mwaka, kwa takwimu hizo za wastani wa kipindi hicho.

**SHDEPHA+ Kahama**

Katika kupambana na Kifua Kikuu na Ukimwi nchini, shirika lisilo la kiserikali la SHDEPHA+ wilayani Kahama, mkoa wa Shinyanga kwa kushirikiana na halmashauri za kutoka mikoa ya Geita na Shinyanga, zilitoa elimu kwa waganga wa jadi 12, lengo ni kuwawezesha kutambua dalili za ugonjwa huo.

Ni hatua inayoelezwa inatokana na wagonjwa wengi wanapopata na maradhi hayo, wanakimbilia kwao kupatiwa matibabu, maamuzi yayaotajwa kuwa ya hatari, kwani wapo wengi waliopoteza maisha, imani kubwa ikiangukia katika hisia wamerogwa.

Wilayani Kahama, kunatajwa kuwa na wagonjwa wengi wa kifua kikuu na ukimwi, hali inayotajwa inachangiwa na mazingira ya kuzungukwa na migodi mingi midogo, vilabu vya pombe na magulio mengi.

Inaelezwa kwamba, ndio hali inayoikabili Mkoa wa Geita, hasa kwenye wilaya za Bukombe na Bongwe, hivyo katika mafunzo hayo walihusishwa na wilaya nne za Bukombe, Mbongwe za mkoani Geita, pia kuna Halmashauri za Msalala na Kahama Mjini, kutoka mkoani wa Shinyanga.

Ni sehemu ya mapambano mahsusi ya kupunguza kasi ya kuenea maradhi hayo, inayoangukia katika kupoteza nguvu kazi ya Taifa.

Mariam Mabanga, ni Mratibu wa Kifua Kikuu na Ukoma kutoka katika Hospitali ya Halmashauri ya Mji Kahama, anayesema kuwa mpaka sasa wameshawafikia waganga wa jadi 12 na kuwapatia maudhui ya dalili za ugonjwa huo.

Mratibu huyo anaainisha mgawanyo wao kiwilaya: Mbogwe na Msalala, kuna washiriki wawili kila moja na Kahama Mjini, imehudhuriwa na waganga watano.

Anasema, katika utendaji hao awali, ni mmoja tu kutoka Halmashauri ya Kahama Mjini, ndiye amekuwa akipeleka wagonjwa wa kifua kuku na ukimwi kila mara wanapomfikia na akawagundua wana maradhi hayo.

"Hatuwezi kupambana wenyewe kama wauguzi katika vita ya ugonjwa wa TB na Ukimwi. Ili tuweze kufanikisha vita hii, tuliona ni vyema kuwapatia elimu waganga wa jadi juu ya kuzitambua dalili za ugonjwa huu, ili watakapopata wagonjwa wa namna hiyo, waweze kutuleta katika vituo vyetu kwa kutolewa huduma za afya," anasema Mabanga.

**TB ILIVYO**

Mariam anataja chanzo cha kasi kubwa ya Ukimwi Kahama,

Inaendelea Uk. 15

AFYA

Inatoka Uk. 14

ni kutokana na mji kuzungukwa na utitiri wa migodi, vilabu vya pombe na kumbi za sterehe, yote yanajenga mazingira rahisi ya kuambukizana kutoka kwa wenye virusi hasi kwa wasio navyo.

Pia, anatoa takwimu kwamba, kuanzia kipindi cha mwezi wa Januari hadi mwezi uliopita, wameshatoa huduma za watu 428, wakiwamo wagonjwa wa maradhi hayo. Lengo lao ni kuwafikia wananchi 1,001 ifikapo mwisho wa mwaka huu.

Anatoa masikitiko yake, kwamba wananchi wengi bado hawana mwamko wa kupima afya zao ili wajitambue, badala yake wamejitokeza kupima maambukizi ya virusi vya ukimwi kwa msukumo kama ushirikiano na asasi kama SHDEPHA+, ambayo inatoa elimu nyumba kwa nyumba.

# Waganga wa jadi waingizwa darasani kukabili TB, Ukimwi



Mgonjwa akipatiwa huduma nyumbani.**PICHA: MTANDAO**

**MIGODINI/VILABUNI**

Ofisa wa mradi huo katika halmashauri ya mji kutoka shirika lisilo la kiserikali la SHDEPHA+ Annasia Mringo, anaelekeza mtazamo mahsusi kwamba asilimia kubwa ya wanaoambukizwa ni wanaotoka maeneo ya migodi midogo, viwandani, vilabu vya pombe, magulio na sokoni na kinamama wanaojihusisha na biashara ya ngono.

Anataja njia ya kutokomeza ugonjwa huo, ni umuhimu wa wataalamu wa afya kushirikiana na wataalamu wa SHDEPHA+ wanaowafuata moja kwa moja wakazi wa migodi na vilabu vya pombe, kupata elimu stahiki kuhusu ugonjwa huo, ili waanze maisha chanya.

Mringo anasema, wameweka wataalamu katika kila kata, wanaotoa elimu ya kifua kikuu. Utaratibu wao ni siku, wataalamu hao wanatembea kuwaelimisha wananchi mmoja mmoja au kwa nyumba na kuchukua vipimo vya makohozi, kwenda kuyapima.

Anasema, katika kipindi cha kuanzia mwezi Oktoba mwaka jana, hadi sasa, wamewatembelea wagonjwa 69,521 na waliofanyiwa uchunguzi ni 52,509.

Pia, anasema katika hao waliofanyiwa uchunguzi, waliotoa makohozi kwa ajili ya vipimo jumla yao ni 6,704; katika kundi hilo 6,358, walibainika kuwa na TB.

**CHANGAMOTO**

Mratibu wa Kifua Kikuu na Ukimwi kutoka Halmashauri ya Bukombe, Dk. Joshua Mazingo, anasema changamoto wanayoipata katika utoaji huduma kwa wagonjwa, ni baadhi yao kukatiza dozi wanazopewa, hivyo inaathiri matibabu kwa jumla.

Anafafanua kuwa, asilimia kubwa kati yao wanaobainika kukatiza dozi za TB ni wachimbaji wadogo, wanaoishi maisha ya kuhama, hali inayojenga usugu wa maradhi, hata baadhi tiba zao zinachukua wastani wa miezi 20 kupona.

Pia, anasema kuna baadhi ya zahanati zilizopo jirani na migodi au pembezoni, hazina vifaa maalumu vya kupima ugonjwa huo, hali inayochangia wagonjwa kupata vipimo na matibabu ya haraka, kabla ya kufikia usugu wa maradhi yanayowakabili.

Lingine linalotajwa ni kuwapo maadhi ya kifua kikuu kinachosambaa kwa kasi, kutokana na wagonjwa wake wanachangamana na wasioumwa, hasa katika zahanati, vituo vya afya na hospitali.

Dk. Mazingo, anatumia nafasi hiyo kuiomba serikali kujenga kiliniki za wagonjwa wa kifua kikuu, kama ilivyofanyika katika kutenga eneo la kugawa dawa za kufubaza virusi vya Ukimwi na kifua kikuu, ili wasiendelee kuchangamana na wasioumwa.

**WACHIMBA MADINI**

Mchimbaji madini mdogo, Allex Thomas, mkazi wa Arusha, anayepatikana katika Mgodi wa Mwime Ilindi, anakiri wachimbaji wanafanya kazi kwenye mazingira hatarishi na rahisi kupata kifua kikuu na ukimwi.

Thomas anasema, mara nyingi ugonjwa huo hupatikana kwa wachimbaji wanaoingia shimoni kufanya kazi yao, vivyo hivyo wasaga mawe ya dhahabu.

Kuhusu wachimbaji kukatiza dozi za kifua kikuu, kwa kuwa maisha ya wachimbaji ni ya kuhama na anaposikia kuna mahali kunapatikana dhahabu kirahisi, hukimbilia huko na kutelekeza dozi wanazoendelea nazo, wakitoa kipaumbele katika mwelekeo huo mpya wa riziki.

Thomas anajumuisha mtazamo wake, akishauri kwamba ili kupambana na ugonjwa huo, ni vyema serikali ikashirikiana na mashirika mbalimbali kutoa huduma za kiafya na elimu inayohusu athari za ugonjwa na upatikanaji wa tiba.

Anasema, ni hali itakayomfanya mchimbaji kuwa balozi au makini kwa mwenzake, akishauri ni umuhimu wa kupata huduma hizo za kiafya.

**MPANGO WA 2017/18**

Mpango wa Kuhudumia Wagonjwa wa Kifua Kikuu mahali waliko, katika wilaya hizo tajwa ulishawahi kuwapo na kudumu kwa wastami wa miezi 18, kati ya mwezi Machi mwaka 2017, hadi Agosti mwaka jana.

Ni mpango ulioandaliwa kujenga uwezo wa wagonjwa wanaoendelea kutibiwa majumbani, ikiwa ni sehemu ya vita dhidi ya maradhi hayo ya kifua kikuu.

Miongoni mwa mambo muhimu yanayosimamiwa kupitia mpango huo, ni kutumia, kujenga uwezo, na kushirikiana na wanajamii waliko, kuanzia hatua ya kukitambua kifua kikuu katika halmashauri za Mjini Kahama Mjini na Wilaya ya Msalala.

Ni mpango uliofanyika kwa kuwafikia watoto, wachimbaji wadogo na jamii kwa jumla wengine, wakifuatilia hata walio na dalili chanya za maradhi hayo.

Malengo ya mpango huo yanatajwa kuwa ni katika maeneo manne: Mosi, ni kuboresha nafasi ya serikali za mitaa katika kuhudumia maradhi ya kifua kikuu, katika makundi maalum yanayoathirika na maradhi hayo. Pili, ni kuongeza namba bora ya kuwafikia na kuwatambua wanaosumbuliwa na kifua kikuu na jamii husika kwa jumla.

Tatu, kuimarisha baadhi ya watu maalum watambuzi wa tabia inayolengwa kutoka ndani ya jamii jumuiya maalum na nne, ni kuunda mfumo sahihi wa marejeo ya wagonjwa, katika namna ya usimamizi mahsusi, tathmini na kujifunza ilivyo picha halisi

Ni mpango unaotekelezwa kupitia vigezo mahsusi vya Mpango wa Taifa wa Ukimwi nchini, ambayo ina miongozo katika mitazamo ya njia maalum, mitaala na mbinu mahsusi.

> **Anataja njia ya kutokomeza ugonjwa huo, ni umuhimu wa wataalamu wa afya kushirikiana na wataalamu wa SHDEPHA+ wanaowafuata moja kwa moja wakazi wa migodi na vilabu vya pombe, kupata elimu stahiki kuhusu ugonjwa huo, ili waanze maisha chanya.**

AFYA

SIKU YA HEDHI SALAMA

# TGNP: Hii ndio operesheni rasmi inayowabakisha mabinti shuleni

■ Matundu ya vyoo vya wanafunzi hayatoshi



Walemavu wasioona walipohudhuria mafunzo ya hedhi salama wilaya ya Chamwino, jijini Dodoma. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**Na Yasmine Protace**

HEDHI salama inatafsiriwa kuwa njia salama ya kumsaidia msichana na hata mwanamke, asipatwe na magonjwa ya kizazi.

Ili kuliweka hilo katika mafanikio, kunashauriwa elimu iendelee kutolewa kwa wanajamii ili waweze kutumia njia hiyo salama, kwa manufaa ya afya yao ya baadaye.

Inaelezwa kuwa, matatizo ya wanawake kuhusiana na uzazi yanasababishwa na kushindwa kukabiliana na historia zao, hasa walipokuwa katika umri mdogo.

Ni kauli ya Mkurugenzi Mtendaji wa asasi ya TGNP Mtandao, Lilian Liundi, katika ufunguzi wa mdahalo wa maadhimisho ya Siku ya Hedhi Salama, uliofanyika jijini, akisisitiza 'hedhi salama' ni mkombozi kwa mwanamke.

Mdahalo huo wa siku moja, ulihudhuriwa na madiwani, maofisa kutoka halmashauri za manispaa, walimu wa shule za msingi na sekondari na wadau kutoka asasi za kiraia na wanafunzi.

Katika ufunguzi, Lilian anasema Siku ya Hedhi, ni ya kimataifa inayolenga kujenga uelewa na kupaza sauti kuhusu upatikanaji huduma nzuri za kusaidia wanawake wawe salama,

**"Siku hii inatupa fursa kujadili na kutafakari juu ya mifumo yetu, kama nchi tunavyosimamia masuala ya hedhi salama. Kaulimbiu ya mwaka huu ni wakati ni huu chukuwa hatua," anasema.**

wanapofikia hedhi. Hiyo inaadhimishwa kila inapofika Mei 28 ya mwaka.

"Siku hii inatupa fursa kujadili na kutafakari juu ya mifumo yetu, kama nchi tunavyosimamia masuala ya hedhi salama. Kaulimbiu ya mwaka huu ni wakati ni huu chukuwa hatua," anasema.

Anaongeza kuwa TGNP Mtandao katika kutekeleza kaulimbiu ya mwaka ya kimataifa, wanasisitiza kaulimbiu yao inayosema "Tenga bajeti kugharamia mahitaji ya hedhi salama shuleni."

Anasema imani yake ni kwamba serikali za mitaa na kuu, zitatoa kipaumbele kwa jambo hilo, changamoto zinazowakumba wasichana shuleni na wanawake kuhusiana na ukosefu wa nyenzo za kufanikisha hedhi salama.


Lilian anaongeza kuwa, Umoja wa Mataifa uliupa uzito wa kipekee siku hiyo, baada ya kugundua katika nchi zinazoendelea, mwanamke anapokuwa katika hedhi hutaabika.

Anafafanua kwamba mazingira ya tabu hiyo, yanagusa uhaba wa vifaa vya kujisitiri na vina gharama kubwa, ambavyo hawawezi kuvimudu.

Lengo la TGNP Mtandao, ni kukutana na wadau kujenga utamaduni wa kuvunja ukimya, kuondoa woga wa kutamka wazi kuhusu changamoto zinazowakumba wanawake wakiwa kwenye hedhi, hasa watoto wa shule za msingi na sekondari.

Anasema TGNP Mtandao, inaendelea na kampeni iitwayo 'wape mabawa' inayolenga kuhakikisha wasichana wanapata mazingira salama ya kuelimika.

Lilian anasisitiza kwamba, njia kuu ya ufanikishaji lengo ni kuvunja ukimya, kushawishi watunga sera watenge bajeti za kutosha, kuwezesha upatikanaji taulo za kike na vifaa vingine, matundu ya kutosha ya vyoo shuleni na upatikanaji maji safi na salama.




Mkurugenzi huyo anajisifu kuwa, kwamba hadi sasa wameshaanza kuona mabadiliko makubwa kwenye halmashauri kadhaa nchini, akizitaja kuwa ni za: Kishapu, Kisarawe na Manispaa ya Ilala, Mbeya, Morogoro kote kupitia bajeti zao, zimeonyesha wana nia thabiti ya kukabiliana na changamoto hizo.

"Halmashauri hizo zimejipanga na zimetenga fedha kwenye bajeti kutoka makusanyo ya ndani, kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya vyoo, ili kukidhi mahitaji ya wasichana wanapokuwa kwenye hedhi na kutoa pedi," anasema.

Anaongeza kuwa suala la hedhi salama, lina changamoto zaidi kwenye nchi zinazoendelea, ambako maji na vyoo havitoshi katika shule nyingi.

Kwa mujibu wa Lilian, asilimia 98 ya shule za sekondari na asilimia 99 shule za msingi walizozitembelea, haziendani na mwongozo wa kitaifa wa ujenzi wa vyoo shuleni,

kati ya matundu yaliyopo na idadi ya wanafunzi.




Wanafunzi katika harakati na mafunzo ya kutetea hedhi salama.

Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi, katika taarifa yake imeeleza asilimia 72.7 ya shule zote haijafikia uwiano wa tundu moja kwa kila wanafunzi 20 kwa wasichana na wastani huo wa tundu, kwa wavulana 25.

Pia, inarejewa wizara hiyo ikisema asilimia 11 tu ya shule ndio zina vyoo bora, kwa mujibu wa utafiti wa shirika la SNV, wa mwaka 2014.

Jingine ni kwamba, hadi sasa asilimia 99 ya shule nchini hazina huduma ya maji, wala vyumba vya kubadilishia wakati wa hedhi.

Anaueleza utafiti uliofanywa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia watoto (Unicef) katika mwaka 2009, ulionyesha asilimia nne ya vyoo vya shule ndio viko kwa ajili ya watoto walemavu masomoni.

Anautaja utafiti mwingine wa wa asasi anayoiita NMR mwaka 2016, wanaeleza asilimia 98 ya shule zina idadi ndogo ya sehemu ya kunawia mikono.

Dk. Rosemery Daniel, anayetoka asasi ya Tawasanet, anasema wadau wa masuala ya maendeleo na hedhi salama, wamekuwa wakiwaangalia wadau wa shuleni, mitaani na vijijini na wamebaini makundi hayo yana changamoto kubwa za kila siku.

Dk. Rosemary anasema katika malengo yao, wamebaini kukosekana elimu ya hedhi salama na upatikanaji maji katika maeneo waliopita.

Inaelezwa, mwaka 2010 serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi, imeshaanzisha miongozo inayotaka kuwapo matundu sahihi ya vyoo kwa wasichana na wavulana.

Ni jambo ambalo ndau huyo analalamika kasi yake imeanza kurudi nyuma, kwa sababu ya upungufu wa vyumba vya wasichana kujisitiri wakiwa katika hedhi na vyumba hivyo sasa vinatumika kuhifadhi fagio na taka ngumu.

Anasema, utafiti walioufanya

**"Halmashauri hizo zimejipanga na zimetenga fedha kwenye bajeti kutoka makusanyo ya ndani, kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya vyoo, ili kukidhi mahitaji ya wasichana wanapokuwa kwenye hedhi na kutoa pedi," anasema.**

wamebaini maduka vijijini hayana taulo za kike, hali inayo sababisha upatikanaji wake kuwa mgumu vijijini.

Baadhi ya wanafunzi walioshiriki katika mdahalo huo,walitoa maoni yao kwamba pedi wanazopewa haitoshi, wakitoa mfano moja wanayopewa wanaitumia kutoka asubuhi hadi jioni kiafya sio sahihi.

**MWALIMU ANENA**

Janeth Boma, ni Mwalimu wa Shule ya sekondari Mabibo, jijini Dar es Salaam, anasema katika shule yake wapo wanafunzi w 700 na matundu ya vyoo sita na hakuna.

maeneo ya kujihifadhi.

Ombi lake ni halmashauri yake katika bajeti husika, iwapatie fungu la fedha kuokoa hali ya mtoto wa kike.

Devotha Stewart, ni mwalimu Shule ya Furaha, anayesema,

INAENDELEA UK.20

# Aonja ahueni baada ya maumivu makali miaka 40

**Na Mwandishi Wetu**

HUJAFA hujaumbika. Ndivyo methali inavyotamka. Mwanamama Mwingereza Alison Cameron, leo hii anajisikia nafuu dhidi maumivu.

Ni hali inayomfanya ageuke nyuma kukumbuka historia, wakati alipokuwa binti mwenye umri wa miaka 17 pekee.

Mzee huyo wa leo anakumbuka ilipomtokea kwanza akaugua kidole tumbo au kitaalamu 'stomach appendix' yaliyotawala maumivu makali sana kwa miongo minne, hata akafikia hatua mbaya zaidi na mateso ya kiafya.

Kilichodumu wakati wote huo ni maumivu makali ambayo yalidumu kwa miaka 40, sasa akiwa na wajukuu, ilhali wakati yalianza alikuwa ni kijana.

Madaktari walichukua hatua ya kumchoma sindano nyingi za kudhibiti maumivu hayo pasipo mafanikio, hatua iliyochukuliwa kwa miezi sita.

Hapo akafikishwa hatua kubwa ya kupatiwa dozi za ziada ambazo ziliumuumiza maradufu. Hakuweza kula na kuna wakati alilazimika kulishwa kwa mipira, maana hali ya maumivu hayo yalimwia mbaya zaidi.

Lakini Alison anasema, pamoja hali hiyo ngumu, kila penye dalili za nafuu alijitahidi kukabili uhalisi kwa kujaribu kufurahi aendane na uhalisia katika jamii, 'akijichanganya' katika kile kinachotokea kwa umma.

"Mimba zangu zilitoka mara saba, mara sita nikiwa katika maumivu makali," anaeleza Alison, ambaye pamoja na changamoto hizo, alijitihadi katika uzazi na amefanikiwa kupata watoto wawili na sasa ana wajukuu watatu.

Miaka mitano iliyopita alipata matatizo makubwa ya mapafu na alilazimika kukimbizwa kwa daktari bingwa katika hospitali iliyoko katika Chuo Kikuu cha



Alison Cameron akiwa na mumewe, Girish Vajramani. **PICHA/MAKALA: MTANDAO.**

Southampton, Uingereza kutibiwa.

Ubunifu wa madaktari bingwa hao, walau ndio uliweza kutoa majibu ya kumsaidia na wanasema ilimpunguzia nusu ya maumivu aliyodumu nayo, huku akiishi katika masharti maalum ya kitabibu yaliyomsaidia.

Pia, alitembelea baiskeli ya wagonjwa, akikumbuka ni wakati aliyopata wajukuu, kwamba alitumia fursa hiyo kufurahi nao kwa namna mbalimbali.

Inaelezwa kwamba, mabingwa hao wa tiba walijitahidi kumsaidia, ikiwa ni pamoja na kutafuta maoni nje ya nchi kwa mabingwa wenzao, lakini wigo wa ujuzi wao uligota.

Ilifika hatua, daktari mmoja bingwa alifanya ubunifu wa kumuingizia kifaa cha kielktroniki katika mfumo wa mishipa mkuu wa fahamu unaopita mgongoni hadi kichwani, kazi iliyofanyika kupitia operesheni mbili, ndipo mafanikio yakashuhudiwa maumivu kusita.

Hilo lilifanyika Desemba mwaka jana. Hapo ndiko kwenye siri ya maumivu kumtoka mama huyo mwenye miaka 57 sasa.

Anasema ilimchukua wiki tano upo maumivu ya miaka nenda rudi kutoweka, huku akijivunia maisha mapya ya kuweza kula, kunywa na kujichanganya na wenzake.

Moja ya anayoyafurahia, katika maelezo yake huku akitabasamu ni kwamba anachekelea sherehe ya Krismas, iliyopita, kwamba alikula, kunywa ndani ya furaha, jambo alilolisahau kwa miaka 40, muda mwingine akila na kunywa kwa mpira

AFYA

# MAKUBWA VITA YA FISTU

- Aliyetaabika miaka 20 asimulia ya kwake
- CCBRT: Asilimia 80 hohehahe, elimu duni
- Dar imedhibiti; Rukwa, Kusini hali mbaya
- Miaka 16 wagonjwa 7,000 wahudumiwa

**Na Yasmine Protace**

VITA ya fistula sasa inatajwa na kuzungumzwa kila mahali na kila wakati. Lakini, fistula ni nini? Ufafanuzi wake ni kwamba tundu lisilo la kawaida linalotokea katika kibofu cha mkojo na sehemu zote za siri za mwanadamu.

Ni ugonjwa unaompa adha ya kiafya na kiheshima na matokeo mazuri yake ni kwamba, mhusika anashindwa kujizuia haja ndogo.

Chanzo cha maradhi hayo ni pale mwanamama anakuwa na uzazi pingamizi, bila ya kuwa na huduma ya haraka kumasaidia.

**BOSI CCBRT**

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya CCBRT, Brenda Msangi, anatamka katika Siku ya Kimataifa ya Kutokomeza Fistula ya Uzazi Duniani, kwamba mtu anatakiwa kutafakari, akigeukia alikotoka an aliko sasa, akifikiria namna ya kuendelea na juhudi za kuitokomeza fistula ya uzazi nchini.

Anasema, Umoja wa Mataifa ulianzisha mwongozo wa kutokomeza fistula mwaka 2003, ikiwa ndicho kipindi nacho CCBRT ilianza kutoa matibabu ya fistula.

"Kama mnavyojua fistula inatokea Kwa wingi Afrika, hasa Kusini mwa Jangwa la Sahara na Asia," anasema Brenda na kufafanua ni miaka mingi sasa mataifa ya magharibi, walishafanikiwa kutokomeza fistula katika jamii zao.

Brenda anasema, ni hatua iliyofikiwa kwa matunda ya juhudi za pamoja na mikakati, jambo linalowezekana katika nchi zinazoendelea katika utokomezaji wa maradhi hayo.

"Kaulimbiu ya mwaka huu inasema fistula ya uzazi ni ukiukwaji wa haki za binadamu tuitokomeze sasa," anasema Brenda.

Anasema, CCBRT ni moja ya wadau wakuu kwenye harakati za kutokomeza fistula nchini na imekuwa ikitoa mchango mkubwa katika kinga na matibabu.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, mradi wa mama na mtoto umezuia fistula mpya kutokea mkoani Dar es Salaam, huku katika hospitali ya CCBRT, kukijengwa wodi za uzazi na vyumba vya upasuaji.

Anasema, ni maboresho yanayovifikia vituo vingine vya afya 22 kusaidia utoaji wa vifaa muhimu vya huduma ya uzazi katika hospitali na vituo vya afya 24 na kuimarisha mifumo ya uboreshaji huduma za afya katika hospitali na vituo 23.

Brenda anaeleza kuwa, lingine wanalofanya ni utoaji mafunzo kwa watoa huduma za uzazi na watoto, ili kuimarisha maarifa na stadi zao kikazi, lengo ni kifanikisha huduma bora kwa kinamama, ambao ni moja ya walengwa




Kutoka kushoto ni Meneja Programu ya Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto kutoka UNFPA, Feldter Bwana, Mkurugenzi Mtendaji CCBRT, Brenda Msingi na Mkurugenzi Mkazi AMREF Health Tanzania, Dk.Frolence Temu, wakizungumzia Siku ya Fistula hospitalini. CCBRT. **PICHA ZOTE: YASMINE PROTACE.**

> **"Kaulimbiu ya mwaka huu inasema fistula ya uzazi ni ukiukwaji wa haki za binadamu tuitokomeze sasa," anasema Brenda.**

wakuu katika eneo hilo.

Brenda anasema, CCBRT tangu mwaka 2003 imeishatibu kinamama zaidi ya 7000, katika wastani wa wagonjwa 400 kila mwaka.

Anafafanua kuwa, katika kundi hilo wengi ni jamiii kutoka hali ya chini kiuchumi, asilimia 80 (wastani wa 560) wa elimu isiyovuka ya msingi.

Vivyo hivyo, anasema katika kundi hilo la wagonjwa 560, asilimia 35 katika yao (wastani wa1960) hawakusoma kabisa.

Anasema, kinamama hao wana uwezo mdogo kifedha unaowafanya wasimudu nauli za kuja na kurudi hospitalini kutoka makwao, gharama za matibabu, malazi na chakula. Wanapatiwa huduma hizo.

**KUTOKA UNFPA**

"CCBRT pamoja na hospitali washiriki, tunaendelea kutoa matibabu ya fistula kwa kila wanawake wenye tatizo hilo, ambaye anajitokeza bila ya malipo yoyote, ikiwa ni pamoja na nauli ya kuja hospitali na kurudi nyumbani baada ya matibabu," anaeleza mwakilishi waa Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA).

Felister Bwana, ni Meneja Programu, Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto, kutoka UNFPA anayesema kuwa kuendelea kuwapo fistula katika jamii, kunamaanisha kuwapo uhaba mkubwa wa baadhi ya huduma.

Bwana, anataja maeneo hayo ni upatikanaji huduma za afya ya uzazi na vikwazo katika mfumo mzima wa afya, changamoto kubwa inayowakabili wanawake na wasichana.

Anasema, hapo inajumuisha mambo kama umasikini, unyanyasaji wa kijinsia, ukosefu wa elimu, kushindwa kuendelea na masomo, ndoa na mimba za utotoni .

"Kila siku wanawake 800 hupoteza maisha duniani kutokana na matatizo ya ujauzito," anasema na kuongeza kwamba wapo wengine 100,000 wanaopata tatizo jipya la ugonjwa huo kila mwaka



Baadhi ya wagonjwa wanaopata matibabu ya fistula katika Hospitali ya CCBRT, Siku ya Fistula, hospitalini hapo.

AFYA

# ...LA NCHINI



Bwana anafafanua kuwa fistula ya uzazi ni moja ya majeraha makubwa wapatayo kinamama wakati wa kujifungua, akisema: "Tatizo hili linazuilika na kwa walio wengi wametibiwa kwa njia ya upasuaji."

Anafafanua kuwa juhudi zimeshafanyika na wakati huo huo, kuna uhitaji mkubwa wa kuwasaidia wahanga wa fistula, kwa takwimu zinaonyesha hali si nzuri.

Bwana anasema, tangu mwaka 2003 UNFPA imekuwa inaongoza kuratibu kampeni kutokomeza fistula duniani, ikishirikiana na wadau wengine.

Anasema, UNFPA inapoadhimisha miaka 50 ya kuzaliwa, inafurahi kusema ilichokianzisha kimewasaidia wanawake na wasichana 105,000 kupata huduma ya upasuaji kutibu fistula, tangu mwaka 2003.

Mwakilishi huyo anataja mwaka huu, ambao unakaribia nusu kuna wanawake na wasichana 10,000 waliokwishafanyiwa kwa msaada wa UNFPA, ni kampeni iliyopo katika nchi 55 za Afrika.

Anaongeza kuwa, kidunia zaidi ya wanawake wasichana 9,000 wamepatiwa mafunzo na ujuzi aina mbalimbali na kupewa mitaji midogo ya kuanzisha biashara baada ya matibabu.

Vilevile, shirika linafanya kazi ya kuwajengea uwezo zaidi ya wahudumu wa afya 4,000 nchini, wamudu kutoa huduma kwa wagonjwa wa fistula. Nchini Tanzania, anasema UNFPA inashirikiana kwa karibu na baadhi ya wadau kuboresha afya ya uzazi, mama mtoto na vijana, ili kupunguza vifo vya kinamama na watoto na matatizo yatokanayo na uzazi, ikiwamo fistula.

Anataja baadhi ya wadau hao ni Wizara za Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee an Watoto; Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali ya Mitaa (Tamisemi)' na mashirika mengine yasiyo ya kiserikali, kama CCBRT na Shirika la Afrika Linaloshugulika na Utafiti wa Tiba - AMREF.

Bwana anasema, UNFPA imeendelea kununua dawa za uzazi wa mpango na dawa zingine zinazotumika kuokoa maisha ya mtoto na mama wakati wa kujifungua, lengo ni kuzuia mimba zisizotarajiwa, zile za utotoni na zinazoendelea kuchangia kutokea fistula.

> **"AMREF tunataka kinamama warudi katika biashara, tumekuwa tukichangia kudumisha masuala ya lishe na kuwalenga vijana walio katika umri wa kuzaa" anasema.**



Kwa mujibu wa ofisa huyo, UNFPA imejipanga kutokomeza fistula ya uzazi ndani ya kipindi cha Malengo Endelevu ya Maendeleo, ifikapo mwaka 2030.

**BOSI AMREF**

Mkurugenzi Mkazi wa AMREF nchini, Dk Florence Temu, anaitafsiri fistula ya uzazi kuwa ni kiukwaji mkubwa wa haki za binadamu.

Dk Temu anasema, kupitia AMREF yenye umri zaidi ya miaka 60 sasa ikichangia huduma za afya, mwaka

mwaka 2002 kwa kuungana na wadau wengine, ilichukua hatua za kupigana kutokomeza fistula.

"AMREF tunataka kinamama warudi katika biashara, tumekuwa tukichangia kudumisha masuala ya lishe na kuwalenga vijana walio katika umri wa kuzaa" anasema.

Anaongeza kuwa hivi sasa AMREF imechangia kufungua wodi za wazazi, kuwawezesha mabinti kupata taarifa za uzazi, kuboresha afya zao na lishe kwa jumla .

Dk. Temu anasema tangu mwaka 2002 mpaka sasa, kuna wahudumu zaidi ya 1000 waliowekwa kutoa huduma hiyo na wamekabidhi vifaa tiba 41 katika ngazi ya wilaya na mkoa.

Anatoa mfano wa wilayani Magu, ambako kuna janga la fistula, waliwasaidia kinamama 50 kurudi katika maisha ya kawaida, ikiwa sehemu ya vita kwa kushirikiana na serikali, kukabili na kukomesha fistula nchini.

**TATIBU WA FISTULA**

James Chapa, ni daktari wa CCBRT anayetibu ugonjwa wa fistula na Rais wa Chama cha Fistula Tanzania, anasema hivi sasa ni mwaka wa tisa tangu kuanzishwa chama hicho.

Anasema kuna uwezekano kwa mwanamke kukingwa dhidi ya kuugua fistula na hata kutokomeza kabisa ugonjwa huo, iwapo kunahatua thabiti katika hilo.

Dk. Chapa anasema mwongozo wa kutibu fistula unaandaliwa kwa njia zinazomfanya mgonjwa apate matibabu bora na anafafanua:

"Watu wanaotibu fistula, wanatakiwa wawe na ujuzi mkubwa katika kutoa matibabu na kuhakikisha mama aliyepata fistula hapati tena fistula," anasema.

Kwa mujibu wa daktari huyo, kila mwaka kuna wagonjwa wapya 3000 wa fistula, lakini wanaofika kupata matibabu ni nusu yao ambao jumla yao ni 1500 .

Anasema madaktari bingwa wa fistula nchini wapo 40 tu, waliopata mafunzo, lakini katika utaalamu wa upasuaji hawafiki 10, idadi ambayo kitaifa ni ndogo sana.

Dk. Chapa anataja mikoa inayoongoza kuwa na fistula ni Rukwa na mikoa ya Kusini mwa nchi, pia anaeleza athari zake kuwa ndoa zimekuwa zinavunjika kila baada ya kuugua fistula.

**MGONJWA FISTULA**

Rehema Emmanuel, anayepata matibabu hospitalini CTBRT, ni mkazi na mzaliwa wa Bunda mkoani Mara, anayesema ndoa yake imevunjika baada ya kuugua fistula.

Rehema, mwenye elimu ya msingi, ni mzaliwa wa mwaka 1977, anayesema alifunga ndoa mwaka 1996 na kufanikiwa kupata mtoto 1998, ndipo akapata mtoto fistula, hali aliyoduimu nayo kwa miaka 20.

Anaongeza kuwa baada ya kuugua fistula, alianza kupata manyanyaso katika ndoa hadi kuachika na sasa mumewe ameoa mwanamke mwingine.

Anasema Aprili mwaka huu, alipata wasamaria waliomfikisha CCBRT kupata matibabu na sasa anaendelea vizuri akiwa na matumaini ya kupona .

Wito wake, ni kuwataka kinamama wanaokutwa na hali hiyo, wasiogope kujitokeza kuchuguzwa afya zao na anaongeza kuwa fistula inatibika na sasa anaendelea vizuri kiafya.



...jijini Dar es Salaam, wakifurahia jambo. Juu, wakiwa katika maadhimisho ya

MAZINGIRA

# Profesa: Mabadiliko tabia nchi yanauteketeza uvuvi




JEDWALI: JENIFER JULIUS.

**Na Jenifer Julius**

SEKTA ya uvuvi ina mchango mkubwa katika uchumi na maendeleo ya jamii, ikiwamo kuupatia mwili protini, kuongeza kipato, fedha za kigeni, ajira, kukuza utalii na uhakika wa chakula.

Ndoto za mafanikio hayo, yanaelezwa kulega kutokana na kupungua samaki baharini, kunakotokana na sababu mbalimbali za athari za tabianchi.

Ripoti ya Takwimu ya Hali ya Mazingira nchini ya mwaka 2017, inaeleza kuwa uzalishaji samaki umeshuka kutoka mita za ujazo tani 364,602 mwaka 2013 hadi mita za ujazo tani 308,772 kwa mwaka huo.

Mtaalamu wa sekta ya uvuvi, kutoka Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, Profesa Philip Bwathondi, anasema mvua zinapowahi kunyesha au kuchelewa, zinaathiri ikolojia ya samaki, hasa wanaotaga.

Vilevile anasema, joto linapozidi na kuchanganyika na hewa ya ukaa, huwa ina kawaida ya kuchelewesha au kuzuia kabisa uanguliwaji samaki, nayo inachangia samaki kupotea.

"Hali ikiendelea hivi mazalia ya samaki yatakwisha. Hivyo, kunahitajika kupandwe miti mingi na kupunguza matumizi ya kuni na ikienda pamoja na kupunguza uchafuzi wa mazingira," anashauri Profesa Phillip.

Ofisa Uvuvi Mfawidhi wa Mkoa wa Kagera, Gabriel Mageni, anakiri kupungua kwa kiwango cha samaki baharini kunakosababishwa na mengi anayoyataja ni pamoja na kuongezeka nguvu ya uvuvi na matumizi ya zana za uvuvi haramu.

Akizungumzia athari za mabadiliko ya tabia nchi, anasema inachangia kuongezeka joto tindikali kwenye maji.

Mageni anasema kuwa, mabadiliko ya tabia nchi yanasababisha kubadilika kwa kina cha maji kuongezeka.

Pia, inasababisha baadhi ya visiwa kupungua au kukauka mabwawa kunakosababishwa na kuwapo joto kali katika mazingira.

Lingine kuhusu mabadiliko ya mabadiliko ya tabia nchi, ni kwamba yanasababisha kuongezeka tope kwenye ziwa na bwawa, kutokana na mmomonyoko wa udongo kwenye kingo za maziwa, mabwawa na mito inayoingiza maji kwenye maeneo hayo.

"Matokeo ya hali hii ni kupungua kwa samaki nchini, pia kupotea kabisa kwa baadhi ya samaki,"anasema Gabriel.

Mtaalamu huyo anasema, athari za mabadiliko ya tabia nchi, zinawagusa moja kwa moja kwa kiasi kikubwa wavuvi, kwani mavuno yao yanashuka, ikilinganishwa na uwekezaji unaofanyika.

Kwa mujibu wa mtaalamu huyo, hivi sasa hali ya malighafi imeshuka kutoka kwa wawekezaji wakubwa, pamoja na mazingira kwa ujumla kuathirika, kutokana na kutegemeana kiumbe mmoja na kingine, hivyo mmoja anapotoweka basi mwingine anaathirika.

Gabriel anashauri elimu kuhusiana na athari za mabadiliko ya tabia nchi, inapaswa itolewe kwa jamii na kuhamasisha upandaji miti ili kupunguza kiwango cha joto na usafishaji hewa ukioko.

Kingine kinachotajwa ni kupunguza nguvu za uvuvi, kwa maana ya kuondoa uvuvi haramu na holela, kwani kunaelezwa kuwapo baadhi ya maeneo ya uvuvi yasiyodhibitiwa, kila mwenye nguvu anaingia na kuvua.

Vilevile, kunatajwa uwapo wa uhamasishaji unahusu ufugaji samaki kupunguza uvuaji wa samaki wa baharini.

Mvuvi anayetoka mkoani Kagera,Tuwfiq Sharif, ana mtazamo kinzani na mtalamu, akisemea hali ya samaki baharini inaridhisha, katika ulinganisha na miaka ya nyuma.

Tahadhari yake nui kwamba, iwapo juhudi hazitachukuliwa kupambana na mabadiliko hayo ya hali ya nchi, kuna hatari ya kupoteza samaki wengi.

"Hali ya samaki kwa sasa sio mbaya, wapo, wanapatikana na tunashukuru Mungu, tunapata samaki wa kutosha kuendesha maisha yetu," anasema huku akitoa angalizo,

"Lakini, njaa inatunyemelea wavuvi wa Kagera kama tusipopambana na mabadiliko ya tabia nchi."

**MVUVI/ MCHUUZI**

Mfanyabiashara mdogo wa samaki jijini Dar es Salaam, Hadija Hizza, anasema kuwa biashara ya samaki imekuwa ngumu kwa sasa, kutokana na samaki kuadimika.

Anasema, zamani alikuwa akinunua samaki wengi kwa ajili ya kukaanga na kuuza, lakini sasa analazimika kununua kidogo wa kutokana bei kupanda maradufu.

Mabadiliko ya tabianchi yamekuwa tishio duniani kwa mengi, ikiathiri maisha katika sekta mbalimbali.

Hivi sasa mataifa yameungana duniani kuhakikisha yanapambana na hali hiyo, kabla haijendelea kuleta athari zaidi.

Hatua mojawapo iliyochukuliwa, ni kujadili hatua zilizochukuliwa na nchi za Kiafrika, kujadili hali ya mabadiliko ya tabinchi yanayoendelea duniani, kikao kiichofanyika kwa jijini Accra, Ghana, mnamo miezi michache iliyopita.

Ndani na kikao hicho, baadhi ya makubaliano yaliyofikiwa ndani ya mkutano wa siku tano uliopewa dhana ya 'Wiki ya Mabadiliko ya Tabia Nchi' ililenga kuwekeza kwenye kilimo cha kijani, ambayo mtazamo wake ni uzalishaji mimea endelevu, ikiwemo mimea na misitu.

***Makala nyingine ya samaki kewsho***

# TGNP: hii ndio operesheni rasmi inayowabakisha mabinti shuleni

**INAENDELEA UK.17**

kwamba manispaa ziwe wazi kueleza ainisho la pesa za pedi zinazotolewa katika bajeti husika, kwani maana huja katika jila la pesa za afya, pasipo uainishi wa kiasi cha pedi cha kununuliwa.

Pia, Mwakilishi wa Ofisa Elimu wa Manispaa ya Kinondoni, Amina Simwami, anasema katika manispaa yake, kumetolewa asilimia 10 ya bajeti kwa ajili ya ununuzi wa pedi na katika mwaka wa fedha 2019/2020, ni Sh. milioni 35, wanazotenga kununua pedi katika Shule zote.

Amina anarejea nyuma zaidi, kwamba katika mwaka wa fedha 2017/2018, walijenga majengo 10 ya kujisitiri kwa shule za sekondari na msingi.

"Mwaka 2019/2020, Sh.milioni 160 watajenga majengo ambayo yatakuwa na vyumba kubadilishia," anasema Amina na anawaomba wadau husika, washiriki kuisaidia serikali na wasiiachie pekee katika jukumu hilo la kuwahudumia wasichana masomoni. Bepo Martine, Ofisa Mipango katika ansipaa ya Ilala, anasema wanatekeleza masuala ya pedi na katika mwaka wa fedha uliopo, wametenga fedha Sh. milioni 20 za kununua taulo za watoto wa kike.

Pia, anataja bajeti ya Sh. milioni 100 kimetengwa kwa ajili ya kujenga vyumba vya kujistiria, ikijumuisha shule tano za msingi na sekondari tano za sekondari zitaanza kunufaika na mpango huo.

Anaongeza malengo yao kila mwaka kujenga vyumba vya kujistilia na kuongeza bajeti ya pedi.

**KUTOKA HALMASHAURI**

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Morogoro, Frolence Mabebe anasema changamoto zipo katika uwiano wa matundu ya vyoo. Anaeleza matarajio ni ifikapo mwaka 2022, uwiano utakuwa sawa mkoani Morogoro katika shule zote, matarajio ni vyoo vitatengenezwa na kutakuwapo vyoo maalam kuhudumia wenye mahitaji maalum kama wagonjwa.

Anasema halmashauri itenge mafungu maalumu ya taulo na isipofanya hivyo kutatokea matatizo. Wanchoke Chechegela, ni Ofisa Maendeleo ya Jamii Kisarawe, anasema katika mwaka wa fedha ulioisha 2017/18, zilitengwa Sh. milioni 9.4, kupitia ya mlengo kijinsia.

Anasema, walipewa tuzo maalumu kwa kutenga bajeti ya kijinsia na TGNP Mtandao, walizonunua katoni 21 za pedi na walizisambaza kwa shule za msingi na sekondari.

Anaongeza kwamba, katika mwaka wa fedha ulioisha, kulikuwapo bajeti ya Sh. milioni mbili, kwa ajili ya taulo za kike.

"Siku ya maadhimisho ya siku ya mtoto mwaka jana, katoni 400 za pedi ziligawiwa kwa shule zote za sekondari," anasema.

Anaongeza katika mwaka 2019/2020, wanatarajia kutenga asilimia 40 ya bajeti ya afya kununua pedi, hatua itakayoendana na utoaji elimu husika kwa wasichana wavulana jumla yao 5,248.

Chechegela anataja malengo mengine ni kuongeza matundu ya vyoo na mahali pa faragha ya kujisitiri.

Ofisa Maendeleo ya Jamii huyo, anasema katika kuhakikisha watoto wanakuwa na mahudhurio mazuri shuleni, kutakuwapo kikundi cha kuisaidia kutengeneza taulo za kike za asili, lengo ni kuondoa utoro kwa mabinti wanafunzi na papo hapo wa wapende shule

HABARI MBEYA

# Wasiojulikana wamnyonga dereva bodaboda hadi kufa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATU wasiojulikana wamemuua kwa kumnyonga dereva wa bodaboda, mkazi wa Sinjili, wilayani Chunya, Omary Kandonga (25) na kutokomea na pikipiki hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake, Kaimu Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Sebastian Mbuta, alisema tukio hilo lilitokea Juni 3, mwaka huu na inadaiwa kijana huyo alikodiwa na watu wasiojulikana wakitaka awapeleke sehemu.

Alisema baada ya kukodiwa kijana huyo hakuonekana tena mpaka siku iliyofuata asubuhi mwili wake ulipokutwa pembezoni mwa uwanja wa mpira wa Sinjili ukiwa umenyongwa kwa kutumia kamba ya manila.

"Pikipiki aliyokuwa anaendesha kijana huyo ni aina ya T-Better yenye namba za usajili MC. 274 CDM yenye rangi nyekundu mali ya Mussa Jeremia (22), ambayo watu hao waliondoka nayo," alisema Kamanda Mbuta.

Alisema Jeshi la Polisi linaendelea kufanya upelelezi wa tukio hilo ikiwa ni pamoja na msako wa kuwabaini watu waliotenda unyama huo na kuwachukulia hatua za kisheria.

Aliwataka madereva bodaboda kuwa makini katika shughuli zao ikiwa ni pamoja na kuepuka kuwabeba watu ambao hawawafahamu hasa nyakati za usiku.

Alisema Jeshi hilo litaendelea kutoa elimu kwa madereva hao ili wawe makini na kutoa taarifa kwenye vyombo vya usalama wanapowaona watu ambao wanawashukia ili hatua zichukuliwe.

# Chadema yajisafisha kwa kufuta wanachama

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) Wilaya ya Mbeya Mjini, kimeanza kujisafisha kwa kufuta uanachama wenyeviti wa mitaa ambao wanadaiwa kukisaliti chama hicho kwa kushirikiana na Chama cha Mapinduzi (CCM).

Uongozi wa chama hicho ulitoa taarifa ya kuwatimua wenyeviti wa mitaa mitatu katika kata tofauti jana na kueleza kuwa kinachofanyika ni maandalizi ya uchaguzi wa serikali za mitaa ambao unatarajiwa kufanyika mwezi Novemba, mwaka huu.

Mwenyekiti wa Chadema Wilaya ya Mbeya Mjini, Obadia Mwaipalu, alisema mmoja wa wenyeviti waliofukuzwa uanachama ni Mwenyekiti wa Mtaa wa Ilolo katika Kata ya Sinde, Ng'ambi Kulambi ambaye ndiye alikuwa wa mwisho kutimuliwa.

Mwaipalu alisema viongozi wengine waliotimuliwa ndani ya chama hicho ni wa kutoka katika Kata za Ilemi na Mwakibete ambao hakuwataja majina wala mitaa wanayotoka.

Alisema viongozi hao walikuwa wanakiuka misingi ya uongozi wa chama hicho ikiwa ni pamoja na kutotunza siri za chama hicho kwa kuzisambaza nje ya chama kwa wasiokuwa wanachama wa chama hicho wakiwamo CCM.

"Walikuwa ni wajumbe kwenye vikao vyetu vya chama na hivyo tulikuwa hatuwezi kuwatenga, walikuwa wanachukua vitu tunavyojadili kwenye chama na kuvipeleka upande wa pili wa wapinzani wetu (CCM), sasa tumeona ni bora watupishe," alisema Mwaipalu.

Alisisitiza kuwa chama hicho kitaendelea kuwatimua viongozi wenye tabia za aina hiyo ili kuhakikisha wanabaki na wale wanaoaminika ndani ya chama na kwa wananchi ili kukiwezesha kuendelea kupata ushindi.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Hamasa wa Chadema Kanda ya Nyasa, John Mwambigija 'Mzee wa upako' alisema mbali na kukisaliti chama hicho pia walikuwa hawashiriki kwenye kampeni ya Chadema ni Msingi ambayo inaendelea nchi nzima.

Alisema kampeni hiyo ni maandalizi ya chama hicho kushiriki na kupata ushindi kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika mwezi Novemba mwaka huu na kwamba kutoshiriki kwao kunakifanya chama hicho kukosa imani nao.

Alisema jambo la kuondolewa kwa viongozi hao limepokelewa kama inavyopokelewa kwa wale wanaokihama kwa kutimiza haki zao za kikatiba.

"Tunapoelekea kwenye uchaguzi huwa tuna kaulimbiu moja kwamba mtu kama hakufanya vizuri tunaangalia, tumtose yeye tukiokoe chama au kumlinda yeye pamoja na chama, sasa tulipobaini hawashiriki kazi za chama ikiwamo Chadema ni msingi tunaona hawatufai," alisema Mwambigija.

Alisisitiza kuwa Mwenyekiti wa Mtaa wa Ilolo, Ng'ambi, alikuwa anakwepa vikao vya chama na kushiriki vikao vya CCM hasa nyakati za usiku na kwamba baadhi ya shughuli alikuwa anashirikiana na wajumbe wa CCM.

Mwambigija alisema kinachofanyika ni mbinu za CCM kuwarubuni baadhi ya viongozi wa Chadema ili kukidhoofisha chama hicho kikuu cha upinzani, lakini akaeleza kuwa bado chama chake kitashinda kwenye chaguzi zijazo.



Wananchi wakisaidia kulikwamua gari la serikali lililokwama kwenye matope kufuatia mvua zinazoendelea kunyesha wilayani Kyela, Mkoa wa Mbeya juzi na kusababisha baadhi ya barabara kutopitika. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# TBS yaelimisha wazalishaji ubora wa bidhaa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SHIRIKA la Viwango nchini (TBS), limeanza kutoa elimu ya ubora wa bidhaa kwa wazalishaji na wenye Viwanda vidogo na vikubwa ili kuwezesha bidhaa zao kukidhi matakwa ya kisheria na kuuzika kwenye soko la ndani na nje ya nchi.

Akizungumza jijini Mbeya wakati wa utoaji wa mafunzo hayo Ofisa Uhakiki Ubora wa TBS kutoka makao Makuu jijini Dar es Salaam, Stella Mrosso, alisema lengo la elimu hiyo ni kuhakikisha bidhaa zinazalishwa katika ubora unaotakiwa.

Alisema mafunzo hayo yanatolewa kwa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ambayo ni Njombe, Iringa, Mbeya Songwe, na Rukwa na kuwa wamepewa elimu na TBS ya mifumo ya uongozi katika masuala ya ubora na mfumo ili waweze kukidhi viwango vya ubora vya kimataifa.

Alisema hadi sasa wazalishaji zaidi ya 300 kutoka mikoa sita nchini wamepatiwa mafunzo hayo ambayo yanalenga kuhakikisha wanazalisha bidhaa bora zitakazokuwa zinaendana na ubora unaotakiwa ndani ya nchi na nje ya nchi ili kupata masoko.

"Baadhi ya wazalishaji wetu wamekuwa wakizalisha bidhaa ambazo zinakidhi viwango ambavyo vinatakiwa hivyo kutokana na elimu waliyoipata itawasaidia waweze kuongeza bidii na wale ambao bidhaa zao ni hafifu watayatumia mafunzo haya kuboresha," alisema Stella.

Kaimu Meneja wa TBS Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Mhandisi Yekonia Sanga, alisema wanataka wazalishaji waweze kuzalisha kwa malengo ya kuwa washindani na masoko ya nje ili kupata manufaa.

Alisema mafunzo hayo ni ya kuwahamasisha wazalishaji kuzitambua bidhaa zao kuwa zinafaa na zinatakiwa kuendelea kuzalishwa ili kuhakikisha wanakuwa washindani.

Aidha, baadhi ya wafanyabiashara wamesema mafunzo hayo yana tija kubwa kwa kuwa watakuwa wakitambuliwa kwa bidhaa wanazozalisha.

Gerge Msyani kutoka kiwanda cha Jambo mkoani Songwe ambacho kinazalisha bidhaa ya chokaa, alisema elimu hiyo itawasaidia kuzalisha bidhaa zitakazokuwa zikishindana na zile zinazotoka nje ya nchi.

Alisema ilikuweza kukua kiuchumi kupitia bidhaa wanazozizalisha ni lazima kuwapo na ubora unaotakiwa ili kupata masoko ya uhakika ndani ya nchi na nje ya nchi kwa kutumia rasilimali za ndani.





## Dodoma watenga vituo wagonjwa wa dengue

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

MKOA wa Dodoma umetenga vituo viwili kwa ajili ya kuwahudumia watu watakaokumbwa na ugonjwa wa homa ya dengue.

Akizungumza jana na Nipashe jijini hapa, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. James Kiologwe, alisema mkoa huo ambao ni makao makuu ya nchi wamechukua tahadhari mbalimbali za kukabiliana na ugonjwa huo na magonjwa mengine ya mlipuko.

"Kama mnavyojua Dodoma ni makao makuu na muingiliano wa watu kutoka mikoani kufika hapa ni mkubwa, tumechukua tahadhari za kuhakikisha wanazuia magonjwa yanayoweza kuzuilika,"alisema.

Mganga huyo alisema kwa sasa wametenga vituo viwili vya kuwapokea wagonjwa wa homa ya dengue ambavyo ni Hospitali ya Rufani ya Dodoma na Hospitali ya Agakhan.

Aidha, alisema wahudumu wa afya wa vituo mbalimbali vya afya wameshawezeshwa mafunzo ya namna ya kuwatambua na kuwasaidia wagonjwa hao kama wataonekana katika maeneo yao.

Dk. Kiologwe aliitaja mikakati mingine kuwa mkoa ulifanya zoezi kuua mazalia yote ya mbu pamoja na kufukia baadhi ya madimbwi ambayo ndio chanzo cha mzalia hayo.

"Tunaendelea pia kutoa elimu ya afya kwa wananchi ili kuchukua tahadhari ya magonjwa haya pamoja na kuwatambua wagonjwa wakijitokeza huko wanapoishi,"alisema.

Kuhusu ugonjwa wa kipindupindu, Dk. Kiologwe, alisema maeneo yaliyokuwa yanakumbwa na kipindupindu yaliwekewa mikakati ya kutokomeza na kuzuia ugonjwa huo.

Alisema sababu kubwa ilikuwa ni ukosefu wa maji safi kwa matumizi ya wananchi, lakini serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali walichimba visima vya maji. Aliitaja mikakati mengine ya kuwa maeneo yaliyokuwa hayana vyoo waliwezeshwa elimu na vijiji 331 ambavyo vilishambuliwa na magonjwa ya mlipuko kwa sasa hakuna vinyesi vinavyozagaa kutokana na kujenga vyoo bora.

"Dodoma tunamshukuru Mungu, mikakati hiyo ilisaidia tangu mwaka jana hadi mwaka huu hakuna mgonjwa wa kipindupindu aliyeripotiwa , kwa sasa mvua zimeisha tutaendelea kuhamasisha jamii kujikinga na kujihami na magonjwa yanayoweza kuzuilika,"alisema.

# Jamii yaonywa kuwafungia watoto mguu kifundo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZAZI na walezi nchini wametakiwa kuacha kuwafungia nyumbani watoto wenye ulemavu wa mguu kifundo ili waweze kupata haki zao za msingi ikiwamo elimu.

Wito huo ulitolewa na Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. James Kiologwe, katika maadhimisho ya siku ya mtoto mwenye matatizo ya mguu kifundo, jijini hapa.

Alisema zaidi ya watoto 2,500 wamegundulika kuwa na tatizo la ulemavu wa mguu kifundo hapa nchini.

Dk. Kiologwe alisema jamii inatakiwa kubadilika na kuacha tabia ya kuwaficha na kuwanyanyapaa watoto hao kwa kuwa wana haki kama watoto wengine.

Pia alipongeza muungano wa wadau wanaojihusisha na matibabu ya mguu kifundo (TCCO), waliodhamini maadhimisho hayo ambao wameshahudumia watu zaidi ya 4,000, ambao wamefanyiwa marekebisho ya ulemavu huo.

Alisema kuwa TCCO wana jumla ya matawi 35 kote nchini na kuiomba taasisi hiyo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kuanzisha kliniki kila mkoa na wilaya kutokana na kila mwaka watoto 1,000 huzaliwa na tatizo hilo.

"Kuna tatizo kubwa sana kwa watoto wenye ulemavu wa mguu kifundo na wengine wamekuwa wakishindwa kupata matibabu kwasababu ya kukosa uwezo, kuzinduliwa kwa kliniki hii kutasaidia kwa kiasi kikubwa kuepuka gharama za kwenda kupata matibabu nje ya Jiji la Dodoma," alisema.

Alifafanua kuwa matibabu katika kliniki hiyo yatakuwa yanafanyika kila Alhamisi na kwa watoto wote chini ya umri wa miaka mitano watakuwa wakipata matibabu bure.

Mwenyekiti wa TCCO, Dk. Robert Mhina, alisema bado kuna changamoto miongoni mwa jamii kuhusu ugonjwa huo na wamekuwa wakihusisha na imani za kishirikina.

Alisema wataendelea kutoa elimu kwa jamii ili iache kuwanyanyapaa watoto wenye matatizo hayo.

"Natoa rai yangu kwa wazazi, walezi pamoja na wananchi kiujumla waache kuwafungia ikiwamo kuwaficha watoto wenye ulemavu kwa kuwa tatizo hilo linapona hivyo jamii iache tabia ya kuwanyanyapaa na kuhusisha ugonjwa huo na imani za kishirikina," alisema Dk. Mhina



Shekhe Mohamed Thabiti (kulia), akitakiana heri ya Eid El Fitri na Mzee Ismail Dawood, baada ya kumalizika kwa Swala ya Eid iliyoswaliwa viwanja vya Jamhuri, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Gwajima ahimiza ulinzi, usalama wa watoto

**Na Mwandishi wetu,** DODOMA

NAIBU Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), anayeshughulikia Afya, Dk. Doroth Gwajima, ameitaka jamii kuwa makini kuimarisha ulinzi na usalama wa watoto ili waweze kuwa na malezi bora.

Kauli hiyo aliitoa jana alipotembelea kituo cha kulelea watoto cha nyumba ya matumaini jijini hapa na kutoa misaada mbalimbali kwa ajili ya Sikukuu ya Eid.

Alisema ni wajibu wa kila mzazi kutekeleza jukumu lake la msingi la kuhakikisha mtoto yuko salama hasa wanaposherehekea sikukuku.

"Mzazi anatakiwa kujenga mazingira rafiki na yenye kumjenga kimwili na kiakili zaidi bila kupata adha ya aina yoyote," alisema.

Alipongeza kituo hicho kwa jukumu kubwa walilo nalo la kuhakikisha watoto wanapata malezi bora na kuwaasa kuzidisha upendo na mshikamano miongoni mwao.

"Tunatekeleza hili kwakuwa ni wajibu wetu kuwalea watoto, hata sisi leo tumekuwa watu wazima kwa sababu ya juhudi za wakubwa zetu, nanyi watoto mtakuwa wakubwa kama sisi na mtakuja kuwa viongozi wa taifa hili katika nyanja mbalimbali, hivyo pendaneni na kuishi kwa amani na msome kwa bidii," aliwaasa watoto wa kituo hicho.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Msaidizi anayeshughulikia masuala ya ustawi wa Jamii wa Ofisi hiyo, Rashed Maftah, alisema Tamisemi ni jukumu lao la msingi kuhakikisha watoto walio katika mazingira magumu wanapata vituo vya kuwalea katika misingi bora na usalama wao unaimarika.

"Dini iliyosafi ni yenye kuwajali Yatima na wenye uhitaji kwa kuunganika na kushiriki nao katika mahitaji yao ya msingi, aidha sheria ya mtoto namba 21 ya mwaka 2009 kanuni ya 12 inahimiza suala la kulelea watoto," alisema Maftah.

Akitoa shukrani kwa niaba ya walezi wa kituo hicho, mmoja ya walezi, Sister Urea, alisema kituo hicho kina jumla ya watoto 63 na kimekuwa kikifanya kazi zake tangu mwaka 1995 kwa kuhudumia watoto wanaopatikana katika mazingira magumu na ukatili wa kijinsia kutoka mikoa ya Dodoma na Singida.

Alishukuru kwa misaada hiyo na kuwaomba kuendelea kuwakumbuka watoto hao ili nao wajione ni sehemu ya jamii.

"Tunawashukuru sana kuja kutuona na kutupatia misaada, lakini msiishie kuja kuleta misaada tu, hata kama hamna kitu msisite kuja kutusalimia na kuongea na sisi, tunaomba Mungu awazidishie pale mlipotoa na siku nyingine tena mtukumbuke," alisema.



# Raza aibua jambo mambo ya nje

**Na Rahma Suleima, ZANZIBAR**

MWAKILISHI wa Uzini, Mohamed Raza, amesema wakati umefika mabalozi wa Tanzania kuandikiwa barua maalum ya kuwafahamisha kuwa Tanzania kuna serikali ya Zanzibar na ile ya Muungano.

Raza ambaye pia ni mfanyabiashara maarufu Zanzibar, alisema hayo juzi alipokuwa akichangia makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Biashara na Viwanda katika mkutano wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

Alisema hatua hiyo itasaidia kuondoa vikwazo vya biashara wanavyopata Wazanzibari wanapotaka kununua bidhaa nje ya nchi kutokana na mawakala wa biashara kutambuliwa kuwa wako Tanzania, hivyo kukwama kununua bidhaa moja kwa moja bila kupitia kwao.

"Nimwombe mheshimiwa Waziri atoe barua kwa mabalozi wetu kuwaambia kwamba hapa tuna serikali mbili ya Zanzibar na Tanzania," alisema Raza.

Alisema bidhaa zinazotoka nje ya nchi kuingia Zanzibar zieleweke kuwa ni za Zanzibar na hakuna sababu ya kupitia kwa mawakala wa biashara wa Tanzania kwa sababu masuala ya biashara si ya Muungano.

Raza alisema kimsingi Tanzania imepatikana kwa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar lakini Zanzibar imekuwa inakosa haki zake za biashara na kutaka Waziri wa Biashara na viwanda Zanzibar kuandika barua ya kuwaarifu mabalozi wa Tanzania kuwa wafanyabiashara Zanzibar wako huru kufanya biashara bila vikwazo.

"Wanakuwa hawafahamu lugha tunasema nchi mbili Zanzibar, Tanganyika imepatikana Tanzania. Mheshimiwa Spika, funika kombe mwanaharamu apite. Kule Dodoma Serikali ya Tanganyika imejificha ndani ya Muungano, huo ndio ukweli hapa kuna Waziri wa Biashara anatoa bajeti yake mwisho chumbe na Dodoma anatoa mwisho chumbe lakini lazima Wazanzibari tupewe haki yetu ya biashara," alisema Raza.

Hata hivyo alisema kutokana na kuridhiana kwa pande mbili za muungano wa Tanganyika na Zanzibar acha serikali ya Tanganyika iendelee kufichwa katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Aidha, Raza alitaka kufahamu hatua gani za kisheria zimechukuliwa ikiwamo kufunguliwa mashitaka watu waliokamatwa na magendo ya karafuu za Zanzibar mkoani Tanga baada ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Mohamed Abod, kuthibitisha karafuu zilikuwa za Zanzibar.

Alisema kimsingi Tanzania Bara hakuna karafuu kama ilivyo kwa Zanzibar ambako hakuna madini ya dhahabu na watuhumiwa wa karafuu walipaswa kufunguliwa mashitaka Zanzibar kama wanavyoshtakiwa watu wanaokamatwa na madini Zanzibar na kushitakiwa Tanzania Bara.

Akizungumzia viwanda vya mifuko Raza alisema SMZ lazima iweke sheria ya kodi ya kulinda viwanda vya ndani ili kuendeleza sekta ya viwanda katika kuelekea Zanzibar ya uchumi wa Viwanda.



Waumini wa Dini ya Kiislam Zanzibar, wakifuatilia hutuba ya sala ya Eid Fitr katika viwanja vya Maisara Suleiman, mjini Unguja jana, iliyosomwa na Sheikh Khamis Gharib Khamis (hayupo pichani). **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Ataka wanawake wahamasishwe kuwa viongozi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MENEJA Sera na Utetezi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, Hawra Shamte, amewaomba viongozi wa dini, vyama vya siasa na jamii kuhamasisha wanawake kugombea nafasi za uongozi katika majimbo badala ya kusubiri nafasi za kuteuliwa.

Akizungumza katika kikao cha majadiliano kilichowashirikisha viongozi wa makundi hayo juzi, Shamte alisema jamii inapaswa kufahamu mwanamke anaweza kuwa kiongozi mzuri endapo atapewa nafasi ya kugombea katika ngazi ya ubunge, uwakilishi na udiwani.

Shamte alisema jamii yenyewe, hususani wanawake, wanapaswa kuwakubali wanawake wenzao pale wanapojitokeza kugombea nafasi ya uongozi na kuacha tabia ya kuwakatisha tamaa kwa kuwa anayegombea ni mwanamke.

"Wanawake wanatakiwa wasaidiane kwa kumuunga mkono mwanamke mwenzake pale anapogombea uongozi katika jimbo badala ya kusema mabaya yake ya nyuma pale tu anapotangaza nia ya kugombea," alisema.

Katika kuhakikisha wanawake wanahamasika kugombea uongozi, alisema Tamwa imeweka kamati za wanaume ambazo zimewashirikisha watu mbalimbali kama viongozi wa dini, wanasiasa kwa Unguja na Pemba ili kuhamasisha jamii kuona umuhimu wa kuwachgua wanawake katika uongozi.

Akiwasilisha mwongozo wa ushirikishaji wa wanawake katika uongozi, mwanaharakati Asha Aboud, alisema wanawake wanaweza kuwa viongozi na wakaleta mabadiliko makubwa katika jamii.

"Maendeleo yanayoweza kuletwa na mwanamke yanatokana na imani, huruma na kuwa msuluhishi mkuu katika ngazi ya familia, hivyo mwanamke akipewa nafasi ya kugombea anaweza kufanya vizuri na kuleta mafanikio," alisema.

Pia alisema wanawake wakiwa viongozi, mara nyingi husisitiza maisha bora katika familia na hata kuchangia shughuli za uchumi kutokana na kuwa wazalishaji wazuri kupitia ujasirimali wanaofanya pamoja na hata kuwa mstari wa mbele katika kupinga vikali vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia .

"Tunaona katika Baraza la Wawakilishi wanawake wanavyochangia kwa hisia vitendo vya udhalilishaji hususan vya ubakaji na ulawiti wa watoto. Hii inatokana na kwamba inawauma kuliko hata inavyowauma wanaume. Kwa hiyo mwanamke akipewa nafasi ya kugombea katika jimbo atafanya vizuri kwa sababu ni mtu anayependa maendeleo, "alisema.

Alisema jamii yenyewe iwachague wanawake wenye heshima na wanaojua kuzungumza vizuri na wenye kujiamini ili kuleta ushawishi ili wanawake wajitokeze katika kugombea.

# DK Shein amwagiwa sifa kumteua Balozi Amina

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, hakufanya makosa kumteua Balozi Amina Salum Ali kuwa Waziri wa Biashara na Viwanda kutokana na uzoefu wake katika diplomasia ya kiuchumi na biashara, imeelezwa .

Hayo yalielezwa juzi na Waziri asiye na Wizara, Maalum Said Soud, alipokuwa akichangia makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Biashara na Viwanda kwa mwaka wa fedha wa 2019/20.

"Zanzibar imepinga hatua kubwa sana ya maendeleo. Napenda kumpongeza sana Rais kwa kumteua na kumpa nafasi ya Waziri wa Biashara na Viwanda mwanamke mwenye ujasiri wa hali ya juu na mwenye mvuto wa kimataifa, mwanamke ambaye aliyefika UN (Umoja wa Mataifa) na kusimamia mambo ya kimataifa," alisema Waziri Soud.

Alisema maendeleo ya sekta ya viwanda na biashara yameanza kuonekana tangu kupewa dhamana ya kuongoza sekta ya biashara na viwanda Balozi Amina, ikiwamo utekelezaji wa mpango wa Zanzibar wa kuwa na uchumi wa viwanda.

Waziri Soud alisema mabadiliko ya maendeleo ya viwanda yameanza kuonekana ikiwamo kufufuliwa kwa kiwanda cha makonyo kwa kushirikiana na wawekezaji kutoka China na kuongeza uzalishaji wa mafuta ya makonyo na mikaratusi.

Alisema iwapo mchakato wa kuanzishwa viwanda vya kuchakata mazao na kusarifu utatekelezwa kama ulivyopangwa katika mwaka wa fedha, mpango wa Zanzibar wa kuwa na uchumi wa viwanda utafikiwa.

# Wataalamu kuandaliwa kufundisha Kiswahili nje

**Na Enock Charles.**

BARAZA la Kiswahili la Taifa (Bakita) limetaja mikakati yake ya kuandaa wasomi wa kufundisha somo la lugha Kiswahili nje ya nchi ikiwamo kuandaa kanzidata ya wanataaluma wote wa Kiswahili nchini na kuwapa mafunzo maalum.

Akizungumza na gazeti hili juzi msemaji wa Baraza hilo, Consolata Mushi, alisema kanzidata hiyo itasaidia kuwatambua wanataalumu wote wenye uwezo wa kufanya kazi hiyo nje ya nchi ili kuwaweka tayari kwa fursa hizo.

"Hapo awali zilikuwa zikija fursa moja moja sio kwa wingi kama hizi, hivyo sasa tunaandaa kanzidata ya kuwatambua wanataaluma wote wa Kiswahili ili iwe rahisi zinapokuja fursa pawapo na utaratibu mzuri," Consolata alisema.

Akizungumzia kuhusu kozi fupi ya wiki moja inayotolewa na Baraza hilo licha ya kuwa wanaopatiwa kozi hiyo kuwa tayari ni wasomi wa lugha hiyo, Mkurugenzi wa Taasisi ya Taaluma za Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dk. Ernesta Simon Mosha, alisema kozi hiyo ni muhimu kwa kuwa huwapa fursa ya kufanya maandalizi ya mwisho kabla ya kwenda kufundisha lugha hiyo nje ya nchi. "Unaweza kuwa umesoma Kiswahili na unakielewa vizuri tu, lakini usiweze kufundisha kwa hiyo hiyo kozi fupi ni ya muhimu sana,". Dkt Mosha alisema.

Mmoja ya wanafunzi waliopata mafunzo kutoka Bakita, Tuladega Tweve, alieleza kuridhishwa na mafunzo hayo kwa kile alichokielezea kuwa ni kupata ufanisi zaidi pamoja na kutambua malengo maalum ya wageni wanaohitaji mafunzo hayo.



Mafundi wakiandaa sehemu inayotenganisha barabara inayoelekea kituo cha daladala cha Mawasiliano, jijini Dar es Salaam jana. Kabla ya kujengwa kwa kiwango cha lami, ilikuwa na mashimo mengi yaliyosababisha usumbufu kwa madereva wa magari. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Kigwangalla aishauri TTB

**Na Mwandishi Wetu**

Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamisi Kigwangalla, ameitaka Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) iwekeze zaidi katika matumizi ya njia za kisasa za mawasiliano na mbinu rahisi zenye gharama nafuu kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo nchini.

Kigwangalla aliyasema hayo jijini Dodoma wakati akizindua rasmi Bodi hiyo iliyoongezewa miaka 3 na Rais John Magufuli Aprili 23, mwaka huu.

Alimshukuru Rais Magufuli kwa kuiongezea kipindi kingine cha miaka mitatu na kuitaka bodi hiyo iendelee kubuni na kuongeza mbinu mpya za kutangaza utalii zitakazoleta tija na matokeo ya haraka.

Aliwataka wajumbe wa Bodi hiyo kufanya kazi pamoja na kushirikiana na taasisi nyingine za Wizara ili kuongezea idadi ya watalii wanaoitembelea Tanzania akiweka msisitizo katika matumizi ya mifumo ya kisasa ya mawasiliano ili kupanua wigo wa kutangaza vivutio vya utalii kuliko ilivyo sasa.

"Bodi ya utalii mnapaswa kuona fursa zilizopo na kutimiza majukumu mliyopewa kwa tija na ufanisi zaidi, namna pekee ya kufikia malengo hayo ni lazima mtumie teknolojia na mbinu rahisi za mawasiliano zenye gharama nafuu kutimiza majukumu yaleyale ya kutangaza vivutio vya utalii kisasa zaidi," alisisitiza.

Alisema kupitia kaulimbiu hiyo watalii wengi wanaoitembelea Tanzania wataendelea kukumbuka mambo mazuri na vivutio vizuri walivyoviona na kuendelea kuichagua Tanzania kuwa mahali pao pa kufanyia utalii.

Aidha, alitoa wito kwa Bodi hiyo kuendelea kuweka mazingira na kuongeza soko la bidhaa za utalii za Tanzania nje ya nchi kupitia maonesho ya kimataifa.

Kadhalika, aliiitaka Bodi hiyo kuweka mkakati mahususi ya kukamata masoko mapya ya watalii kutoka nje ya nchi kutoka nchi za Marekani, Hispania, Urusi na nchi za Falme za Kiarabu zikiwamo za Dubai na Oman ambazo watu wake wakiwamo wasomi, wafanyabiashara, wanamichezo na watu maarufu wanapenda kwenda mapumziko ya muda mrefu na kutumia fedha nyingi kwa shughuli za utalii.

# Wasomi wa kilimo sasa wajengewa fursa ajira

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WAHITIMU wa vyuo vikuu waliohitimu masomo ya shahada ya kilimo na kukosa nafasi za kazi, wamepatiwa mbinu na mafunzo ya ujasirimali kuweza kutumia elimu yao kujiajiri kupitia kilimo.

Kupitia mpango wa mradi wa Kituo Atamizi cha kilimo Biashara kilichopo Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) na Taasisi Binafsi ya kusaidia Sekta ya Kilimo (PASS) kwa ufadhili wa Serikali ya Denmark, wameanza kuwasaidia wahitimu 20 ili wakimaliza kwenda kujiajiri.

Akizungumza mbele ya Balozi wa Dernamak nchini ambaye ndio wanaosaidia mradi huo, Meneja wa mradi huo, Richard Bruno, alisema kupitia mpango huo wahitimu hao wanafundishwa kilimo biashara cha nyanya na wameweza kujipatia kiasi cha shilingi milioni 15 kutokana na mavuno ndani ya miezi minne.

Kwa Upande wake Balozi wa Denmark nchini, Einar Jensen, ambayo inafadhili mradi huo, alitembelea kujionea mradi huo na kusema lengo lao ni kuhakikisha wahitimu wa masomo ya kilimo wanatumia taaluma yao ili kuongeza tija katika uzalishaji wa chakula nchini.

Alisema ili kuongeza uzalishaji wa kilimo nchini, wameamua kuwasaidia wahitimu wa kilimo ili kutumia taaluma walizozipata kusaidia kulima kilimo cha kisasa kwa kuanzia na kilimo cha nyanya ambacho kwa sasa kina soko kubwa.

Nae Mkurugenzi Mkuu wa PASS, Nicomed Bahay ,alisema wameamua kuwasaidia wahitimu wa vyuo vya kilimo ambao wanakosa ajira za Serikali ili kutumia taaluma zao kwa maendeleo ya kilimo nchini kusaidia utekelezaji wa mpango wa serikali wa uchumi wa viwanda.

Alisema kupitia mradi huo baada ya kukamilika mafunzo hayo ya kilimo kwa wahitimu hao PASS, itawezesha kuwadhamini kupata mikopo kwenye Taasisi za fedha ili kuanzisha miradi ya kilimo kuongeza ajira.

Mwenyekiti wa Bodi ya PASS hiyo, Prof. Andrew Temu, aliiomba Serikali kusaidia wahitimu hao wanapomaliza mafunzo hayo kupewa maeneo kwa ajili ya uzalishaji kupitia sekta ya kilimo.

Mmoja wa wahitimu wa shahada ya kwanza ya kilimo biashara na uchumi wa SUA, Zephania Philimon, alisema kuwa kupitia mafunzo hayo sasa wamejua jinsi ya kulima kilimo biashara na jinsi ya kupata masoko.

Mhitimu mwingine wa SUA, Naomi Mkumbo, kwa kupitia kilimo cha mafunzo ya nyanya sasa wanazalisha kilo 6,000 kwa wiki na kuuza kwa wananchi mbalimbali mkoani hapa.

HABARI KIMATAIFA

# Baraza la kijeshi lasema liko tayari kwa mazungumzo

**KHARTOUM, Sudan**

MKUU wa Baraza la Kijeshi la Sudan, Luteni Jenerali Abdel Fattah al- Burhan, amesema baraza hilo liko tayari kwa majadiliano kuhusu mustakabali wa taifa hilo, siku moja baada ya kuyasimamisha.

Amesema wako tayari kuzungumza kwa maslahi ya kitaifa na mapinduzi.

Luteni Jenerali Abdel Fattah al-Burhan ametoa matamshi hayo katika ujumbe wa sherehe ya Eid al- Fatr, siku moja baada ya kutangaza kwamba baraza la mpito (MTC) limefuta makubaliano yote na muungano wa waandamanaji na makundi ya upinzani, na badala yake walikuwa wanakwenda kwenye uchaguzi wa taifa katika kipindi cha miezi tisa.

"Sisi katika Baraza la Kijeshi tunafungua mikono yetu kwa majadiliano bila vikwazo vyovyote zaidi ya maslahi ya kitaifa ya kuendelea kujenga mamlaka halali inayoakisi malengo ya mapinduzi ya Sudan kwa kila njia," alisema Luteni Jenerali Burhan katika hotuba kupitia televisheni ya taifa.

Kamati kuu ya madaktari wa Sudan, imesema idadi ya waliouawa katika ukandamizaji wa kijeshi imepanda na kufikia watu 60, na kwamba zaidi ya 300 walijeruhiwa.

Imesema imekuwa vigumu kubainisha hasa idadi ya waliojeruhiwa kwa sababu baraza la kijeshi limezima mawasiliano ya intaneti katika maeneo mengi ya nchi.

Idadi ya awali waliouawa ilikuwa 40, lakini kamati ya madaktari inasema vikosi vya usalama viliuwa watu wasiopungua 10 katika mji mkuu Khartoum na mji wake pacha wa Omdurman.

Hii ni baada ya watu wengine 10 kuuawa wakiwamo watano katika jimbo la White Nile, watatu mjini Omdurman na wawili katika kiunga cha Bahri mjini Khartoum.

DW

# Amshona mwanawe mdomo kisa hajafanya vizuri darasani

**NAIROBI, Kenya**

KATIKA hali ya kushangaza na isiyo tarajiwa na wengi, Mwanamke mkazi wa Maai Mahui mjini Naivasha Jimbo la Nakuru nchini Kenya amemshona mdomo mtoto wake wa kiume anayesoma darasa la tano baada ya kushuka kimasomo.

Kutokea kwa tukio hilo kumewashangaza watu wengi na kuwaacha midomo wazi katika Jimbo hilo, ambalo lilitokea jumamosi.

Mkazi mmoja katika eneo hilo alisema mwanamke huyo anayefanya kazi kwenye saluni ya urembo, alichukizwa na maendeleo ya mtoto wake shuleni yaliyokuwa yameshuka.

Alisema katika kumuadhibu, Mama huyo alimshona mdomo mtoto wake kwa kutumia sindano kabla ya majirani kuingilia kati.

Kamishna msaidizi wa Kaunti hiyo, Julius Nyaga, ameiambia Daily Nation kuwa taarifa za tukio hilo zimemfikia na wameanza kulifanyia kazi.

Tukio hilo limeelezwa kuwa ni la kikatili na Polisi wanamsaka mshukiwa.

"Polisi wanamtafuta Mama wa mtoto baada ya uongozi wa shule kuripoti kwenye mamlaka," Alisema Nyaga.

Nyanga aliwataka wazazi kuacha kuwafanyia vitendo vya kikatili watoto wao, akiwaasa kuwachukulia hatua kali za kisheria.

Alisema ni vyema wazazi kutafuta msaada wa kitaalamu kuwasaidia watoto badala ya kuchukua hatua kali zinazosukumwa na hasira.

BBC



Rais wa Marekani, Donald Trump ,akiwasili nchini Uingereza. **PICHA: REUTERS**

# Viongozi wa dunia kuadhimisha D-Day

LONDON, Uingereza

RAIS wa Marekani, Donald Trump ataungana na viongozi wa nchi 16 katika kuadhimisha miaka 75 tangu kuanza kwa operesheni ya kijeshi iliyoikomboa Ulaya kutoka mikononi mwa Wanazi wa Ujerumani, maarufu kama D-Day.

Rais Trump atakuwa pamoja na wenyeji wake, Malkia Elizabeth II na Waziri Mkuu Theresa May, na pia Kansela wa Ujerumani Angela Merkel katika maadhimisho hayo yanayofanyika katika mji wa Portsmouth Kusini mwa Uingereza.

Wakongwe 300 walioshiriki katika operesheni hiyo watahudhuria pia.

May 5, 1944, wanajeshi 170,000 wa nchi washirika walivuka bahari na kufika kwenye fukwe za Normandy nchini Ufaransa, ikawa mwanzo wa mwisho wa utawala wa Wanazi wa Ujerumani waliokuwa wameyakalia maeneo makubwa ya Ulaya katika vita vikuu vya pili.

Rais Trump anatarajiwa kutoa heshima kwa wanajeshi waliouawa katika vita hivyo, kabla ya kuondoka Uingereza akielekea Ireland.

Katika mkutano na waandishi wa habari juzi mjini London, Trump alisema anayo heshima kubwa kwa wanajeshi hao, aliowataja kama mashujaa walioijitolea maisha yao kuunusuru ustaarabu.

Alisema urafiki uliotengenezwa wakati wa operesheni hiyo, na kuimarishwa na damu iliyomwagika, utadumu milele.

Kansela wa Ujerumani Angela Merkel, Waziri Mkuu wa Canada Justin Trudeau na Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron ni miongoni mwa viongozi wengine watakaoshiriki katika maadhimisho hayo yanayoongozwa na May na Malkia Elisabeth II.

Mashambulizi yaliyoanza siku ya D-Day dhidi ya wanajeshi wa Ujerumani waliokuwa wakiikalia kimabavu Ufaransa, ndio operesheni kubwa zaidi ya kutokea baharini katika historia ya dunia.

Mashambulizi hayo yalitokea wakati sehemu kubwa ya wanajeshi wa Ujerumani wakipambana na Umoja wa Kisovieti sehemu ya Mashariki, operesheni hiyo iliyotokea Magharibi iligeuza mkondo wa vita ulioendelea hadi kuangushwa kwa Adolf Hitler na utawala wake wa kinazi.

*DW*

# Idadi wanaougua Ebola yafikia 2,000

**KINSHASA, Congo**

WIZARA ya Afya ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), imesema zaidi ya watu 2,000 wameripotiwa kuugua ugonjwa wa Ebola nchini humo katika kipindi cha miezi 10, huku theluthi mbili walikuwa kwenye hali mbaya zaidi.

Mlipuko wa ugonjwa wa Ebola ni wa pili kwa ukubwa nchini DRC, kukiwa na ripoti ya kutokea maambukizi mapya wiki za hivi karibuni.

Lakini wafanyakazi wa afya wamekua wakipata vikwazo vya kutoaminika na machafuko nchini humo.

Watu wengine hawawaamini watoa huduma za afya, hivyo hufanya watu wenye dalili za ugonjwa huo kukwepa matibabu, hali hiyo inawia vigumu kuzuia kuenea kwa virusi vya ebola.

Hadi sasa zaidi ya watu 1,300 wamepoteza maisha tangu Agosti, mwaka jana, Shirika la misaada la Oxfam linasema linakutana na watu kila siku ambao hawaamini kama kuna virusi vya ugonjwa wa ebola. Taarifa zaidi zinaeleza kuwa kati ya Januari hadi Mei kulikua na matukio 40 ya mashambulizi dhidi ya vituo vya afya, Hata hivyo machafuko yamepungua katika wiki za hivi karibuni.

Shirika la Afya Duniani (WHO), limesema kuwa hatari ya kusambaa zaidi kwa ugonjwa wa Ebora siyo kubwa sana, lakini inawezekana ugonjwa huo kuingia nchi jirani.

Mlipuko wa ebola mara nyingi husambaa haraka na kuathiri idadi ndogo ya watu

Ebola ni ugonjwa unaoambukizwa na virusi ambapo aliyepata maambukizi hupata dalili za homa, uchovu, maumivu ya viungo na koo. Kisha mgonjwa hutapika, kuharisha na kutoka damu.

Watu huambukizwa kwa njia ya kugusana, njia ya mdomo na pua, pia kwa njia ya damu, matapishi, kinyesi, majimaji ya kwenye mwili wa mtu mwenye Ebola

Wagonjwa hupoteza maisha kutokana na kupungukia maji mwilini na viungo kushindwa kufanya kazi.

*BBC*

# Sheikh ataka wahalifu 'Teleza' wafichuliwe

**Na Joctan Ngelly, KIGOMA**

SHEIKH wa Mkoa wa Kigoma, Hasan Kiburwa, amewataka wananchi wa mkoa huo kuhakikisha wanawafichua vijana ambao wanajipaka mafuta ya mawese na oili chafu maarufu 'Teleza' na kwenda kuwabaka wanawake katika maeneo ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji.

Kiburwa aliyasema hayo wakati akizungumza na Waislamu jana kwenye sikukuu ya Iddi iliyofanyika katika Shule ya Msingi Ujiji Manispaa ya Kigoma/Ujiji na kueleza kuwa huo ni uhalifu mpya ambao umezuka katika Manispaa hiyo na kila mmoja wao anatakiwa kuukemea.

Alisema uhalifu uliyozuka ni mbaya zaidi kwa sababu unaathiri mahusiano yao katika jamii na kuwafanya watu waishi kwa hofu, hasa kinamama kwa hofu ya kuingiliwa na watu wasiyojulikana na kuingiliwa kinaumbile kinyume cha sheria, uhalifu huo ni lazima upigwe vita na kulaaniwa.

Aidha, alisema watu wote wa dini ya Kislamu na Wakiristo washirikiane kutokomeza uhali huo kwa sababu unalenga kuangamiza jamii yao kwa kuwa kuwezi kujua huyo mtu anaekwenda kufanya uhalifu huo ni mgonjwa au siyo mgonjwa.

"Yule unaekwenda kumbaka ana maradhi au hana, kwa hiyo wewe ni chanzo cha kusambaza maradhi hayo," alisema.

Alisema jamii isiishi kwa woga bali watoe taarifa inapoonekana kwamba kuna watu wanafanya mambo hayo ili waweze kushughulikiwa kwa mujibu wa sheria kwa sababu kila mtu anaishi kwa kutii sheria.

"Bahati nzuri nchi yetu ina mifumo mizuri ya kisheria, hivyo watu wasiwe na uoga na mimi naamini watalindwa kwa taarifa zao za siri... wafanye hiyo kazi vizuri kwa ajili ya kutokomeza uhalifu huo, lakini si Teleza tu hata dada poa waachane na hizo biashara kwa sasa hazilipi, watakufa," alisisitiza Sheikh Kiburwa.

Aidha, aliwataka wananchi kujitahidi kutunza mazingira yao na kukataa matumizi ya mifuko ya plastiki ambayo haiozi kwa sababu inawaathiri watu pamoja na viumbe hai kwa sababu ya tamaa.

Alisema kila mwananchi anatakiwa kutumia mifuko iliyotangazwa na serikali kwa sasa ambayo ni salama na rafiki kwa mazingira yao.

Pia Sheikh huyo aliwataka waumini wa dini ya kiislamu waache tabia ya uovu wamalizapo mfungo wa Ramadhani, bali waendelee na matendo mema ambayo waliyafanya wakati wa Mfungo wa Ramadhani.



Mkuu wa Mipango wa Wakala wa Barabara nchini (Tanroads), Mkoa wa Manyara, Mhandisi Dutu Masele (kulia) na Mhasibu wa wakala huo, Julieth Kyaruzi, wakipanda mti kati ya miti 100 mjini Babati kuadhimisha Siku ya Mazingira Duniani juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Viongozi wa dini, serikali, wanafunzi wala Iddi pamoja

**Na Salome Kitomari**

VIONGOZI wa serikali kwa kushirikiana na viongozi wa dini ya Kiislamu wa Wilaya ya Ikungi mkoani Singida, wamesherehekea sikukuu ya Eid pamoja na wanafunzi wenye mahitaji maalum na walimu wa Shule ya Msingi Ikungi.

Chakula hicho kiliandaliwa kwa pamoja kati ya Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, Mwenyekiti wa CCM Wilaya na Mashehe wa wilaya hiyo kwa wanafunzi 30 wa shule hiyo.

Akizungumza baada ya chakula hicho, Mkuu wa wilaya hiyo, Miraji Mtaturu, alisema lengo la viongozi wa juu wa wilaya kula chakula pamoja na wanafunzi ni kuwafanya wajione ni watu muhimu sana kwa jamii.

Alisema jamii ya wenye mahitaji maalum wanahitaji kuangaliwa kwa jicho la pekee, ikiwamo kutoa kipaumbele kutatua changamoto zao nyingi zinazowakabilia.

Naye, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Ikungi, Justice Kijazi, alisema wanatoa kipaumbele kwa kundi hilo kwa kuwa wanatambua umuhimu wao na mchango kwa maendeleo yao binafsi na taifa kwa ujumla.

Alisema katika kutekeleza kwa vitendo halmashauri imetengeneza mashine nane za kuandikia watoto wenye mahitaji maalum, ikiwa ni pamoja na kuwapa karatasi maalum za kusomea na kutatua changamoto kubwa waliyokuwa nayo kwa muda mrefu.

Kijazi alisema malengo ya halmashauri ni kuwasaidia wanafunzi hao ili wasome bila kikwazo na kufikia ndoto zao maishani bila kujali changamoto za kimaumbile walizonazo.

"Tuko bega kwa bega kuwasaidia watoto wenye mahitaji maalum ili wasome kama watoto wengine wasio na changamoto za maumbile, tunaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya na kuhakikisha inawafikia kwa kutatua changamoto zozote zilizopo," alibainisha.

Wakizungumza mara baada ya chakula hicho, wanafunzi hao walipongeza uamuzi wa mkuu wa wilaya na mkurugenzi kuandaa chakula hicho kwa kuwa wamewajali na kuonyesha wanawapenda.

## TPA kurasimisha bandari bubu 73 Ziwa Victoria

**Na Mary Geofrey, MWANZA**

MAMLAKA ya Bandari Tanzania (TPA), kupitia Bandari ya Mwanza ipo kwenye mchakato wa kurasimisha bandari bubu 73 kati ya 342 zilizopo katika maeneo ya Ziwa Victoria.

Kaimu Meneja wa Bandari ya Mwanza, Geofrey Lwesya, aliyaeleza hayo juzi jijini Mwanza, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa miradi ya bandari katika Ziwa Victoria. Alisema walifanya ukaguzi katika maeneo yote ya bandari bubu kwa ajili ya kuzibaini na kutoa elimu kwa wananchi na kwamba kati ya hizo 73 zinafaa kurasimishwa na kuingizia serikali mapato.

"Kwa mujibu wa Sheria ya Bandari namba 17 ya mwaka 2004, TPA imepewa mamlaka ya kusimamia maeneo yote ambako meli zinashusha na kupakia mizigo hivyo kwa kutambua hilo, tulianza kubaini zilizopo kwanza, tukatoa elimu katika mikoa yote inayozunguka Ziwa Victoria na tayari tupo kwenye mchakato wa kuzirasimisha bandari bubu 73," alisema Lwesya.

Alisema shughuli za upakiaji na ushushaji wa mizigo kwenye meli, kusimamia na kufanya ukarabati wa miundombinu ya eneo la bandari ni kazi ambazo zinapaswa kufanywa na TPA katika bandari zote hivyo walitimiza wajibu wa kuzibaini ili zinazoweza kurasimishwa zitumike kwa manufaa ya taifa.

Lwesya alisema bandari nyingine bubu zimefungwa kwa lengo ya kuzirasimisha zile walizoona zinaweza kuwa na manufaa kwa watumiaji kwa kuzingatia mazingira ya eneo husika.

Alisema mbali na bandari hizo bubu, wanamiliki na kusimamia bandari kubwa za Mwanza Kaskazini, Mwanza Kusini, Nansio, Kemondo Bay, Bukoba na Musoma. Lwesya alisema pia zipo bandari ndogo ndogo ambazo zipo mwambao wa ziwa hilo ambazo ni Maisome, Kome, Bukondo, Kahunda, Nkome, Miharaba, Buchesi, Solima na Karumo, Ntama, Kanyala mkoani Mwanza.

Alitaja nyingine ni Chato na Kanyala mkoani Geita ni Kyamkwikwi na Magarini Mkoa wa Kagera na Shitari na Kenesi Mkoa wa Mara.

"Kati ya hizo zipo ambazo TPA imeshaanza kuziendeleza kwa kuzijengea miundombinu kama bandari ndogo za Ntama, Lashamba na Kyamkwikwi ambazo kuna miradi inayoendelea katika bandari hizo," alieleza.

Lwesya alisema pia katika mwaka huu wa fedha, kuna bandari ambazo zimepangiwa miradi ya uendelezaji wa miundombinu ambazo ni Nyamirembe, Magarini na Kasenda.

**TANGAZO**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MAGARI NA VIPURI**

**BASI LINAKODISHWA,** Basi aina Toyota HIACE dungu liko Dar linakodishwa kwenda mahali popote. Piga simu: 0784 316570 au 0754 316570 au 0715 316570 au 0629 316570.

**NAFASI ZA KAZI**

**SALES LADY ANAHITAJIKA,** SALES LADY ANAHITAJIKA MWENYE UZOEFU WA COMPUTER, MITANDAO YA KIJAMII INSTAGRAM NA FACEBOOK. KWA MAWASILIANO PIGA SIMU NAMBA: 0715 88 55 33

**MCHANGANYIKO**

**MONKALI INSULIN:** Inaponya maradhi mbalimbali sugu ya muda mrefu,inarejesha kongosho katika utoaji ute mchunguna kuwa normal balance 4.5.6 ipo ktk mfumo wa maji na vidonge husaidia mmengenyo wa chakula , tiba lishe, gaut, vidonda vya tumbo,bawasili, 0713293988/0758078280.

**MAGARI NA VIPURI**

**CRANE FUSO FOR SALE,**

(1.) Fighter 2002, SAKAI_340,3 stages, New in TZ,

2. Magnum 1991, TADANO_290, 2 Stages, 3 years in TZ.

**"Dalali Hatakiwi" Simu 0692 469 669**

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

**GOROFA INAUZWA**



**BOKI KAMWANGA STR LOW DENSITY AREA BLOC "C", PLOT NO. 65**

**SIMU**: 0754 226 687 / 0756 410 345.

115258002

**NAFASI ZA KAZI**

**MR SMART BARBERSHOP**

*Tunahitaji vinyozi wenye uzoefu na Wasichana wa kufanya huduma za saloon*

**kama scrub, mask n.k.** Tuma ujumbe mfupi kwenda **0629 069 552**

**Tunapatikana kona ya Sanawari- Arusha.**

115262402

***Uza, Chenye Thamani Kubwa***

***Kwa Kutangaza***

***Nasi Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0767 223 311***

## JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

# Nipashe

NI JIBU LAKO,

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz au piga simu: 0767223311**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# STURRIDGE, MORENO WAONDOKA LIVERPOOL

**LIVERPOOL, England**

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amewashukuru Daniel Sturridge na Alberto Moreno wakati wakitangaza kuondoka katika klabu hiyo ya Anfield wakiwa wachezaji huru.


Wachezaji hao mikataba yao imefikia mwisho na klabu hiyo haikuwa na mpango wa kuwaongezea na hivyo wameondoka wakiwa wachezaji huru.

Sturridge alijiunga na klabu hiyo akitokea Chelsea Januari mwaka 2013 na amefunga mabao 105 katika mechi 306 alizoichezea kwenye mashindano yote, huku Moreno akiwa amewasili hapo akitokea Sevilla mwaka 2014 na amecheza mechi 141.

Koch wa Liverpool, Klopp amewashukuru wawili hao na kuelezea kuwa Sturridge ni mmoja wa washambuliaji wamaliziaji bora zaidi ambao amewahi kuwashuhudia.

"Jambo la muhimu ni kwamba, nawashukuru wachezaji hawa wamekuwa kwenye kikosi kwa muda mrefu na wamefanya makubwa, nasema asanteni sana," alisema Klopp.

"Alberto ni mchezaji ninayemfahamu vizuri na nina uhakika atakokwenda kufanya vizuri zaidi."







# MAN UTD

## YAMTENGEA KOULIBALY PAUNI MIL. 95

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United, ipo tayari kutoa kiasi cha euro milioni 95 ili kumsajili beki wa kati, Kalidou Koulibaly, wakati kocha Ole Gunnar Solskjaer akitafuta namna ya kuimarisha kikosi chake hasa kwenye safu ya ulinzi.

Hata hivyo, klabu yake ya Napoli imeshabainisha wazi kwamba haina mpango wa kumuuza beki huyo raia wa Senegal.

Koulibaly amejipatia umaarufu zaidi na kuonekana kuwa mmoja wa mabeki bora duniani baada ya kuonyesha kiwango cha juu pale Napoli na ametajwa kuwa beki bora wa Serie A kwa msimu wa 2018/19.

Mchezaji huyo amekuwa nguzo kubwa ya Napoli na kukifanya kikosi hicho kucheza mechi 14 bila kuruhusu bao chini ya kocha wao, Carlo Ancelotti.

Msimu huu Napoli imemaliza katika nafasi ya pili kwenye msimamo ikiwa ni mara ya pili mfululizo.

Kwa muda mrefu amekuwa akiwaniwa na United na kwa mujibu wa Gazeti la Corriere dello Sport, 'Mashetani Wekundu' hao wapo tayari kutoa kiasi hicho cha euro milioni 95 ili kupata saini ya Koulibaly.

United imekua na mismu mbaya na sasa inataka kuimarisha kikosi chake kwani imemaliza katika nafasi ya sita kwenye msimamo wa Ligi Kuu msimu huu.

# Sevilla yamchukua kocha Real Madrid

**SEVILLA, Hispania**

KLABU ya Sevilla imethibitisha kwamba kocha wa zamani wa Real Madrid na timu ya Taifa ya Hispania, Julen Lopetegui atakuwa kocha wao mpya kwa msimu ujao wa 2019/20.

Baada ya Pablo Machin kuondoka, Sevilla, walikuwa wanatafuta kocha mpya na mwisho wa siku wamekamilisha dili la kumchukua Lopetegui, ambaye amekuwa hana kazi tangu alipoondoka Real Madrid Oktoba mwaka jana.

Sevilla ilithibitisha ujio wa kocha Lopetegui kupitia kwenye ukurasa wao wa twitter ikisema: "Sevilla FC na Julen Lopetegui Argote wamefikia makubaliano."

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 53, sasa anarudi kwenye benchi la ukocha baada ya kukaa nje kwa muda mfupi.

Kocha huyo aliwasili katika viunga vya Seville Jumanne na jana Jumatano alitambulishwa rasmi.

Lopetegui alianza kazi ya ukocha akiwa na Klabu ya Rayo Vallecano na baadaye Porto, na hivyo kupata nafasi ya kuitwa kuinoa timu ya Taifa ya Hispania.

Aliisaidia Hispania kufuzu kwa michuano ya Kombe la Dunia mwaka 2018, lakini hakupewa nafasi ya kuiongoza kwenye michuano hiyo, kwani alitimuliwa siku moja kabla ya kuanza kwa mashindano hayo.






# MOURINHO

## AMPIGIA CHEPUO SALAH TUZO YA BALLON D'OR

**LONDON, England**

KOCHA wa zamani wa Chelsea, Jose Mourinho anaamini Mohamed Salah ana ubora wa kuwania tuzo ya Ballon d'Or, lakini nyota huyo wa Liverpool anatakiwa kwanza kuliongoza taifa lake kutwaa ubingwa Afcon 2019.

Salah amekuwa mchezaji muhimu kwenye kikosi cha Jurgen Klopp ndani ya misimu miwili iliyopita ambapo aliibuka kuwa mfungaji bora mara zote mbili mfululizo huku 2017/18 akiwa mchezaji bora wa mwaka EPL.

Mkwaju wake wa penalti na shambulio lililoanzia kwake na kabla ya kumfikia Divock Origi aliyefunga bao la pili, viliifanya Liverpool kutwaa Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu wa 2018/19 kwa mara ya sita katika historia ya klabu hiyo.

"Salah anatakiwa kuchukua kombe la fainali za Mataifa ya Afrika ili aweze kushindana ipasavyo kwenye tuzo za Ballon d'Or," alisema Mourinho alipokuwa akizungumza na beIN Sports.

"Fainali zinafanyika nyumbani kwao, Misri atakuwa na nafasi kubwa ya kufanikiwa."

Tangu 2008 ni Cristiano Ronaldo na Lionel Messi, waliokuwa wakipishana kutwaa tuzo hiyo ya mchezaji bora wa dunia hadi mwaka jana ambapo Lukas Modric aliitwaa.

SALAH




# JOVIC

## AKAMILISHA USAJILI REAL MADRID

**MDRID, Hispania**

MSHAMBULIAJI Luka Jovic, amejiunga na Klabu ya Real Madrid kwa ada ya dau ya Euro milioni 62 na kupewa mkataba wa miaka mitano.

Mshambuliaji huyo ambaye alikuwa akiitumikia Klabu ya Eintracht Frankfurt amekuwa straika wa kwanza kusajiliwa kwa ada ya dau kubwa kuliko wote ambao wamewahi kusajiliwa klabuni hapo.

Lakini anakuwa mchezaji wa tatu kununuliwa kwa ada kubwa baada ya Cristiano Ronaldo na Gareth Bale.

Bosi wa timu yake ya zamani ya Eintracht Frankfurt, Fredi Bobic, amesema kuwa kuondoka kwa Jovic ni hasara kubwa kwao kutokana na mchango wake mkubwa ndani ya klabu.

"Kwetu sisi ipo wazi kabisa kwamba tutapata fedha ila bado kuna kitu ambacho tutakikosa kwake, tunamuombea Jovic mafanikio mema katika kuishi ndoto zake, tunajivunia uwepo wake kwetu na uwezo alioonyesha," alisema.

## Mwanamke aliyevamia fainali Uefa maarufu zaidi

**MADRID, Hispania**

MWANAMKE aliyeingia uwanjani nusu uchi katika pambano la fainali ya Ulaya kati ya Liverpool na Tottenham Uwanja wa Wanda Metropolitano amefahamika kuwa ni Kinsey Wolanski kutoka nchini Urusi.

Kinsey alisimamisha kwa muda pambano hilo baada ya kuingia uwanjani akiwatoroka walinzi wa uwanja ambao huwa wanajipanga vema kwa ajili ya kudhibiti mashabiki wanaoweza kuingia uwanjani.

Kamera ilimnasa kwa sekunde kadhaa kabla ya kugeukia wachezaji wengine.

Kinsey amefahamika ni mrembo ambaye anafanya masuala yake katika mtandao wa Instagram na aliingia uwanjani na nguo ya kuogelea ambayo ilikuwa imeandikwa jina la 'Vitaly Uncensored' akitangaza mtandao wa Youtube wa mpenzi wake wa kiume, Vitaly Zdorovetskiy ambaye ni maarufu kwa kumiliki akaunti ya mtandao wa Youtube iitwayo Vitalytv.

Kutokana na kitendo chake cha kuingia uwanjani huku umbo lake likiwa na mvuto kwa watazamaji, akaunti ya Instagram ya Kinsley iliyokuwa na mashabiki 230, 000 iliongezeka wafuasi kufikia zaidi ya milioni mbili.

Baadaye aliandika katika mtandao wake wa Youtube akidai "kuvamia uwanja wa Ligi ya Mabingwa, maisha yapo kwa ajili ya kuishi, kufanya vitu vya kiwehu ambavyo utavikumbuka kwa maisha yako yote."

Wolanski anadai alishikiliwa na polisi kwa saa tano kabla ya kuachiwa, lakini kabla ya hapo walihakikisha kwa muda wote aliokuwa katika kituo chao alikuwa amejifunika mwili wake vyema tofauti na awali.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MBAPPE AOMBA KUONDOKA PSG

●●●Safari ya Madrid sasa yanukia, adaiwa kuwasilisha ombi rasmi baada ya awali kufunguka kuwa...

**PARIS, Ufaransa**

KYLIAN Mbappe anatafuta "mradi mpya" mbali na Paris Saint-Germain, na sasa inaonekana kama mvuke umeanza kujikusanya katika mpango huo.

Nyota huyo wa PSG mwenye umri wa miaka 20, alifurahia msimu mwingine mzuri hapo kwa mabingwa wa Ligue 1, akifunga mabao 39 katika mechi 43 za mashindano yote alizocheza.

Lakini nyota huyo wa kimataifa wa Ufaransa alijiweka katika mkao wa kusikilizia mustakabali wake wa baadaye mwezi uliopita wakati alipofunguka kuhusu kuondoka Paris.

Na taarifa kutoka Hispania sasa zinadai kuwa Mbappe anaweza kuwa amepiga hatua karibu ya kutua Real Madrid ambapo amekuwa akiendelea kuhusishwa nako.

**AOMBA KUONDOKA**

Mbappe anataka kuondoka PSG baada ya kuwasilisha ombi la kuondoka, kwa mujibu wa TV ya Hispania El Chiringuito.Real Madrid imekuwa ikihusishwa sana na kutaka kumsajili mshambuliaji huyo, na zaidi tangu nguli wa Ufaransa, Zinedine Zidane kurejea klabuni hapo.

Lakini inaonekana Madrid imenyoosha mikono juu katika kujaribu kumsajili mchezaji mwenza wa Mbappe, Neymar, kwa mujibu wa AS.

Ikiwa tayari imeanza kujijenga imefanikiwa mbio za kumsajili mshambuliaji Luka Jovic na Eden Hazard anaonekana kuwa njiani, Madrid pia ipo tayari kusikiliza ofa kwa Isco, kwa mujibu wa Marca.

**KWINGINEKO**

Real Madrid, hata hivyo inaweza kumkosa Christian Eriksen, na tayari Gazeti la The Mirror limeripoti kuwa Mwenyekiti wa Tottenham, Daniel Levy ameiambia klabu hiyo ya La Liga kwamba Spurs haina mpango wa kumuuza kiungo huyo.

The Mirror pia limeripoti kuwa kiungo wa Real Betis, Giovani Lo Celso anajaribu kulazimisha kwenda kujiunga na wanafainali hao wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, Spurs.

## KWA UFUPI

### BECKHAM AMTAKA SUAREZ MLS

NAHODHA wa zamani wa England, David Beckham, anataka kumsajili straika wa Barcelona na Uruguay, Luis Suarez, 32, katika klabu yake mpya wa MLS, Inter Miami. ***(Be Soccer)***

### BAJETI ARSENAL KUSAJILI WAWILI TU

KOCHA wa Arsenal, Unai Emery, yupo tayari kutumia bajeti yake yote, kiasi cha pauni milioni 40 kwa kusajili wachezaji wawili tu wote kutoka Sampdoria, Kiungo Mbelgiji Dennis Praet, 25, na beki Mdenmark Joachim Andersen, 23. ***(Sun)***

### MADDISON AKUSANYA VIGOGO EPL

LIVERPOOL, Manchester City, Manchester United na Tottenham zote zinavutiwa kwenda kumsajili kiungo wa Leicester City, Muingereza James Maddison, 22, kwa pauni milioni 60. (Star)

### HUDSON-ODOI AITESA CHELSEA

CHELSEA inaamini mshambuliaji wao Muingereza Callum Hudson-Odoi, 18, atasaini mkataba mpya utakaomwezesha kulipwa pauni milioni 100,000 kwa wiki hapo Stamford Bridge, licha ya kuivutia Bayern Munich. ***(Mirror)***

### CITY YAMPANDISHA DAU FELIX

MANCHESTER City imesababisha kuwapo kwa kifungu kinachomtaka Joao Felix, 19, kuuvunja mkataba wake kwa pauni milioni 106 kama mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Ureno anataka kuondoka Benfica. ***(Sun)***

### POGBA, DYBALA KUPISHANA

Juventus imewasiliana na Manchester United kuhusu uwezekano wa kumsajili kwa mara nyingine kiungo Paul Pogba. Kiungo huyo wa kimataifa wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 26, ameonyesha ishara kuwa atakuwa na furaha kama atajiunga tena na mabingwa hao wa Serie A, ambapo alidumu kwa miaka minne kuanzia mwaka 2012-2016, lakini uwezekano wa kumpata ni endapo wataafikiana kumjumuisha Muargentina Paulo Dybala, 25 katika dili hilo. ***(The Guardian and Express)***

### LIVER NAYO KWA DE LIGT

LIVERPOOL imejiunga katika mbio za kumsajili beki wa Ajax na Uholanzi, Matthijs de Ligt. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19, pia anawindwa na Manchester United na Barcelona. ***(Bild - in German)***

### LJUNGBERG KUMSAIDIA EMERY ARSENAL

KIUNGO wa zamani wa Arsenal, Freddie Ljungberg, anajiandaa kujiunga katika benchi la ukocha la kikosi cha kwanza cha Unai Emery hapo Emirates msimu ujao. ***(Times)***

### ERIKSEN AWEKEWA NGUMU SPURS

MWENYEKITI wa Tottenham, Daniel Levy, ameiambia Real Madrid kuwa kiungo Mdenmark, Christian Eriksen, 27, hauzwi majira haya ya joto. ***(Mirror)***

### RODRIGO AISHUKIA ATLETICO

KIUNGO Mhispania Rodrigo, 28, ameitaka Atletico Madrid "kumpa nafasi" wakati huu kukiwa na taarifa za Manchester City kuvutiwa naye. ***(Deportes Cuatro, via Goal)***

### JAMES SASA ANUKIA UNITED

MANCHESTER United inakaribia kuchomoza katika mchakato wake wa kuinasa saini ya winga wa Swansea na Wales, Daniel James, 21, wakati huu AS Monaco pia ikieleza kuvutiwa naye. ***(Standard)***

### UNITED YATOA OFA KWA KOULIBALY

MANCHESTER United imetoa ofa ya pauni milioni 84 kwa beki wa kati wa Napoli na Senegal, Kalidou Koulibaly, 27. ***(Corriere dello Sport, via Metro)***

### CELSO ATAKA KUTUA TOTTENHAM

KIUNGO wa Real Betis na Argentina, Giovani lo Celso, 23, anataka kujiunga na Tottenham. ***(Sky Sports)***

## HABARI MICHEZO

# WADAU WAFUNGUKA TANZANIA KUPELEKA TIMU 4 MICHUANO CAF

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya Shirikisho la Soka Afrika (Caf), kuthibitisha kuwa Tanzania Bara itawakilishwa na timu nne kwenye michuano ya kimataifa, mbili Ligi ya Mabingwa na mbili Kombe la Shirikisho Afrika, wadau wa soka nchini wamesema ongezeko hilo litaongeza ushindani mkali kwenye Ligi Kuu msimu ujao.

Taarifa kutoka Caf zilizotua Shirikisho la Soka nchini (TFF) juzi na kusambazwa kwa vyombo vya habari, zilieleza katika msimu mpya wa 2019/2020 Tanzania Bara itawakilishwa na timu mbili katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na nyingine mbili kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho kutokana na kushika nafasi ya 12 bora kwenye viwango vya ubora vya Shirikisho la Soka Afrika.

Na kwa mujibu wa Kanuni za Ligi Kuu zilizofanyiwa marekebisho na Kamati ya Utendaji baada ya kupatikana nafasi nne, timu za Tanzania zitakazoiwakilisha nchini kwenye mashindano hayo ni Simba na Yanga ambazo zitapeperusha bendera hiyo Ligi ya Mabingwa (Caf CL), huku Azam FC na KMC zikiiwakilisha nchi Kombe la Shirikisho (Caf CC).

Shija Richard, Mjumbe wa Kuteuliwa wa Kamati ya Utendaji ya Yanga, aliliambia gazeti hili kuwa sasa timu zitakuwa zinapambana kuhakikisha zinamaliza katika nafasi tatu za juu kwa sababu ya kuwania tiketi za kushiriki mashindano hayo ya kimataifa.

Richard alisema kuwa hii itasaidia kuwaimarisha wachezaji kwa sababu kila mmoja atataka kuona ndoto zake za kushiriki michuano ya kimataifa na kuitwa katika kikosi cha Timu ya Taifa ( Taifa Stars) zinatimia.

Katibu Mkuu wa zamani wa Yanga, Jonas Tiboroha, kwa upande wake aliema klabu zote zilizopata nafasi hii zihakikishe zinajipanga kufanya vizuri ili kutoipoteza fursa hii iliyopatikana.

Tiboroha alisema kwa Tanzania Bara kutoa timu nne katika mashindano hayo ya kimataifa, inamaana wachezaji wetu watapata nafasi zaidi ya kuonekana na makocha na mawakala mbalimbali ambao wanafuatilia michuano hiyo ya Caf.

"Tunaposema Simba ni Timu ya Taifa tunamaana hii, kupeleka timu nne katika mashindano ya kimataifa si mchezo. Simba ipewe nishani ya Uhuru ya Uzalendo uliotukuka. Eid Mubarak," alisema Mbunge wa Kigoma Mjini, Zitto Kabwe.

Mafanikio ya Simba kucheza hatua ya robo fainali katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu uliomalizika, ndio yameifanya Tanzania kuwa kwenye nafasi 12 bora kutokana na kuiwezesha Tanzania kufikisha pointi 18 kutoka alama tatu zilizopatikana kutokana na Yanga kushiriki michuano hiyo kwa zaidi ya misimu minne bila mafanikio ya juu.

**TUNAWAKILISHA...**



Wawakilishi wa Tanzania kwenye michuano ya Castle Lager Africa 5s, timu ya Four Ways FC na Girls Queens wakiwa katika mazoezi ya pamoja Upanga jijini Dar es Salaam jana kuelekea michuano hiyo inayotarajiwa kuanza Ijumaa wiki hii katika Uwanja wa Uhuru.
**MPIGAPICHA WETU**

# Eto'o kuwashuhudia Kiba, Nandy, Harmonize Castle Lager Africa 5s

**Na Mwandishi Wetu**

WASANII wa muziki wa kizazi kipya nchini, Ally Kiba, Faustina Charles('Nandy Kivuruge') na Rajabu Abdul('Harmonize') watakutana katika jukwaa moja kwenye Uwanja wa Uhuru ('Shamba la Bibi') wakati wa kutoa burudani kwenye fainali za mashindano ya Castle Lager yajulikanayo kama "Castle Africa 5s(5- aside) Jumamosi wiki hii wakati wa mechi ya fainali ya michuano hiyo.

Fainali hizo ambazo zitaanza Ijumaa wiki hii katika Uwanja wa Uhuru, Tanzania ikiwa mwenyeji, zitashirikisha nchi nane kutoka Afrika huku kila moja ikiwakilishwa na timu za wanaume na wanawake.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Meneja wa Bia ya Castle Lager nchini Tanzania, Pamela Kikuli, alisema timu kutoka nchi saba zikiwakilishwa na timu ya wanaume na wanawake zinatarajiwa kuwasili nchini leo kuanzia asubuhi ambapo watazipokea kwa namna tofauti kwa kadri zitakavyokuwa zikiwasili katika Uwanja wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam pamoja na Balozi wa Castle Africa 5s, Samwel Eto'o.

Pamela alizitaja nchi shiriki katika fainali hizo kuwa ni Africa Kusini, Zambia, Zimbabwe, Swaziland, Lethoto, Uganda, wenyeji Tanzania na nchi alikwa ya Nigeria.

Naye Balozi wa Castle Africa 5s nchini Tanzania, Ivo Mapunda, alizitaja timu zitakazoiwakilisha Tanzania kuwa ni Four Ways FC yenye makazi yake Kinondoni na Girls Queens yenye ya Msimbazi Kariakoo.

Mapunda alisema timu zimejiandaa vizuri kiushindani na zimeahidi ushindi utabaki Tanzania hivyo anaomba Watanzania wajitokeze kwa wingi kuzishangilia timu zao.

## Ndayiragije bado kiduchu Azam FC

**Na Mwandishi Wetu**

SIKU na saa sasa zinahesabika kwa Kocha Mkuu wa KMC FC, Etienne Ndayiragije, kujiunga na Azam FC baada ya mabosi wa Kombe la FA kusema kuwa wako katika hatua za mwisho za mazungumzo na kocha huyo, imeelezwa.

Nipashe iliwahi kuandika taarifa za Ndayiragije kufanya mazungumzo na Azam FC mapema Aprili mwaka huu, na kocha huyo raia wa Burundi akasema kwamba atakuwa katika nafasi nzuri ya kuzungumza baada ya kumaliza mkataba na KMC.

Tayari Ndayiragije amemaliza mkataba wa kuifundisha KMC na sasa anakaribia kusaini mkataba na Azam FC ambayo mwakani itashiriki mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin "Popat" alisema anaamini mazungumzo yao yatakamilika na wataanza msimu ujao wakiwa na Mrundi huyo ambaye mara ya kwanza alianza kuifundisha Mbao FC ya jijini Mwanza.

Popat alisema kuwa klabu yao imejipanga kuimarisha kikosi chao na benchi la ufundi ili wafanye vema katika Ligi Kuu Tanzania Bara msimu 2019/20 na mashindano yote ya kimataifa watakayoshiriki.

"Ni kweli tuko katika mazungumzo na Ndayiragije, tutakapokamilisha tutaweka wazi, tunaamini ni mtu sahihi atakayeweza kutupa kile tunachokitafuta," alisema kiongozi huyo.

## Mwakyembe mgeni Akhwari marathon

**Na Woinde Shizza, Arusha**

Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe anatarajiwa kufungua rasmi mashindano ya mbio za wazi zijulikanazo kama John Stephen Akhwari, zinazotarajiwa kufanyika Juni 9, mwaka huu katika viwanja vya Kumbukumbu ya Sheikh Amri Abed jiji Arusha.

Mashindano hayo ambayo yanafanyika kwa mara ya kwanza jijini Arusha, yanatarajiwa kushirikisha wanariadha kutoka klabu mbalimbali ndani na nje ya nchi ikiwamo klabu za Jeshi la Polisi, Magereza na JKT.

Mkurugenzi wa mbio hizo, Sylvester Orao alisema jana kuwa maandalizi yanaendelea vizuri na lengo la mashindano hayo ni kumuenzi mwanariadha wa zamani wa Tanzania, John Stephen Akhwari, pamoja na kuinua vipaji za wanariadha chipukizi sambamba na kuvitangaza vivutio vya utalii vilivyopo nchini.

Alisema Dk. Mwakyembe atakuwa mgeni rasmi katika hafla ya kufungua mbio hizo huku akifafanua kuwa mbali na waziri pia wanatarajia wageni mbalimbali wakiwamo wanariadha wa zamani kama Juma Ikangaa, Gilbert Bayi na wengine wengi na kwamba kiingilio kitakuwa ni Sh. 15, 000.

Michezo
Alhamisi Juni 6, 2019
Nipashe




## Mbappe aomba kuondoka PSG

HABARI UK 30

HICHO...



Harry Kane akijaribu kufunga kwa kichwa wakati wa mazoezi na wachezaji wenzake wa timu ya Taifa ya England, kabla ya kukwea pipa jana kuifuata Uholanzi kwenye mechi yao ya nusu fainali ya Ligi ya Mataifa ya Ulaya ['Nations League'], itakayopigwa leo nchini humo. England leo itamkosa Jordan Henderson. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA YATOA NENO LIGI YA MABINGWA

●●●Ni baada ya Caf kubariki kupanda ndege kushiriki msimu ujao, wasema usajili sasa utakuwa...

**Na Somoe Ng'itu**

HISTORIA itaandikwa! Hayo ni maneno kutoka kwa uongozi wa Yanga ya jijini Dar es Salaam baada ya timu yao kupata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao pasipo kutarajia.

Rasmi sasa Yanga itaungana na mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, kupeperusha bendera ya nchi katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika huku Azam FC na KMC FC wakielekea kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka Caf zilizotua Shirikisho la Soka nchini (TFF) juzi na kusambazwa kwa vyombo vya habari, zilieleza msimu mpya wa 2019/2020 Tanzania Bara itawakilishwa na timu mbili katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na nyingine mbili kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho kutokana na kushika nafasi ya 12 bora kwenye viwango vya ubora vya Shirikisho la Soka Afrika.

Na kwa mujibu wa Kanuni za Ligi Kuu zilizofanyiwa marekebisho na Kamati ya Utendaji baada ya kupatikana nafasi nne, timu za Tanzania zitakazoiwakilisha nchi kwenye mashindano hayo ni Simba na Yanga ambazo zitapeperusha bendera hiyo Ligi ya Mabingwa (Caf CL), huku Azam FC na KMC zikiiwakilisha nchi Kombe la Shirikisho (Caf CC).

Akizungumza na gazeti hili jana, Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Frederick Mwakalebela, alisema kabla ya kupata tiketi hiyo ya kushiriki mashindano hayo yanayoandaliwa na Caf, uongozi wa Yanga ulidhamiria kujipanga ili kikosi chao kipate mafanikio ambayo hayajawahi kufikiwa kwa miaka ya nyuma.

Mwakalebela alisema kufanya vema katika mashindano yote katika msimu ujao ndio malengo yao makubwa na hilo limechangia kuanza kusajili wachezaji wenye viwango vya juu na uzoefu wa kupambana katika ngazi ya kimataifa.

"Kiukweli tunakiimarisha kikosi chetu kwa kusajili wachezaji wa kiwango cha juu na wenye kuweza kutoa ushindani, kama mnavyoshuhudia, tunajua kufanya hivi ni kutekeleza matakwa ya mwalimu, hapo jukumu litabakia kwake," alisema Mwakalebela.

Alisema pia wamejipanga kuitendea haki nafasi waliyoipata na kuipa heshima nchi na kamwe hawatakwenda kukamilisha ratiba.

"Miaka miwili iliyopita tuliteleza, tulikuwa na changamoto mbalimbali, hatutaki kuona tunarejea huko, tunajipanga kuandika historia mpya, tunaamini kombe litakuja nyumbani," alisema Mwakalebela, Katibu Mkuu wa zamani wa TFF.

Aliongeza kuwa taarifa za kurejea katika mashindano ya Caf wamezipokea kwa furaha wao viongozi, wachezaji, benchi la ufundi na wanachama wa klabu hiyo.

"Sisi tumefurahi, Zahera pia amefurahi, kilichobaki ni kujipanga ili tusiwaangushe waliotuamini," alisema kiongozi huyo.

Katika kuonyesha Yanga imedhamiria kufanya kweli, mchakato wake wa kusajili nyota wapya umekuwa wa kasi ukilinganisha na watani zao, Simba ambao ndio wameleta mafanikio hayo hadi kutolewa kwa nafasi nne kufuatia msimu wa 2018/19 kutinga robo fainali ya Ligi ya Mabingwa ambapo katika michuano hiyo iliiwezesha Tanzania kuvuna pointi 15 na kuifanya kufikisha jumla ya alama 18 hivyo kukwea hadi nafasi 12 za ubora kwenye ngazi ya klabu.

Simba ambayo katika michuano hiyo ilitolewa hatua ya robo fainali na TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo ( DRC), ilipata mafanikio makubwa ukilinganisha na Yanga ambayo kwa zaidi ya misimu minne iliyoshiriki michuano hiyo, iliiwezesha nchi kuvuna pointi tatu tu.

Yanga pia imealikwa kushiriki katika mashindano ya Klabu Bingwa Afrika Mashariki na Kati maarufu Kombe la Kagame ambayo yanatarajiwa kufanyika kuanzia Julai 7 hadi 21, mwaka huu jijini Kigali, Rwanda.

## Mourinho ameguzia Salah tuzo Ballon d'Or



**LONDON, England**

KOCHA wa zamani wa Chelsea, Jose Mourinho anaamini Mohamed Salah ana ubora wa kuwania tuzo ya Ballon d'Or, lakini nyota huyo wa Liverpool anatakiwa kwanza kuiongoza taifa lake kutwaa ubingwa Afcon 2019.

Salah amekuwa mchezaji muhimu kwenye kikosi cha Jurgen Klopp ndani ya misimu miwili iliyopita ambapo aliibuka kuwa mfungaji bora mara zote mbili mfululizo huku 2017/18 akiwa mchezaji bora wa mwaka EPL.

UK. 29

## Koulibaly atengewa pauni mil. 95 United




**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United, ipo tayari kutoa kiasi cha euro milioni 95 ili kumsajili beki wa kati, Kalidou Koulibaly, wakati kocha Ole Gunnar Solskjaer akitafuta namna ya kuimarisha kikosi chake hasa kwenye safu ya ulinzi.

Hata hivyo, klabu yake ya Napoli imeshabainisha wazi kwamba haina mpango wa kumuuza beki huyo raia wa Senegal.

UK. 28

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >